BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kwanza - Tarehe 27 Septemba, 2017

WIMBO WA TAIFA

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

TAARIFA YA NAIBU SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa Saba wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 27/9/2017.

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kutoa taarifa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza la Wawakilishi, uliofanyika kuanzia tarehe 10 Mei, 2017 mpaka tarehe 13 Juni, 2017. Katika Mkutano wa Sita wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza hili lilipitisha Miswada mitano ya Sheria ambayo ni:

1. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015.

2. Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi *Trillion* 1,087,359,400,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2018 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3. Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

4. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa *Stamp* na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo na kufuata Sheria ya Ushuru wa *Stamp* Nam. 6 ya Mwaka 1966.

5. Mswada wa Sheria ya Kuweka Vifungu vya Uanzishaji wa Kodi itakayojulikana kama Ushuru wa Bidhaa na Huduma Zinazoingizwa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe, kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo 2016, naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo yote niliyoitaja sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 24 Juni, 2017.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hati ya Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria na Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam.3 ya 1985 na

Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine yanayohusiana na hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 59

Maafa Kipindi cha Mvua za Masika

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:

Kila mwaka wakati wa mvua za masika, sehemu nyingi za Zanzibar kumekuwa na tatizo la mafuriko na kuleta maafa kwa wananchi na kuharibu miundombinu muhimu ya nchi.

(a) Kwa kuwa sehemu kubwa ya maafa hayo husababishwa na ujenzi holela. Je, serikali ina mpango gani kumaliza tatizo hilo na kuacha kufumbia macho wanaojenga sehemu zilizokatazwa.

(b) Katika msimu wa masika wa 2016/2017, serikali imepata hasara kiasi gani kutokana na kuharibika miundombinu na pia uharibifu wa nyumba za watu umesababisha hasara ya kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, nchi yetu kwa miaka mitatu iliyopita imekuwa ikipata mvua kubwa hasa katika msimu wa mvua za masika. Mvua hizo zimekuwa zikileta athari kubwa kwa wananchi wetu hasa wale wanaoishi katika maeneo hatarishi (mabondeni na kwenye njia asili za maji). Kutokana na hali hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuunda Kamati ya Kitaalamu ya kubaini sababu zinazopelekea Zanzibar kuathiriwa na mvua za masika na kuishauri juu ya hatua zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na athari za hali hiyo.

Kamati hiyo tayari imeshawasilisha ripoti serikalini na kutoa mapendekezo yake, moja kati ya hatua zinazochukuliwa na serikali ni kuendelea na kutayarisha kanuni na miongozo ya ujenzi katika maeneo ambayo

hayakupimwa rasmi, ili kuwawezesha wananchi kujenga nyumba bora katika maeneo salama kulingana na mazingira ya eneo husika, na kuepusha ujenzi holela katika maeneo hatarishi ya mabondeni na njia za asili za maji. Aidha, serikali itasimamia ipasavyo sheria zote zinazohusiana na masuala ya maafa, ili kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa sheria hizo katika kukabiliana na maafa.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli mvua zilizonyesha katika msimu wa Masika wa 2016/2017 zilisababisha hasara kubwa ikiwa ni pamoja na vifo vya watu takriban kumi na mbili (12), kuathiri nyumba za makaazi zipatazo 6,005, kuharibika kwa miundombinu ya barabara na madaraja, kuporomoka kwa milima hasa Kisiwani Pemba katika Wilaya ya Mkoani, kudidimia kwa baadhi ya maeneo pamoja na kuathirika kwa maeneo na mazao ya kilimo, ambapo jumla ya heka 2,823 za mazao mbali mbali yenye thamani ya shilingi 5,400,750,500/= zimeathirika kwa Unguja na Pemba.

Kutokana na athari hizo zilizojitokeza serikali ilitumia kiasi cha shilingi 290,450,000/= za kitanzania. Kati ya hizo shilingi 219,000,000/= zilitumika kufanya matengenezo ya dharura ya miundombimu ya barabara katika Kisiwa cha Pemba na shilingi 71,450,000/= zilitumika kusaidia wananchi walioathirika na mvua na upepo kwa Unguja na Pemba.

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Saada Ramadhan Mwenda: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni lini serikali itatoa muongozo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwenda swali lake la nyongeza kama ifutavyo.

Lini serikali itatoa muongozo. Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi kwamba tayari Kamati ya Kitaalam imeshawasilisha baadhi ya mapendekezo yake na hoja zake serikali. Hivyo, serikali sasa imesharidhia baadhi ya mapendekezo yaliyowasilishwa na Kamati ya Kitaalamu.

Jukumu litakalofuata kwanza ni kutangaza yale maeneo yaliyokuwepo katika hatarishi hasa maeneo ya asili yaliyokuwa yakipita maji, kama kwamba kutatoka

tangazo na badhi ya hatua zitachulikuwa kunusuru vizazi vya sasa na vya baadaye, ili kuwanusuru wananchi wetu kuondoka katika maeneo hayo.

Lakini, elimu itatolewa na kwa sasa elimu imeshaanza kutolewa kupitia Kamisheni yetu ya Maafa, kupitia wizara na taasisi zote zinazohusinana na kadhia hiyo. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza suala moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba taaluma wanatoa lakini hadi sasa kuna wananchi wanajitoa mishipa ya fahamu katika kujenga ujenzi holela na kuzuia njia hizi za maji.

Je, wizara yake ina mpango gani kuhakikisha kufuatilia shehia kwa shehia, ili kukomesha suala hili la kuisababishia serikali hasara kubwa yanapotokea maafa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwanza hili ni jukumu letu sote sio la kuiachia serikali tu. Serikali Kuu, *local government* pamoja na ngazi za chini, ndio maana ukitizama katika *chain* ya Kamati za Maafa zimeanza katika ngazi ya shehia. Kwa maana hiyo, sote viongozi wakuu hata sisi tuliomo ndani kwa kupitia katika maeneo yetu kwa kupitia katika Kamati za Maafa na Shehia tuna wajibu wa kuweza kulinusuru na kutoa elimu hii.

Serikali inachoendelea kukifanya ni kutoa muongozo na kusimamia kile ambacho itaweza kutoa, kama ambavyo nimesema serikali itakuja kutangaza maeneo yote ambayo yamekuwa yakikithiri inapotokea mvu hizi za masika. Kwa hiyo, itakapotokea hili tutaomba sana Waheshimiwa Wajumbe taasisi zote zinazohusika kudhibiti na kulinda maeneo haya, tushirikiane lazima tuweze kunusuru watu wetu na kadhia hii.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Kamishna au Mkurugenzi wa Maafa ambaye ni mchapa kazi anaweza kuingia katika mazingira yoyote katika kutafuta mambo ambayo ni usalama katika nchi yetu swali langu lipo hapa. *(Makofi)*

Wakati wa amani kama tuliokuwa nao sasa hivi, ni wakati wa kutathmini kupita maeneo yote ya hatarishi, ili wananchi wajue inapotokea maafa ya mvua wawe wameshapewa maelezo.

Je, wizara kupitia Mkurugenzi wa Maafa ina mpango gani wa kutembelea katika maeneo mbali mbali ya hatararishi, hasa kwa upande wangu mimi Jimbo la Kijitoupele, ambalo linapata maafa mengi siku za mvua na kusababisha wananchi wengi kukosa amani na kushindwa kuishi katika nyumba zao. Hivyo, ana mpango gani wa kutembelea katika maeneo hayo na mimi namkaribisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba kwanza tayari serikali imeshakagua maeneo yote hatarishi, wizara imefanya hivyo, kamisheni imefanya hivyo lakini hata Kamati ya Wataalamu iliyowahusisha watu watu tofauti kutoka katika taasisi tofauti za serikali na hata za binafsi imeshakagua maeneo yote.

Kwa hiyo, yale maeneo anayoyaona Mhe. Mjumbe ya Kijitoupele, maeneo ya Maziwamaboga, Kinuni, Nyarugusu na baadhi ya maeneo mengine yote hatarishi. Hivyo, tumhakikishie tu Mhe. Mjumbe kwamba kazi hiyo tayari imeshafanywa na ripoti tayari imeshawasilishwa serikalini. Kutokana na hali hiyo, kinachofuata sasa ni kuanza utekelezaji wa kile ambacho wataalamu wetu wameweza kushauri kwa upande wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema sana utakapofika wakati wa utekelezaji, tulikuwa tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja katika nafasi yake na taasisi anayotoka tuweze kusaidiana katika kuhakikisha tunalitekeleza lile, ili kunusuru vizazi vya leo na vya baadaye katika majenzi na katika maeneo. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Wanu Hafidh Ameir, hatukusikii mitambo ina matatizo kidogo, naomba uende kwa Mhe. Saada Ramadhan Mwenda. Mhe. Mjumbe, lazima tupate *hansard* yako, hivyo usogee katika kipaza sauti chengine

Nam. 7

Malipo ya Kiinua Mgongo na Pencheni

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:

Moja ni malipo yanayolipwa moja kwa moja na Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo yanawahusu wale watumishi walioajiriwa kabla ya Juni, 1998 wakati aina ya pili ni yale yanayolipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, yaliyoanzia Julai, 1998.

(a) Je, hadi kufikia Disemba, 2017 ni watumishi wangapi ambao bado watakuwa wapo kwenye utumishi na ambao wanastahiki kulipwa Kiinua Mgongo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

(b) Kwa kuwa, malipo yanayolipwa na Wizara ya Fedha na Mipango muda wake wa utumishi kwa mfanyakazi hauongezeki tena. Je, ni kwa nini serikali haitoi nafasi ya hiari kwa wale watumishi ambao wanastahiki malipo yao kupitia utaratibu huo kulipwa kabisa kiinua mgongo chao badala ya kusubiri kufikia muda wa kustaafu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir, swali lake Nam, 7 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, jumla ya watumishi 10,760 watakuwa wapo kwenye utumishi wa umma hadi kufikia Disemba 2017, ambao watastahiki kulipwa kiinua mgongo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

(b) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ni Mfuko wa Pencheni, ambao lengo lake kuu ni kulipa pencheni na viinua mgongo kwa wastaafu. Mfuko huo unaongozwa na Sheria nambari 2 ya mwaka 2005 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016. Hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, mwanachama anapaswa kulipwa mafao yake kwa

uanachama wake. Kwa maana hiyo, ili mwanachama alipwe mafao yake anahitaji kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Awe ametimia umri wa kustaafu na awe amestafu kazi
2. Awe amepata tatizo la kiafya ambalo litamuondolea uwezo wa kufanyanya kazi, au
3. Iwapo mwanachama atafariki.

Kutokana na muongozo huo hakutakuwa na malipo ya kiinua mgongo kwa mtumishi wa umma, ambaye hatakuwa ametiza vigezo vilivyotajwa hapo juu. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali langu nadhani ni vizuri watu wa *technician* kuangalia hizi *microphones* kabla ya Baraza halijaanza, ili wawe wanazirekebisha hizi *amberassment* ambazo zinatokea.

Swali langu ni kwamba pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo amejibu lakini katika swali langu la (b) niliuliza *specifical* wale ambao wameajiriwa hadi kufika kabla ya Juni, 1998. Lakini yeye amenijibu pamoja na kwamba amenifafanulia sheria na vifungu vya sifa, amenijibu wale ambao wanalipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naulizia wale ambao waloajiriwa kabla ya Juni 1998. Kwa hivyo, swali langu (b) linabaki pale pale kwa kuwa malipo yanayolipwa na Wizara ya Fedha na Mipango muda wake wa utumishi kwa mfanyakazi hauongezeki tena. Je, serikali haioni haja sasa ya kwamba kupitia Wizara ya Fedha na Mipango wakawalipa wale ambao wanakaribia kustaafu, yaani wakawalipa kiinua mgongo chao moja kwa moja ili wakamalizana nao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba swali (a) lilikuwa linahitaji kujua hadi kufikia Disemba, 2017 ni watumishi wangapi ambao bado watakuwa

wapo kwenye Utumishi wa Umma ambao wanastahiki kulipwa kiinua mgongo kupitia Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, nimejibu na naendelea kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwamba jumla ya watumishi kwa mujibu wa swali lako (a) jumla ya watumishi 10,760 watakuwa wapo kwenye utumishi wa umma hadi kufikia 2017 na ambao watastahiki kulipwa kiinua mgongo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango hilo ndio swali lako (a) nafikiria (a) limejibika. Mhe. Naibu Spika…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, analotaka kujibiwa Mhe. Mjumbe ni swali lake (b), ambalo ameliulizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika ...

Mhe. Naibu Spika: Samahani Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba nitoe maelezo ya ziada kama ifuatavyo:-

Nadhani sheria ziko wazi, kwa wale wafanyakazi ambao wameajiriwa kuanzia 1998 wakati wa Mfuko wa *ZSSF* unaanzishwa wale wanalipwa mafao yao moja moja na *ZSSF*. Lakini kwa wale walioajiriwa nyuma ya hapo wana-*qualify* kulipwa sehemu *ZSSF* na sehemu wanalipwa ya Hazina Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utaratibu huo uko wazi na ndio unaofuatwa kwa mujibu wa sheria zetu. Nakushukuru.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, ni wafanyakazi wangapi hadi sasa ambao wameshastaafu na hawajalipwa viinua vyao mgongo na lini serikali itawalipa wafanyakazi hao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, swali la Mhe. Yussuf Hassan Iddi *detail* za kutosha kwa maana hesabu. Sasa hapa naofia kusema moja kwa moja ni watumishi wangapi, ambao walioulizia lakini nimwambie kwamba hili nitajibu kwa maandashi na baadaye nitawasilisha Barazani nashukuru sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kulipa nafasi hii, pamoja na majibu tuseme mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kuna wafanyakazi ambao kwamba wanafikia kustaafu wengine wanafika hadi kufariki, kiinua mgongo chao kinachelewa ni sababu ipi inayosababisha hasa kiinua mgongo kwa wafanyakazi wale kuchelewa, mpaka kufika mtu kufariki hajapata kiinua mgongo chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, sio sahihi kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inavichelewesha viinua mgongo vya wafanyakazi wake pale ambao wanapostahiki kustaafu. Lakini Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Mwakilishi aelewe kwamba swali la kiinua mgongo kuna taratibu zake, sio kwamba leo unastaafu uweze kupata siku hiyo hiyo.

Kwa hivyo, upo utaratibu kwamba katika ile wizara au taasisi husika maofisa utumishi pale wanatakikana kumwandika *CAG* kwa maana kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Sasa na yeye hapa atakuwa anafanya uchunguzi wake na sio moja kwa moja kuandikiwa kwamba yeye aidhinishe aseme basi aa yende mbele tu hapana isipokuwa yeye atakagua. Kwa maana hiyo, kama kutakuwa na hitilafu au wasiwasi juu ya kile ambacho alichopelekewa *file* lile atalirejesha kule kule, ili wale maafisa utumishi waweze kurekebisha.

Na iwapo atapelekewa baada ya kufanya ukaguzi, patakuwa hapana wasiwasi wowote, basi yeye Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *file* lile atalipeleka Wizara ya Fedha na Mipango halikadhali atapeleka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, kwa ajili ya muhusika yule kupata kiinua chake mgongo nashukuru.

Nam. 63

Tozo Kubwa ya Leseni ya Biashara ya Halmashauri

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hivi karibuni kuna taarifa kuwa Halmashauri za Wilaya zimepanga kutoza shilingi 25,000/= za leseni kwa ajili ya kufanya biashara katika maeneo ya Halmashauri hizo.

(a) Je, kiwango hicho kimezingatiwaje kwa wafanyabiashara wadogo hasa wajasiriamali kama mama lishe n.k ambao mtaji wao haufiki hata nusu ya tozo hiyo.

(b) Sheria gani zimetumika kupanga tozo hiyo bila kuzingatia hali ya vipato vya wafanyabishara wadogo ambao wengi wao huwa wanahangaika kupata angalau kula yao ya siku.

(c) Serikali haioni si vyema kuweka kiwango hicho kikubwa cha tozo kwa wafanyabiashara ambao wanahangaika kujikwamua na hali ngumu ya maisha na badala yake kikapunguzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Mhe. Mahiri sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vipengele (a), (b) na (c).

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ada ya leseni ni chanzo kikuu cha mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) na inakadiriwa kuwa chanzo hiki kinachangia takriban karibu asilimia 80 ya pato la Halmashauri. Kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7/2014, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa mamlaka ya kuandaa sheria ndogo ndogo *(By Laws)* na ambazo huainisha viwango vya ada mbali mbali zikiwemo ada za leseni, ambazo kabla ya kuanza kutumika zinatakiwa kupitishwa na Baraza la Madiwani na baadaye Mhe. Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Serikali za Mitaa kabla ya kuanza kutumika.

Mhe. Naibu Spika, hatua hizo zinalenga kuhakikisha kuwa viwango vilivyowekwa vinalingana na huduma inayotolewa na aina ya biashara husika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi swali lake Nam. 63 kama ambavyo nimeeleza kifungu (a) (b) na (c).

(a) Mhe. Naibu Spika, kiwango cha shilingi 25,000/- kinachotolewa kwa ajili malipo ya ada ya leseni kimezingatia kiwango cha mtaji wa mfanyabishara husika. Kwa kuwa kabla ya kukatwa kwa leseni hiyo tathmini ya pamoja hufanyika baina ya Halmashauri husika na muombaji wa leseni, ili kujua thamani ya mtaji wa muombaji leseni. Kwa upande wa wafanyabiashara wadogo kama vile mama lishe na kadhalika; wao wanacholipa ni ada ya kuchangia gharama za usafi tu na wala si malipo ya leseni.

(b) Mhe. Naibu Spika, kiwango cha shilingi 25,000/- kinachotozwa kwa baadhi ya wafanyabiashara bado ni kidogo mno hasa ikizingatiwa kuwa leseni hizo zinatumika kwa muda wa mwaka mzima ikiwa ni wastani wa malipo ya shilingi 2,083/- tu kwa mwezi au sawa na malipo ya shilingi 69/- kwa siku. Kulingana na uchambuzi huu kiwango cha malipo ya shilingi 25,000/- ni kidogo mno Mhe. Naibu Spika. Hata hivyo, hata kwa wale wafanyabiashara wenye mitaji midogo.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa mantiki hiyo ya jibu (b) hakuna haja ya kiwango hicho kupunguzwa badala yake kinahitajika kuongezwa, ili kuziongezea Halmashauri uwezo wa kupunguza utegemezi wa fedha wa kutoka Serikali Kuu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya kusikitisha na ya kuvunja moja kwa wafanyabiashara wadogo wadogo naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu viwili.

Mhe. Naibu Spika, serikali hasa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imekuwa ikichukuwa jitihada kubwa sana nipongeze kujiajiri wananchi na ikitoa fedha ili iweze kujiendesha. Lakini Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ leo anawarudisha nyuma wafanyabiashara wadogo wadogo, kwa kusema ndio kwanza anataka kupandisha ada nyengine zaidi kuliko hii, jambo la kusikitisha sana. Mhe. Naibu Waziri, shilingi 25,000/- tu kuangalia afya na risiti zipo ….

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, unatakiwa uulize swali la nyongeza sio majadiliano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kama hujajenga hoja huwezi kupata swali, basi unaanza kunisikiliza Mhe. Naibu Spika, halafu unaweza ku ….

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, yako imekuwa ndefu mno ifupishe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naheshimu kiti chako. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, alisema shilingi 25,000/- unalipa kwa mwaka, ambapo kitu hicho sio kweli wafanyabiashara wangu Bwejuu, Michamvi na Paje wanalipa shilingi 25,000/- kwa mwezi halafu shilingi 25,000/- kuangaliwa afya, sasa mtu anayo biashara yake ndogo tu ya maandazi mtaji wake 25,000/- leo unamlipisha pesa hizi si kumzulumu au kumuonea kitu ambacho hakielekei.

Lakini swali la pili naomba atueleze hiyo ada ya usafi ni shilingi ngapi, na kwa nini wasiondoe ada hizi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, ishafika wakati kuwaonea huruma, tusiwe na huruma kwa mdomo bali na vitendo vinatakiwa vifuatie nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimuombe tu, Mhe. Mwakilishi kwamba majibu ambayo nimeyatoa sio yakusikitisha, na badala yake ni majibu ambayo yametoka kutokana na hali ambazo biashara zetu ambazo zinaendelea katika mitaa yetu au katika Halmashauri zetu. Mhe. Naibu Spika, nimkumbushe tu Mhe. Mwakilishi kwamba serikali haina dhamira mbaya juu ya wananchi wake, na badala yake imekuwa ikitafuta namna ya kuendelea kuwahudumia wananchi popote pale walipo na sio vyenginevyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, swali jengine ni kwamba wananchi wa Jimbo la Paje ambao wanazungumzia kama hivi ambavyo tumetoa katika majibu yetu, kwamba wanatozwa shilingi 25,000/-. Mhe. Naibu Spika, ningeomba tu kwamba taarifa hii bado katika ofisi yetu bado hatujaipata vizuri nadhani Mhe. Mwakilishi atusaidie katika kulithibitisha hilo, ili mwisho wa siku tuone kwamba ni hatua gani ambazo tunaweza tukazichukua katika kuona kwamba jambo hilo haliendani kinyume na

kanuni ambazo tumekuwa nazo. Kwa kweli, tozo mbali mbali ambazo tulikuwa nazo katika halmashauri zetu, zinazingatia sheria hiyo ambayo nimeisema ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 2014.

Kwa hiyo, kuhusu viwango ambavyo vimetozwa Mhe. Naibu Spika, naomba kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba viwango nilivyosema kwamba katika majibu yangu nilipokuwa nikijibu nilisema kwamba, kati ya hizo asilimia ambazo nimezitaja ni kuonesha kwamba wastani wa bei ambazo katika sisi taasisi zetu tunaziangalia kwamba tumesema ni shilingi 2,083/- ambayo hiyo ni wastani tumesema ni kwa mwezi mzima. Vile vile, tukasema kwamba kwa siku ni shilingi 69/-.

Kwa maana hiyo, hii inaonesha kwamba bado kwa kiwango hicho ambacho tumekisema Mhe. Mwakilishi, mwananchi kutoa shilingi mfano biashara wetu mdogo huyu kutoa shilingi 69/- kwa siku moja, bado nadhani hatujaenda kinyume na utaratibu ambao tumeona. Hivyo, jambo hili limefanyika kwa kuzingatia, yaani biashara halisi ya mfanyabiashara wetu. Mhe. Naibu Spika, nashukuru ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweka kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, waliwahi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ukusanyaji wa kodi hiyo, ili kuondosha malalamiko katika ukusanyaji huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nitoe majibu ya swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, suala la elimu kwa halmashauri zetu ni jambo ambalo endelevu na tumekuwa tukifanya kuelimisha kwa njia mbali mbali, ili kuhamasisha wananchi wetu katika kuona kwamba wanazifahamu shughuli ambazo tunazifanya, vile vile wanafahamu ni namna gani tozo mbali mbali zinatakiwa zitozwe kwa kupitia shughuli wanazozifanya.

Hivyo, Mhe. Naibu Spika naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kazi hiyo ni endelevu na mara zote tunakuwa tunafanya kwa kila siku, na hususan pale ambapo tunafika kwa mfanyabiashara yule ambaye anahitaji ile huduma ni kwamba kawaida anapewa taaluma kwanza ndiyo baadaye anapewa huduma ambayo ameyoikusudia.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu wafanyabiashara na matozo hayo, naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa sheria ipi inayotumika pia Halmashauri kwa Masheha wetu wanapotoza vyeti vya kuuzia karafuu kwa bei tofauti wengine wanatoza shilingi 1000/-, wengine wanatoza shilingi 3,000/- wengine ni shilingi 5,000/=. Je, ni kwa sheria ipi inayotumika katika kutumia vyeti vya kuuzia karafuu hasa huko Pemba. Ahsante

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, kama unaweza kulijibu kwa sababu sio swali la msingi. Kwa hivyo, kama utaweza kulijibu utalijibu na kama utaona huwezi kulijibu naomba uliwache. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za (SMZ): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali ambalo kama ulivyosema Mhe. Naibu Spika, ambalo liko nje ya swali la msingi, ambalo limeulizwa kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuelezwe Mhe. Mwakilishi kwamba taarifa ambayo ametupatia kwa sasa hivi kuhusiana na kwamba kuna tozo mbali mbali zinatolewa na masheha ambazo zinakuwa tofauti katika ya sheha mmoja pengine na shekha mwengine hususan katika Kisiwa cha Pemba. Taarifa hii niseme kwamba Waheshimiwa Masheha wanaongozwa na sheria na kama kuna kitu ambacho kimefanywa tofauti siwezi kuzungumzia kama hiyo itakuwa ni sheria.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Mwakilishi baada ya kutoka anisaidie maelezo kidogo, ili kuona ni wapi tunaweza tukaanzia kukabiliana na hali hiyo, ili tuweze tukatoa jibu ambalo ni sahihi ili liweze kuleta faida kwa waheshimiwa wote, ili tuweze kuona kila eneo tunakwenda kwa mujibu wa sheria za nchi yetu zinaruhusu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 120

Bajeti za Mashirika Yanayojitegemea

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayo Mashirika na Mamlaka nyingi ambazo zinajitegemea na baadhi yake zina uwezo mkubwa wa kifedha, hivyo kuwa tegemeo katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

(a) Ni lini serikali itafikiria utaratibu mpya wa bajeti ya Mapato na Matumizi ya Mashirika hayo kuletwa Barazani, ili Wajumbe wa Baraza kwa niaba ya wananchi wapate fursa ya kujadili bajeti hizo.

(b) Hivi serikali inazikagua vipi bajeti za mashirika yake na kupata kujua undani wa bajeti hizo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali Nam. 120 la Mhe. Machano Othman Said lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Mashirika ya Umma yanasimamiwa chini ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya mwaka 2002 na kuendeshwa pamoja na sheria zinazoanzisha mashirika au mamlaka hizo. Kimsingi, mengi ya mashirika hayapati fedha za uendeshaji kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na pia yanaendeshwa kwa utaratibu tofauti na ule wa wizara na idara za serikali.
Kwa mujibu wa sheria, wakati mashirika hayo yakimilikiwa na serikali, dhamana ya usimamizi wake upo kwa Bodi husika za Wakurugenzi. Miongoni mwa dhamana hizo ni kuidhinisha mipango ya shirika, bajeti na usimamizi wa uongozi.

Mhe. Naibu Spika, hivyo bajeti za mashirika hazijadiliwi na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, serikali inatambua jukumu lake la kisheria la kuwasilisha mbele ya Baraza Taarifa ya Mkakati wa Shirika, Taarifa ya Mwaka pamoja na Hesabu zilizokaguliwa za mwaka uliotangulia na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya mahesabu ya shirika.

Serikali, itafuatilia kuhakikisha kuwa kuanzia mwaka ujao wa fedha, mawaziri wote ambao wizara zao zina mashirika wanawasilisha mbele ya Baraza taarifa hizo kama inavyotakiwa na katika kifungu cha 27 cha Sheria ya Mitaji ya Umma.

(b) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza, serikali inasimamia bajeti za mashirika kupitia Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika hayo na hatimaye

mawaziri husika na shirika kuidhinisha bajeti hizo. Hata hivyo, Sheria ya Mitaji ya Umma inataka kuwa kila shirika liwasilishe kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha, Waziri mwenye dhamana ya Shirika husika na Kamishna wa Mitaji ya Umma, Rasimu ya Taarifa ya Mkakati wa Shirika, Mpango wa Uwekezaji wa Shirika hilo na kuwasilisha taarifa nyengine zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Utaratibu huu, unakusudia kutoa fursa kwa bajeti hizo pamoja na mipango mengine kujulikana na serikali kabla ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi kwa utekelezaji. Serikali itaongeza nguvu za kuusimamia utaratibu huo wa kisheria.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante kwa kunipa nafasi hii, pia nimshukuru na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu yake mazuri ya ufasaha lakini pamoja na kuahidi kwamba Mawaziri wataleta majibu ya Mashirika yao Barazani. Je, wale mawaziri watakaoshindwa kuleta majibu Barazani serikali itawachukulia hatua gani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninavyoamini hakuna Mhe. Waziri atakayeshindwa kuwasilisha taarifa hizo. Suala hili tayari tumeshalizungumza ndani ya serikali, lakini Wizara ya Fedha na Mipango tayari imeshatoa muongozo kwa Mawizara kuanza kuwasilisha taarifa zao katika mwaka wa fedha ujao. Kwa hivyo, naamini kabisa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Mawaziri makini watatekeleza wajibu wao kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Katiba ya Zanzibar kifungu Nam. 112 kinatambua kwamba uwepo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye atakayeteuliwa na Mhe. Rais.

Lakini pia katika kifungu cha 112(4) natambua kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kila mtumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukumbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyenginezo zinazohusika na hesabu.

Swali langu Mhe. Naibu Spika lipo hapa, kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amekuwa akitumia kampuni za nje katika kukagua mashirika na taasisi nyingi za serikali, ambapo inapelekea gharama kubwa sana. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kufahamu ni juhudi gani, ambazo serikali iliahidi mwaka jana hadi kuelekea mwaka huu wa fedha na mwaka huu ya kazi. Vijana wangapi sasa kutoka Zanzibar wameweza kufanyiwa *training* ipasavyo, ili waweze kufanya hizi kazi za udhibiti na kukagua mahesabu, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaongeza ajira kwa Wazanzibari ndugu zetu kwa pamoja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza Mdhitibi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anafanya shughuli zake na anatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Sheria inamuelekeza ama kufanya kazi hiyo ya ukaguzi yeye mwenyewe au kuchagua mkaguzi mwengine ambaye atamuona anafaa kufanya kazi hiyo kwa niaba yake.

Mhe. Naibu Spika, anapozungumzia suala la gharama, ni suala la ulinganifu tunalinganisha na gharama ipi. Nadhani Mhe. Mjumbe inawezekana gharama anayoiona ni kubwa, lakini kwa shughuli za ukaguzi zinazofanya katika nchi nyengine ikawa hiyo ni gharama ndogo sana. Kwa hiyo, kwanza inategemea anahusisha gharama hizo na kitu gani.

Lakini swali lake la kwamba je, watendani wangapi wamepata mafunzo, ni swali ambalo nitahitaji kulijibu kwa maandishi, kwa sasa hivi sina takwimu hizo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kwa mujibu wa Ripoti ya *PAC* kuna baadhi ya mashirika hayajafuatiliwa na *PAC*.

a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuwa mashirika hayo hayajakaguliwa.

b) Ni lini serikali itafanya ukaguzi katika mashirika hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ningeomba alirudie tena, kwa sababu sikumpata hasa anakusudia kitu gani.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, naomba urudie swali lako.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwa mujibu wa Ripoti ya *PAC* iliyotolewa katika Baraza hili mwezi Februari mwaka huu, kuna baadhi ya mashirika hayakufanyiwa ukaguzi na *PAC* likiwemo Shirika la Bandari.

a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea mashirika hayo kutokukabuliwa.
b) Ni lini serikali itafanya ukaguzi wa mashirika hayo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria, mashirika yote yanapaswa kukaguliwa hesabu zao na Mdhitibi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Sasa kama limetokea tatizo katika shirika au baadhi ya mashirika, basi ni suala ambalo tutahakikisha tunalisimamia, ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweze kuyakagua mashirika hayo kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria uliopo.

b) Hivi sasa sina majibu ya kumueleza kwa nini, ilitokea nini kwamba mashirika hayo hayajakaguliwa, lakini kwa vile ameeleza yapo mashirika ambayo hayajakaguliwa, basi sisi tutalifuatilia suala hilo na kuona kwamba mashirika hayo nayo yanakaguliwa kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria uliopo. *(Makofi)*

Nam. 135

Umiliki na Usimamizi wa Jengo la *ZSTC* (Forodhani)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Shirika la *ZSTC* limejenga jengo zuri la kisasa hapo Miti Ulaya kwa ajili ya ofisi zake na kuzipangisha. Lakini jengo la zamani ambalo ofisi hiyo ilipokuwepo hadi sasa halina watu na liko katika hali mbaya ambayo haipendezi kwani majengo yote yaliyolizunguka yameshakarabatiwa na yanafanya shughuli tofauti za kibiashara.

(a) Jengo hilo baada ya *ZSTC* kuhama liko chini ya wamiliki gani.

(b) Je, hatuoni jengo likiwa katika hali ile katikati ya majengo mazuri yaliyokarabatiwa, hatuoni kwamba tunaiharibu mandhari ya eneo la ufukwe wa Forodhani.

(c) Kama serikali hailihitaji jengo hilo, kwa nini hapewi muwekezaji akalikarabati na kuweza kuunganisha ukanda ule uliojaa mahoteli makubwa na yenye hadhi na kuufanya ufukwe kukamilika na kuvutia ukipita kwa chombo cha usafi wa baharini.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali lake Nam. 135 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, jengo la zamani ambalo *ZSTC* lilikuwa linatumia (Forodha Mchanga) kabla ya kuhamia katika ofisi yake ya sasa ilipewa na serikali, jengo hili linamilikiwa na Shirika la Bandari.

Mhe. Naibu Spika, tumeona mpaka sasa uongozi wa Shirika la Bandari utakuwa na maelezo zaidi juu ya mipango ya ukarabati wa jengo hilo hapo baadaye.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub unasemaje kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nasimamia Kanuni ya 37 Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa hakufanyiwa haki ya swali alilouliza. Kimsingi kwa mujibu wa Kanuni zetu kauliza serikali na serikali mawaziri wanaweza kufanya kazi kwa pamoja. Hakuna jawabu la kwenda kumwambia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, mawaziri wanafanya kazi kwa pamoja, hakufanya haki kwa mujibu wa Kanuni zetu na Katiba ya Zanzibar.

Kwa hiyo, swali lake halikujibiwa, mawaziri wanafanya kazi kwa pamoja, kama Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, yupo atujibu swali lake na kama yeye hayupo kaimu wake yupo, atujibu swali.

Mhe. Naibu Spika: Nimesikia Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Suleiman swali la nyongeza.

Mhe. Waziri wa Uchukuzi unaweza kujibu swali ukiwepo hapo hapo sijui ulikuwa una nia ya kujibu swali.

Sawa tunaendelea, Katibu tunaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali langu nilitaka nitoe maelezo kidogo. Hili swali nilivyolipeleka lilikuwa lime *target* moja kwa moja Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndiyo wenye *responsibility* ya kujibu swali hili. Nimesema hayo nachelea kuja kupata majibu kama aliyopata mwenzangu.

Hivyo, kwa ruhusa yako naomba swali langu Nam. 1 lipatiwe majibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Abdalla Maulid Diwani subiri baada ya kujibiwa ndiyo utaweza kuiuliza wizara inayohusika.

Nam. 1

Posho la Walimu Waliofundisha Halaiki Katika Sherehe za Uhuru wa Tanganyika (2016)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza:

Kumekuwa na jitihada kubwa za Serikali ya Muungano katika kuimarisha mahusiano yetu katika sherehe za kitaifa, ambazo katika sherehe za Uhuru wa tarehe 9 Disemba mwaka 2016, Zanzibar ilitoa walimu wa kufundisha halaiki na kwa bahati mbaya walimu wale hawakupewa posho la kujikimu.

(a) Je, wizara yake inalitambua hilo.
(b) Lini wizara yake italishughulikia suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake Nam. 1 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba wakufunzi 4 na walimu 5 na daktari 1 kutoka Zanzibar walishiriki katika shughuli za halaiki Tanzania Bara zilizolenga katika maadhimisho ya sherehe za kitaifa za Siku ya Uhuru wa Tanganyika

zilizopangwa kufanyika tarehe 9/12/2016 katika uwanja wa taifa. Sherehe hizi zilifutwa kwa mwaka huo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutolewa agizo la kuwarejesha nyumbani washiriki wote wakiwemo wanafunzi zaidi ya mia mbili kutoka Zanzibar.

Wakufunzi hawa, ni kweli walirejea nyumbani wakati taratibu za malipo yao ya makaazi na posho la kujikimu hayajalipwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo ndio dhamana ya shughuli hiyo. Kilicholipwa kwa wakati huo ilikuwa ni nauli tu ya kwenda na kurudi kwa washiriki wote kutoka Zanzibar.

(b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunaimani jitihada zinazoendelea katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mashirikiano na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ambayo ndio inayoratibu jambo hili la kitaifa. Jambo hili litapata ufumbuzi na hatimaye wakufunzi na walimu wote wataweza kupatiwa stahiki zao katika utaratibu ambao Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya kwa kila mwaka. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyojitahidi kujibu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kuweka sawa, haikuwa mwaka 2016 ni mwaka 2015 mara tu baada ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuingia madarakani alizisimamisha sheria zile, nalirekebisho hilo.

Je, nataka kujua bila ya majibu ya kisiasa ni lini walimu wale watapatiwa yale malipo yao stahiki, bila ya majibu ya kisiasa, tunajipanga, tunaangali, au namna gani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama ifuatavyo.

Katika maelezo ya awali nilieleza kwamba suala hili linafahamika na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ambayo ndiyo inaratibu shughuli hizi inafuatilia, hatuwezi kusema lini lakini wakati wowote utaratibu utakapokamilika walimu hawa watalipwa stahiki zao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Zanzibar ina upungufu mkubwa sana wa wataalamu wa halaiki, ambao wametajwa au walimu wa kufunzwa halaiki baada ya kufariki kwa Mwalimu Mkuu wa halaiki Mwalimu Faki Mwenyezi Mungu amrahamu, nafikiri kuna walimu wawili wenye utaalamu huu.

a) Je, wizara inalifahamu tatizo hili.

b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na wizara inayohusika na michezo ina mpango gani ya kuwasomesha vijana wetu wa Zanzibar juu ya fani hii muhimu, ili inapotokezea ushiriki katika mambo ya muungano na sisi tunawakilisha. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inalifahamu suala hili na kwa kushirikiana na wizara nyengine inayohusiana na masuala ya utamaduni ingawa Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia ina sehemu Idara Maalum ya Utamaduni suala hili tutaweza kulifanyia kazi na nadhani si muda mrefu upungufu wa wataalamu katika masuala ya halaiki utaondoka. Lakini nieleza kwanza bado tunao wataalamu na bado mafunzo ya halaiki yanatolewa pale inapohitajika. Ahsante sana.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amekiri kumetokea ucheleweshaji huo wa maposho kwa wakufunzi wetu hawa wa halaiki. Je, serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba ucheleweshaji huo hautokezei tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi swali lake na nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba utaratibu wa utoaji maposho kwa shughuli mbali mbali za serikali unafahamika, na suala hili la maposho katika muhtadha huu wa shughuli za halaiki ulicheleweshwa kwa sababu maalum. Sasa pale ambapo sababu kama hizi

zitakuwa hazipo, hakuna sababu ya mtu kucheleweshe pesa zake, lakini niseme tu kwamba kulikuwa na mazingira maalum ndio yaliosababisha hivyo, katika mazingira ya kawaida hakuna ucheleweshaji wa posho. Ahsante sana.

Nam. 23

Uelewa wa Matumizi ya Ardhi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha sekta ya ardhi, bado sekta hiyo imekuwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uelewa mdogo wa wananchi juu ya matumizi mazuri ya ardhi na kutotumika ipasavyo kwa sheria za ardhi.

(a) Je, serikali inafahamu kwamba wananchi wengi hawana elimu ya matumizi mazuri ya ardhi.

(b) Je, serikali imeshawahi kutoa elimu ya umiliki wa ardhi na matumizi yake.

(c) Je, ni utaratibu gani unaotumika kwa mwananchi wa Zanzibar na mgeni kupata ardhi kwa ajili ya matumizi mbali mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarhan Saidi swali lake Nam. 23 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mhe. Naibu Spika, ni wajibu wa kila mwananchi wa Zanzibar kuzielewa, kuzifuata na kuzitii Sheria za Zanzibar zikiwemo za Ardhi. Kutokana na taaluma inayoendelea kutolewa na serikali, wananchi wamepata uelewa mzuri wa matumizi ya ardhi kuhusiana na masuala ya utambuzi, usajili na uhaulishaji wa ardhi.

Halikadhalika, wananchi wanayo elimu ya kutosha juu ya mpango bora ya matumizi ya ardhi kama vile Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi, yaani *(Master Plan)*, Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ardhi ya *(National Spatial Development Strategy)*.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kupitia Kamisheni ya Ardhi imeandaa utaratibu endelevu wa kuwahamasisha wananchi katika matumizi bora ya ardhi, njia zinazotumika katika kuwaelimisha wananchi pamoja na televisheni, redio, majarida, kalenda na semina.

Kwa mwaka huu, imeandaa vipindi mubashara *ZBC* na Semina za Masheha, Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Pia katika kuandaa mpango bora wa matumizi ya ardhi, utambuzi wa ardhi, uhaulishaji wa ardhi na usajili wa ardhi, wizara yangu kwa kupitia Kamisheni ya Ardhi inakuwa na utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi wa kawaida, Masheha, Wakuu wa Wilaya na Mikoa.

(c) Mhe. Naibu Spika, unaratibu unaotumika kwa wananchi wa Zanzibar na wale wageni kupata ardhi kwa ajili ya matumizi mbali mbali ni pamoja na kuomba ardhi hiyo serikalini kupitia aidha Kaminisheni ya Ardhi, lakini pia kuna kuomba kwa kuwasilisha miradi ya uwekezaji kupitia *ZIPA*. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa wanavyojitahidi katika kuwafahamisha wananchi juu ya matumizi bora ya ardhi.

Lakini, kwa kuwa sasa hivi ardhi Zanzibar ni mali na inaonekana baadhi ya watendaji wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wanasabisha baadhi ya migogoro ya ardhi na wasiokuwa watendaji wanatumia baadhi ya nyaraka *fake* katika kusababisha serikali kuiingiza katika migogoro ya ardhi.

a) Je, ni hatua gani za kisheria ambazo anachukuliwa mtu au mtendaji anayehusika na mgogoro wa ardhi na yule mtu ambaye sio mtendaji lakini ni raia anajihusisha katika mgogoro huo na wizara inachukua sheria gani katika kukomesha jambo hili.

b) Je, ni watendaji wangapi waliobainika kujiihusisha na migogoro hiyo na kuchukuliwa hatua za kinidhamu, pia na ni watu wangapi ambao sio watendaji wakajihusisha na migogoro hiyo na kuchukuliwa nidhamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarhan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba migogoro ipo ambayo inasababishwa na sababu mbali mbali. Lakini bado hatujabaini kwamba muhusika mingoni mwa wafanyakazi wetu wanasababisha hilo. Suala la kuwepo kwa nyaraka mbili inatokezea inawezekana wengine wakawa nayo ile kabla ya mapinduzi na nyengine wakawa nazo baada ya mapinduzi inategemea nyaraka yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, sasa watakapokuta labda mfanyakazi kamueleza baada labla ya kwanza kaiona hii ya kwanza ya pili ikatokezea ile nyengine, maana yake tutakuwa tunazilinganisha zile nyaraka. Kwa kweli, hatujapata kusema huyu ndiye mfanyakazi ambaye anayesababisha.

Mhe. Naibu Spika, lakini namna ya kutatua ndiyo maana tukawa na Mahakama ya Ardhi kusudi migogoro ya ardhi inapojitokeza, halafu wakavutana watu zaidi ya mmoja basi zitapelekwa pale kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa kisheria, kwa sababu kuna sheria nyingi zinazihusiana na ardhi ndizo ambazo zinatuongoza, na pindipo akipatikana pia muhusika ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria hizi tulizonazo zinazohusiana na ardhi. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatia kwa kusema kwamba wizara yake imetowa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya matatizo au kadhia ya migogoro hii ya ardhi. Lakini niulize swali moja la nyongeza dogo kama ifuatavyo.

Je, ni migogoro mingapi ya kwa sasa hivi ambayo wameitatua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa hapa sina takwimu sahihi, hivyo naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali hilo kwa maandishi *ishaallah*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kukiri migogoro ipo na kajibu kuwa ni wajibu kwa kila mwananchi wa Zanzibar kuzieleza, kuzifuata na kutii sheria zilizomo za ardhi. Lakini Mhe. Naibu Spika, chanzo kikubwa ni wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi hasa ikiwemo Kamisheni ya Ardhi.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi Maji, Nishati na Mazingira kwa umakili wake nimpongeze kwa dhati kabisa. Lakini Kamisheni ya Ardhi katibu wake bado ni kitendawili kikubwa, kuna miradi ya wawekezaji imekwama sasa hivi karibu mitano baada ya kuondoshwa *ZIPA* na wengine wana hati zao miliki mpaka leo mnachukua hatua gani na nyinyi nyote shahidi.

Kwa kweli, Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira anastahiki pongezi kwa dhati kabisa jitihada zake, lakini Kamisheni ya Ardhi sijui kuna *commission* gani wanayoitaka, kuna miradi ya wawekezaji muhimu watano na mradi huu ulipokuwepo *ZIPA* kulikuwa hakuna usumbufu wa aina yoyote, ni sababu gani zilizosababisha hivyo.

Mhe. Naibu Spika, pili kuna watu washamiliki ardhi zao zimepimwa kisheria hati pamoja na kibali wamepewa na washalipa pesa chungu nzima na miradi imekwama, na wanalipa riba chungu nzima mabenki nani mkosa, kosa la ng'ombe wa mbele unampiga wa nyuma.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyokuwa nimesema ardhi kuna sheria nyingi la suala la msingi ni kufuata sheria. Waziri wa Ardhi Maji, Nishati na Mazingira Mhe. Salama Aboud Talib ndiye kiongozi wa wizara kwa hiyo kama kiongozi yuko sawa sitegemei kuona kwamba kuna taasisi ambayo itakuwa inapinda pinda na inawezekana sana tatizo likawa ni sheria ufuataji wa sheria kwa hao wananchi.

Lakini nikuombe sana kwa vile una imani sana na uongozi wa wizara njoo utuone nini kikwazo, kama ni sheria basi tufate sheria na kama kuna tatizo la urasimu basi tutaweka sawa kwa sababu kichwa kizuri.

Mhe. Naibu Spika, chengine hali kadhalika kwa hao aliosema wamepimiwa pia tuone aje nao na hizo hati ambazo wanazo tuone tatizo ni nini kwa pamoja tunaweza tukatatua migogoro yetu. Ahsante sana.

Nam. 41

Kukosekana kwa Vipimo vya Uchunguzi Katika Hospitali ya Mnazimmoja

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa nia njema kabisa, amehakikisha Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja Wodi ya Mama na Mtoto, zinaimarika kwa kuweka vifaa vya huduma ya mtoto, kama alivyofanya Hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani Pemba, kuwa na vifaa vya kisasa.

Je, pamoja na uzuri huo, ni tatizo gani, linalopelekea kukosekana kwa vipimo vya uchunguzi kama *X-Ray, Utrasound,* na *CT-Scan*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza napenda nichukuwe nafasi fupi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia kukutana tena katika Baraza hili tukufu tukiwa na afya njema, na pia nchi yetu ikiendelea kuwa na amani na utulivu wa kutosha chini ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kudumisha neema hii, pia ampe Mhe. Rais wetu wa Zanzibar pamoja nasi wepesi kuweza kutekeleza majikumu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake Nam. 41 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba kukosekana kwa huduma za uchunguzi kama *vile X-Ray, CT Scan,* na *Ultrasound,* kwa baadhi ya wakati katika Hospitali yetu ya Mnazimmoja pia inachangia na kuzidiwa kwa huduma hizo kutokana na wagonjwa wengi, wakiwemo wagonjwa wanaopata matibabu katika hospitali za *private* hufuata huduma za vipimo hivi katika Hospitali yao ya Mnazimmoja, ambazo huduma hizo zinatolewa bila ya malipo.

Mhe, Naibu Spika, kutokana na wagonjwa wengi kutumia haki yao ya kupata huduma hizi katika Hospitali ya Mnazimmoja, Uongozi wa Hospitali umeweka mpango maalum kwa kudhibiti matumizi ya mashine hizo, ambazo zinahitaji pia muda wa kupumzika kwa kuweka idadi maalum ya wagonjwa wa kufanyiwa kipimo hicho kwa siku.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa mashine ya *X-Ray* na *Ultrasound* zinafanya kazi na kutoa huduma kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo, isipokuwa mashine ya *CT*

Scan imesita kwa muda kutokana na kuharibika kwa kwa *belt*, ambayo haipatikani hapa nchini na inalazimika kuagizwa kifaa hicho nje ya nchi. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya kupitia hospitali zake ndio tegemeo kubwa la wanyonge wa nchi hii na tunategemea baada ya tangazo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizi Dkt. Ali Mohamed Shein kuwaambia wananchi wote vipimo vyote *CT Scan, Ultrasound* pamoja na *X-Ray* bure, wananchi wito huo wameusikia na wanampongeza kwa dhati kabisa pamoja na mimi. *(Makofi)*

Lakini badala yake Mhe. Naibu Spika matokeo yake yamekuwa sivyo kama alivyo agiza mwenyewe Mhe. Rais. Swali langu liko hapa.

a) Ni kitu gani kinachosababisha vyombo vyetu hivi vikaharibika mara kwa mara.

b) Vifaa hivi tumeambiwa kwamba vinaagiziwa kutoka nchi za mbali kabisa sijui nchi gani. Je, vifaa hivyo vinatoka nchi gani na vinachukua muda gani, ili vipatikane kuwaondolea adha wananchi wetu ambao wanataabika wakienda hospitali matibabu yao hawayapati ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo.

Sababu ambazo zinasababisha kuharibika kwa vifaa hivi nimetaja katika jawabu langu la msingi kwamba linazidiwa, lakini pia ni sababu nyengine ni kwamba wakati mwengine zinachelewa kufanyiwa *service* na zile ni mashine kwa hiyo zinasababisha pia kuleta usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ni nchi gani ambazo tunaagiza vifaa hivyo, vifaa mara nyingi vinaagizwa katika nchi mbalui mbali ikiwemo Israel, ikiwemo Afrika ya Kusini pamoja na nchi nyengine. Kwa hivyo, umbali wa kutoka huko mpaka kufikia ni kwa sababu ya *process* ambazo zinabidi zifuatwe na kifaa tunakiagiza baada ya kuharibikiwa hatuagizi kabla. Kwa hiyo, hili pia linafanya kifaa kile kichelewe, na kinapoingia katika nchi kuna *process* za serikali zitumike mpaka zitufike sisi hakitukifi tu moja kwa moja na tukaanza matengenezo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali la nyongeza dogo tu.

Mhe. Naibu Spika, kama tungetaja vifaa vya hospitali hasa hizo mashine za uchunguzi basi ingechukuwa dakika kumi na tano kuzitaja na wala hazimaliziki, lakini bila ya uchunguzi tukubaliane kabisa kwamba hakuna matibabu. Je, wizara yake ina utaratibu gani au ina wataalamu wangapi mafundi wazalendo wakushughulikia mashine hizi pale zinapoharibika.

Mhe. Naibu Spika, katika jibu mama Mhe. Naibu Waziri wa Afya amesema kwamba hawaagizi kitu mpaka mashine iharibike. Hivi kwa nini tusikae na *spare* ambazo zipo tayari, ili wagonjwa wetu wasipate tabu pale zinapoharibika mgonjwa apate huduma haraka, tukasubiri mpaka ziharibike ndio tuweze kuagiza *spare* hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika Hospitali ya Mnazimmoja peke yake tunao wataalamu mafundi na ni mafundi wa kutengeneza vifaa mbali mbali sio *Ultrasound* na *CT Scan* peke yake wapatao 11.

Lakini kuhusu swali lake la pili kwamba kwa nini hatuagizi vifaa hivi kabla. Mhe. Naibu Spika, si rahisi hata kidogo kujua kwamba mashine yangu itaharibika kitu gani, na kwa wakati huu mashine pamoja na teknolojia vinabadilika kila wakati tunaokwenda.

Kwa hiyo, unaweza ukakichukua kifaa ukakiweka kama ni akiba, mashine ikashindwa kuharibika kwa mara ile ikaharibika kifaa chengine na kusababisha kifaa kile kuharibika na kupoteza pesa za serikali. Kwa maana hiyo, utaratibu wetu kifaa kinapoharibika au tunapokiona kwamba kimeshaanza kuwa *weak* tunafanya utaratibu wa kuagiza kifaa kile kwa ajili ya matengenezo. Jambo kubwa ambalo linatusumbua sasa hivi ni *process* ya kukitoa kilipo mpaka kutufikia.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa ziara yetu ya kamati tulifika katika Hospitali ya Micheweni na kuvikuta vifaa vya *X-Ray* vinaharibika kwa ukosefu wa kumalizika kwa jengo la kuwekea vifaa hivyo. Je, Mhe. Naibu Spika ni lini jengo hili

litamalizika, ili vifaa vile vilivyo bora vya msaada visiendelee kuharibika. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika Hospitali ya Micheweni huduma ya *X-Ray* na *Ultrasound* zinapatikana kama kawaida na hakuna kifaa ambacho kinaharibika, labda aniainishie ni kifaa gani ambacho amekikuta kinaharibika. Lakini huduma ya *X-Ray* na *Ultrasound* inaendelea bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Shaib Said Ali unayo taarifa ya kifaa gani ambacho kinaharibika.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Naibu Spika, wakati wa ziara yetu ya kamati tulifika Hospitali ya Micheweni tukavikuta vifaa vya *X-Ray* viko chini vinaanza kuharibika, na ushahidi huo tunao Kamati yote ya *PAC* ukiwauliza ushahidi upo na Daktari wa Dhamana wa pale alitwambia kwamba vifaa hivi mpaka leo jengo hili halijamalizika, vifaa sasa hivi viko chini kabisa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ni lini atamaliza jengo lile kuviweka vifaa vile visiharibike. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, bado nina wasi wasi kwamba inawezekana vifaa hivyo ni vya mashine ambazo zilishatumika na hazitumiki tena. Sina taarifa kwamba kuna mashine ambayo haijafungwa imekaa kwa kukosa kuhudumia.

Mhe. Naibu Spika, naomba hili nilichukue nikalifanyie kazi na nitatoa taarifa katika Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii kama ndio *passport*.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Mhe. Mjumbe amesema watalichukua nadhani ndio jibu zuri zaidi hilo kulichukua na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Nam. 42

Utaratibu wa Upakuaji Mawe katika Gari za Mizigo

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa usafirishaji wa mchanga kwenye magari makubwa uliekewa utaratibu wa kufunikwa turubali, ili kuondoa madhara yatayopatikana kwa waliomo barabarani.

(a) Je, serikali imeweka utaratibu wa usalama kwa wasafirishaji wa mawe kwa kuondoa mawe yanayowekwa mpaka kupitiliza bodi ya gari, (kuweka mnara) kwa barabara za hapa Unguja na Pemba.

(b) Je, kama haijaweka ni lini itaweka utaratibu mzuri ambao utakuwa salama kwa walio barabarani dhidi ya mawe yanayodondoka kutoka kwenye gari.

(c) Je, serikali inajua kama upakiaji huo mbaya wa mawe umeshawahi kuleta madhara barabarani kwa mwananchi kuangukiwa na mawe na kumuathiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali imeweka utaratibu wa usalama kwa upakiaji wa mizigo yote na utaratibu huo unaelezewa katika kifungu cha 121 cha Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 (*Road Transport Act*).

(b) Utaratibu tumeuweka tayari na uko salama kabisa kwa watumiaji wote wa barabara.

(c) Serikali inalijua hilo na wote wanaosababisha madhara kwa watumiaji wengine wa barabara wanapelekwa mahakamani, ili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa majibu yake mazuri aliyotoa, naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba na kwa kuwa sheria amesema kwamba imewekwa ya Nam. 21 ya 2003 inayoelezea usafiri barabarani. Lakini kwa kuwa sheria hizo na utaratibu huo wote unavunjwa hivi sasa, hata ukienda pale Mwanakwerekwe utakuta bado lile suala ambalo kuwa ninalalamikia linaendelea.

Je, sheria hii serikali itachukua hatua gani kuona kwamba sheria na utaratibu huo unaendelea kufuatwa, ili kuepusha madhara ambayo watayapata wananchi wetu wakiwa barabarani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyosema hii sheria imeweka bayana kila kitu, yaani imeweka kwamba mtu anapopatikana na kosa apelekwe mahakamani na watu wanaofanya hivyo ni polisi na vile vile kuna adhabu zake zimewekwa. Kwa mfano, kosa kama hilo unapewa adhabu isiyopungua dola 20, ukifanya mara ya pili kuna adhabu nyengine na pia kuna na kifungo kwa mara ya pili au vyote kwa pamoja.

Kwa hivyo, muhimu ni kwa Jeshi la Polisi na sisi tutaendelea kulihimiza na linafanya kazi nzuri kusema la kweli. Mhe. Naibu Spika, kuendelea kuzifuatilia sheria hizi na wao kiutaratibu chombo kinapoingia barabarani wanapokiona kwa mujibu wa kifungu Nam.168 cha Sheria hii Nam. 7 ya 2003, basi wanao uwezo wa kumsimamisha yule mwenye gari na kuifanyia uchunguzi na kama mzigo umezidi wakautoa au wakaupeleka kwenda kupimwa zaidi na baadaye kumpeleka mahakamani, kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria. Ahasante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona lakini niseme tu kwamba wakati Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anajibu swali hili amekuwa anazungumza zaidi kwa sheria wakati nilipouliza swali hili. Lakini niseme tu kwamba kweli sheria Nam.7 ya *Road Transport Act* inatakiwa isimamiwe. Lakini naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri wizara hii ndio inayosimamia mambo yote juu ya bandari yetu ya Zanzibar. Kwa kweli, tunaona pale magari mengi ambayo yanapakia mizigo haya maarufu yanaitwa ‘mafuso’ yanapatikia mafriji, madebe ya mafuta ya kupikia lakini pia na maboriti ambayo hupita nje ya Kituo cha Polisi cha Malindi, na unaona kabisa wakati yanatoka bandarini yanapakia mizigo ambayo yamejazwa kupitwa kiasi.

Magari haya yanapopita barabarani yanaondoa usalama wa wananchi wanaotumia vyombo vya magari pamoja na wale wanaotembea njiani.

a) Je, wizara yake wakati mizigo inapotoka bandarini, inatumia utaratibu gani kuhakikisha kwamba pale yanapotoka nje ya bandari magari haya hayapakii mizigo kupita kiasi.

b) Katika Jimbo langu la Tunguu eneo la Dunga Mitini pamekuwa pana umaarufu sana wa magari ambayo yanatokea Dunga Kinyongo au Mgenihaji kuelekea Dunga Mitini au yale ambayo yanatoka Dunga Kiembeni kuja pale Dunga Mitini yanapita kwa kasi kubwa, yanapakia mawe, michanga na mambo mengine yenye uzito tofauti au mizigo.

   Je, wizara yake inahitaji vifo au ajali ngapi, ili ianze mchakato wa kujenga matuta ambayo yatasababisha kupunguza kasi ya vyombo hizi vya magari, ili kulinda usalama wa wananchi wetu hasa wa eneo la Dunga Mitini. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kazi za usimamizi wa sheria kwa mujibu wa sheria yetu ni kazi ya Jeshi la Polisi. Kwa maana hiyo, naendelea kutoa wito kwa Jeshi la Polisi kama nilivyosema hata bandarini kuna watu wa polisi ambao wanashughulika na mambo yote ya usalama barabarani pamoja na mizigo hiyo.

   Kwa hiyo, pale ambapo wanaona hii sheria Nam. 7 ya 2003 inakiukwa basi wachukue hatua stahiki na wala wasimuonee mtu yeyote haya katika kutekeleza sheria, kwa sababu sheria ni sheria.

b) Vile vile, kama nilivyosema kwamba hii sheria kuna vifungu ambavyo pia Mhe. Waziri vinamruhusu baadhi ya wakati kutunga kanuni. Lakini sisi tunasema kwamba gari zozote zinazoenda mbio ni kosa kwa mujibu wa sheria hii iliyowekwa na gari ya aina yoyote.

   Kwa hiyo, pale inapotokea tatizo tuna Jeshi la Polisi au kama hamna Jeshi la Polisi nawaomba sana wananchi watoe taarifa kwa sababu sasa hivi kuna mpaka Ubalozi wa Usalama Barabarani.

Pia, Jeshi la Polisi kupitia Kamanda Mkadam wametoa elimu kubwa sana kwa wanafunzi na watu namna gani ya kuzitumia namba zao za simu, kwa hiyo zile namba walizozitoa kupitia vipindi vyetu na kupitia semina zetu wananchi waendelee kuzichukukua na pia watupe taarifa. Hii ni kazi yetu sote si kazi ya Jeshi la Polisi, bali pia na wananchi na hasa sisi ambao tunatunga hizi sheria. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 37(1) ambayo inamtaka waziri au mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na ufupi.

Mhe. Naibu Spika, katika swali langu nililouliza la nyongeza kwenye swali la kifungu (a) nimeuliza juu ya magari haya yanayopakia mizigo ambapo mizigo haya yanapakiwa ndani ya bandari kabla hayajatoka kuingia barabarani. Polisi wanaosimamia mizigo au vyombo vya ulinzi vinavyosimamia mizigo ndani ya bandari hawatambuliwi ndani ya *Road Traffic Act* au sheria Nam.7 ya *Road Traffic Act*.

Kwa hivyo, ni kwamba usimamizi wa yale magari ya mizigo inayopakiwa bado ipo chini ya bandari ambayo wizara husika na Mhe. Naibu Waziri ambaye ndiye huyu anajibu maswali. Kwa hiyo, nataka nifamu ni utaratibu upi wizara inasimamia mizigo wakati inapakiwa ndani ya bandari kabla hayajatoka bandarini kuingia barabarani, ili kulinda usalama wa wananchi pamoja na vyombo vya ulinzi ambavyo viko barabarani. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri naomba umjibu sahihi Mhe. Mjumbe swali lake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa sheria yetu aisome vizuri sheria ina vifungu vingi, askari polisi wote wanaovaa sare tayari ni polisi ambaye anaweza kufanya kazi zote za usalama barabarani kwa mujibu wa sheria hii.

Kwa hiyo, yule madamu amevaa sare ni askari ambaye anatakiwa asimamie usalama wa mali na barabara na kila kitu na mtu mwenyewe. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, swali la msingi limehusu kwa usafirishaji wa mchanga, naomba kuiuliza serikali swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kuna magari yapo Maruhubi yana mchanga yanatakiwa yalipe mengine shilingi 5,000,000/- na mengine 10,000,000/-. Lakini wananchi wale wenye magari yale wamekuwa na kilio kikubwa angalau ule mchanga tu ushushwe kwenye magari yale, ili magari yao yasije yakaharibika.

Je, kuna sheria gani iliyopitishwa katika Baraza hili, ili wananchi wapate kujua wamekuwa na kilio cha muda mrefu baada kushindwa kupata shilingi 10,000,000/- za kulipia, ili watapopata hizo pesa waje walipe yale magari yanazidi kuumia. Kuna sheria tumeipitisha humu kwenye Baraza au kuna kauli gani kuhusu wito huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Samahani Mhe. Naibu Spika, naomba alirejee tena swali lake Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub lirejee swali lako halafu taratibu, ili Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji akusikie vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ushauri wako.

Swali la msingi limehusu usafirishaji wa mchanga. Kuna magari yako Maruhubi yamekamatwa na mchanga karibu miezi miwili au mitatu, wenye magari yale wameiomba wizara ile angalau ushushwe ule mchanga yale magari yabaki pale pale, ili yasiumie na ukiuwacha mzigo ule kwenye magari kama miezi miwili au mitatu yanaumia na kipigo walichopigwa ni kikubwa cha shilingi milioni 10,000,000/- au 15,000,000/- kulipa kwa gari moja.

Je, kuna sheria yoyote iliyopitishwa katika Baraza hili, ili mchanga ule usishushwe ni amri au kuna sheria ule mchanga kubaki kwenye gari, kuna sheria tuliyoipitisha au atatoa wito gani kwa wananchi ambao wanategemea chombo hiki kuwakilisha wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa mujibu wa Sheria yetu ya Usalama Barabarani Nam.7 ya 2003 kifungu cha 168 inaelezea iwapo gari itazidisha mfano mchanga itapozidisha uzito wa aina yoyote, basi ile gari itapelekwa kituo ch polisi baadaye kwa kufanyiwa uchunguzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo inatakiwa zile gari zipelekwe mahakamani, kwa ajili ya kujibu kosa walilolifanya na baada ya hapo ule mchanga ndio unakuwa ushahidi wenyewe, ili baadaye adhabu stahiki iweze kutolewa kwa yule aliyefanya kosa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Kanuni ya 63(37) haina haja ya kuisoma nafikiri. Mhe. Naibu Spika, nimeiuliza serikali kuna sheria iliyopitishwa ndani ya chombo hiki, kuna magari yapo miezi miwili karibu au mitatu yamekamatwa na mchanga wananchi au madereva wale wamekuwa wakilia angalau ule mchanga uteremshwe yale magari yasiumie.

Kwa hivyo, nilichomuuliza Mhe. Naibu Waziri je, kuna sheria tuliyoipitisha ndani ya chombo hiki ule mchanga usishushwe yale magari yanaumia na wananchi ni wanyonge kumlipisha milioni 10,000,000/- sasa hivi ni kumuua mwananchi. Mhe. Naibu Spika, naomba kujua kwamba kuna sheria au atatoa kauli gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (Kny. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza, jambo hili linasimamiwa na sheria Nam. 3 ya 2015 ya maliasili zisizorejesheka, ndani ya sheria hiyo imempa mamlaka Mhe. Waziri kutunga kanuni. Kanuni ndizo zinazoelekeza utaratibu huo ambao Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaulalamikia, kwamba unapomkamata ambaye amehalifu sheria kwa maliasili isiyorejesheka inabidi umkamate na uzuie na hata kile chombo ambacho kimepakia mali ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tungeweza kushusha mchanga serikali maana yake tungepoteza ushajidi wa lile kosa ambalo limetokea. Mhe. Naibu Spika, baada ya kadhia hii kutokea na kwa sababu wananchi waliokuwa raia wema wa nchi hii wanatambua hilo, wapo ambao wamefuata taratibu za sheria na kanuni wamekwenda kulipa faini na kukomboa mali zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimthibitishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba zipo gari chache sana ambazo hizo ndio bado hawajenda kuzikomboa. Kwa hiyo, tunawasubiri waende wakakombowe kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya 2015 na Kanuni zake watakapofanya hivyo tutawakabidhi mali zao, wasipofanya hivyo basi mkono wa sheria utapita katika kuyachukulia hatua. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri na mimi naomba kufuta yale maneno mwanzo niliyoyasema nilipokutaja nafasi yako ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba iingie hivyo kwenye hansard nilikosea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, badala yake iingie Kaimu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 84

Udhibiti wa Mafuriko katika Bwawa la Maji la Mwanakwerekwe na Kibonde Mzungu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Katika Hotuba yake ya Baraza la *Eid-el-Fitri*, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alibainisha hatua kubwa zilizofikiwa katika Mradi wa *ZUSP*, ambao umesaidia kudhibiti mafuriko katika maeneo ya Bintihamrani, Darajabovu, Mnazimmoja na Mpendae. Serikali inastahili pongezi kwa kazi nzuri. Hata hivyo, Bwawa la Mwanakwerekwe na eneo la Kibonde mzungu bado ni changamoto na ni tatizo wakati wa kipindi cha mvua.

Je, serikali ina mpango gani wa kulidhibiti bwawa la Mwanakwerekwe na Kibonde Mzungu, ili yasilete madhara ya mafuriko kila kipindi cha mvua kinapotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika ahsante, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 84 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa eneo la barabara sehemu ya bwawa la Mwanakwerekwe na lile la Kibonde Mzungu bado ni changamoto na tatizo wakati wa kipindi cha mvua. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, wizara tayari imetayarisha fedha kupitia

Mfuko wa Barabara, kwa ajili ya kujenga madaraja na kunyanyua barabara kwenye eneo la bwawa la Mwanakwerekwe, ili sehemu hiyo iweze kutumika wakati wote hata mvua zikinyesha. Kazi hiyo itakamilika kabla ya kuanza kwa msimu wa mvua za masika unaokuja.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu matengenezo sehemu ya Kibonde Mzungu, wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga madaraja pamoja na kunyanyua barabara kwenye eneo hili, ili iweze kupitika kwa muda wote. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri niombe kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

a) Kwa kuwa eneo la Kibonde Mzungu linahitaji ufumbuzi wa haraka, serikali imeweka utaratibu gani wa dharura kuondosha tatizo lile na akichukulia kwamba kila zinapofika mvua huwa eneo lile watu wanafariki. Hatua gani serikali imechukua iliwananchi wanaokaa katika maeneo yale wapate kujua kutoka katika serikali yao.

b) Kiasi gani cha fedha kimetengwa, ili kukamilisha mradi ule ili tupate kujua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema katika jibu mama kwamba pale Kibonde Mzungu tunaendelea kutafuta fedha, kwa sababu pale itahusisha mpaka barabara inayokwenda Tunguu, ambayo tutaitanua kama vile barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni tulipofikia. Kwa hiyo, tuko katika uchambuzi yakinifu na baadaye tutajua gharama ambazo zitatumika pamoja na kujenga yale madaraja na kuinua ile sehemu.

Lakini kwa kuanzia tu, kwa sababu tumeona kwamba katika zile *culvert* lipo pale, lakini limekuwa dogo na vile vile na wala halipitishi maji. Sasa kwa dharura tutaanza kwa kuhakikisha kwamba lile *culvert* kwa kipindi cha mvua za vuli linapitisha maji, na huku tunaendelea na mpango wa utaratibu wa kuhakikisha tunapata fedha za kumaliza lile tatizo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa Maswali na Majibu umemalizika na kwa kutumia Kanuni ya 39(3) niliongeza robo saa kama Kanuni yetu inavyosema ninao uweza wa kuongeza robo saa na hilo tayari nimeshalifanya.

Kwa hiyo, muda huo wa robo saa pia imekwisha bado tumebakiwa na swali moja la Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ambapo sasa kwa utaratibu wetu litakwenda katika *order paper* ya siku nyengine.

Kutokana na hali hiyo, nafikiria Mhe. Omar Seif Abeid swali lako leo halitoweza kujibiwa na litajibiwa siku nyengine. Kwa hiyo, kipindi cha Maswali na Majibu kimemalisa sasa tunaingia katika shughuli nyengine. Ahsanteni. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya 2017

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohammed Said Mohammed nimekuona umesimama.

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 49, naomba kunukuu.

> "Mjumbe anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki na fursa na kinga ya Wajumbe na uwezo wa Baraza anaweza kufanya hivyo wakati unaofaa".

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na jambo nataka kutoa maelezo binafsi kama kifungu cha 27(i).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohammed Said Mohammed nimekuruhusu naomba utumie muda mchache.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, mnamo tarehe 20 mwezi wa Juni niliandika barua kumpelekea Katibu wa Baraza nikiamini na yeye apeleke katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini Katibu wa Baraza alipeleka barua hiyo tarehe 3 mwezi Julai, lakini mpaka hapo taarifa yangu ilikuwa ni kupatiwa taarifa zinazohusu nyumba zilizopatiwa Askari wa Idara Maalum katika nyumba za Michenzani Jumba Nam. 10.

Mhe. Naibu Spika, ni haki ya Mwakilishi ukiangalia kifungu chetu Nam. 9 cha Sheria Nam. 4 ya Kinga na Uwezo, nikiamini taarifa ambazo nimeziomba zinaweza kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kisheria. Lakini hadi hii leo wizara imeshindwa kuniwasilishia majibu ya barua yangu, kama nimepata au nimekosa, na utaratibu huu unaelekea unaanza kutunyima au serikali inaanza kutunyima taarifa zozote ambazo zitatusaidia kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa ninakuomba hili kwa sababu ilibidi nilishitaki mbele ya Baraza letu la Wawakilishi, ambalo ndio lenye nguvu kubwa ya kutunga sheria, nimesema hili nililete mbele yako, ili nipate ufumbuzi au serikali inipe majibu hayo.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniruhusu.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed, nafikiri suala lako umeelekeza kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Waziri naomba utoe maelezo kuhusiana na hoja aliyoitoa Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba niseme yafuatayo: Kwanza cha msingi mwakilishi ni waziri, hiyo barua sina hakika kama imefikia kwa waziri, imekuja kwa Katibu Mkuu, labda ningepata ufafanuzi huo nipate kujua. Lakini nikishapata ufafanuzi huo naweza nikatoa maelezo baada ya kupata majibu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana lakini pia nimshukuru sana Mhe. Waziri na niendelee kumshangaa sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa sababu mtendaji wa wizara ni Katibu Mkuu, yeye pamoja na mamlaka anayopewa ya kutoa labda yeye ndiye mtu wa mwisho, lakini Katibu Mkuu ndiye anayepelekewa barua hizi na hii barua inasemekana imemfika kwa sababu *copy* tunayo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, naomba hiyo *copy* uniwasilishie nimpatie Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, apate uhakika kwamba barua hiyo imekwenda katika wizara yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, barua hii ambayo imeletwa tarehe 3/07/2017 ambayo imeandikwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na imeletwa na Katibu wa Baraza hii barua niliyonayo, naomba sasa nikuletee uione ili uweze kujibu masuala mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ombi langu umelikubali na Mhe. Mjumbe amelitekeleza na ni kweli barua imepelekwa kwa Katibu Mkuu. Hoja yangu ilikuwa barua imekuja kwangu moja kwa moja au ilikuwa kwa Katibu Mkuu, kumbe barua imekwenda kwa Katibu Mkuu. Lakini kwa namna ya muonekano ninavyoiona hii barua nakuomba uniruhusu ninukuu jambo ambalo inalihitaji.

"Nyumba ngapi Askari wa Idara Maalum wamepewa? *Conclusion* ya maelezo ya Mhe. Mwakilishi. Ni nani wanaishi katika nyumba hizi, hivi sasa umiliki wa nyumba hizi uko chini ya nani?"

Mhe. Naibu Spika, kwa uzoefu wangu hata siku nyumba hizi zilipotolewa na aliyekuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa Sherehe za Mapinduzi ya Miaka 50 wakati wa Uzinduzi wa *Block* Nam. 10. Ni kweli kwamba walipewa wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ na kila idara walipewa nyumba tano. Lakini, serikali hawakuwapa Idara Maalum kama taasisi kwa sababu ya kazi ambayo waliifanya katika *block* lile la Nam. 10 isipokuwa walipangishwa wapiganaji wenyewe binafsi sio idara.

Kwa hiyo, Idara ya Nyumba na Majengo ya Serikali kwa wakati ule iliwapangisha wale watu wenyewe mmoja mmoja na wao ni wapangaji halali hivi sasa wa Shirika la Nyumba na wala hizi nyumba sio za Idara Maalum za Serikali. Hiyo ndio taarifa ambayo ninaweza nikaisema, lakini bila shaka kwa sababu hii barua imekwenda kwa Katibu Mkuu bila shaka majibu yataletwa kwa maandishi kwa Katibu wa Baraza. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nianze tu kutanguliza taarifa kwa mujibu ninavyoelewa, kwamba hizi nyumba walipangishwa askari wenyewe moja moja wakati ule na sio za Idara Maalum za SMZ. Ninaposema hivyo inaeleweka, maana kama ingekuwa wamepangishwa idara, basi wangekuwa wanakaa na idara ingekuwa zinalipa kodi halafu zinabakia kuwa ni mali ya zile idara au ni mali ya serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ninakushukuru sana kwa majibu yako. Mhe. Mohammed Said Mohammed kaa kitako hapa utaratibu umeshapita, utaratibu wa Katibu wa Baraza kupeleka barua kwenye wizara kwa ajili ya kupata majibu na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ umejibu vizuri sana, tutatumia utaratibu ule ule kurudisha majibu hapa.

Nafikiri kikubwa ambacho kimefanyika hapa ni kukumbusha lile ambalo lilitakiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed. Naomba sana tujue hivyo kwamba yatakuja majibu kwa Katibu wa Baraza, ili Mhe. Mohammes Said Mohammed apewe majibu kwa maandishi kama alivyotaka mwenyewe. Nashukuru sana, Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuuliza hivyo. *(Makofi)*

Tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa maelezo yanayohusiana na kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Sheria Nam. 3 ya Mwaka 1985 na kutunga Sheria Mpya ya Mahakama ya Kadhi ya Zanzibar ya mwaka 2017.

Mhe. Naibu Spika, taarifa hii nakusudia kuwasilisha mapendekezo ya kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Sheria Nam. 3 ya Mwaka 1985 na kutunga Sheria Mpya ya Mahakama ya Kadhi ya Zanzibar ya mwaka 2017, ili kuondoa kasoro za kisheria kwenye mfumo wa Mahakama hiyo, kuimarisha utendaji kazi wake na pia kuleta ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, historia Mahakama ya Kadhi hapa Zanzibar ilianzishwa na Utawala wa Kisultani mnamo mwaka 1897. Aidha, Waingereza waliitambua Mahakama hiyo na kuiweka kwenye mfumo wa sheria za Zanzibar kupitia *Zanzibar Court Decree* ya mwaka 1908. Tangu wakati huo Mahakama hiyo imetekeleza majukumu yake kwenye mfumo rasmi na ina nafasi kubwa katika sekta za utoaji haki hasa katika masuala ya kifamilia.

Mhe. Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni Mahakama ya Kadhi imekuwa ikilalamikiwa kwa udhaifu katika kutekeleza kazi zake, baadhi ya tafiti za karibuni zimebainisha udhaifu huo kutokana na kasoro mbali mbali ikiwemo kasoro ya kisheria. Miongoni mwa tafiti hizo ni *Perspectives on the Kadhis' Courts in Zanzibar* uliofanywa na *Prof*. Majamba, mwaka 2008. Aidha, utafiti wa *Practice in*

Kadhis' Court with the regard Womens Rights Case Study ya Zanzibar ya mwaka 2010 wa *ZAFELA* na kazi ya ushauri ya kupitia Sheria za Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1987 uliofanyika mwaka 2012 iliyofanywa na Bwana Ali wa Ali Hassan na Mohammed Khamis.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya mapungufu yaliyomo katika sheria ya sasa ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa Sheria Nambari 3 ya mwaka 1985 inayoongoza shughuli za Mahakama ya Kadhi kwa mujibu wa tafiti hizo imeonekana kuwa na udhaifu katika maeneo mbali mbali yakiwemo:

1. Sheria hiyo, imekosa Kanuni za kuendesha Mahakama hiyo na kwa sababu hiyo, Kanuni za Sheria ya Mwenendo za Madai ya Sura ya Nane zinatumika, ingawa si makadhi wengi wanaozielewa vyema kanuni hizo.

2. Sheria hiyo, haielekezi utaratibu wa usuluhishi ambao ungesaidia sana kupunguza idadi ya kesi mahakamani.

3. Sheria hiyo, haiwapi makadhi uwezo wa kuwashughulikia kisheria watu wanaodharau au kuidanganya mahakama hiyo.

4. Sheria hii, haitoi ruhusa ya kutumia mawakili katika kusimamia kesi za Mahakama ya Kadhi wanaoruhusiwa ni mavakili tu, ambao si wengi wenye uwezo wa kutosha katika fani ya sheria na sharia.

5. Sheria, haiweki mipaka ya eneo la kufungua shauri. Kwa mujibu wa Sheria ya sasa ya Kadhi mtu anaruhusiwa kufungua shauri pahala popote bila ya kujali kama anaishi katika eneo hilo au laa. Jambo hilo linasababisha matatizo makubwa ya upatikanaji wa haki kwa wakati kwa sababu mrundikano wa kesi, kukosekana kwa mashahidi kwa wakati na wakati mwengine kutofika kwa wadau.

6. Ni sheria iliyopo haitaji majukumu ya Kadhi Mkuu na hivyo kukosa muongozo wa kisheria wa mipaka na mamlaka ya Kadhi Mkuu.

7. Sheria pia haibainishi sifa za Jaji wa Mahakama Kuu anayetakiwa kusikiliza kesi za rufaa zinazotoka katika Mahakama ya Kadhi.

8. Mahakama ya Kadhi haina Mrajis wa shughuli zake.

9. Mahakama ya Kadhi haina muongozo maalumu wa matumizi ya lugha katika kuendesha shughuli zake za Kimahakama.

10. Mahakama haielezi mipaka ya kitaaluma na mtu wa kuteuliwa kuwa kadhi.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo haya ya kufuta na kutungwa upya Sheria ya Mahakama ya Kadhi yana msingi wa Kikatiba. Kifungu cha 12 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinazungumzia usawa mbele ya sheria na ulinzi wa maslahi ya raia wa nchi chini ya uamuzi wa Mahakama pamoja na vyombo vyengine vilivyowekwa na sheria bila ya kubaguliwa. Aidha, marekebisho haya ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya mageuzi katika sekta ya sheria.

Pia utekelezaji wa kifungu cha 7 cha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 kuhusu Zanzibar kuimarisha Utawala Bora na Utawala wa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii yanatarajiwa kuleta faida nyingi zikiwemo:

1. Kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama ya Kadhi baada ya kuanzisha utaratibu wa utumishi nje ya mahakama;

2. Kurahisisha utendaji na kuijengea heshima Mahakama ya Kadhi kwa kuipa uwezo wa kuwafungulia mashtaka na kuwapa adhabu watu wanaodharau wito wa mahakama hiyo.

3. Kuimarisha mfumo wa kupata msaada wa kisheria kwa kuwaruhusu mawakili wa utetezi kwenye Mahakama ya Kadhi;

4. Wenye utaalamu katika fani ya sheria na sharia na waliosoma kwenye taasisi rasmi ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla mapendekezo hayo yatapelekea kuwepo kwa Sheria Mpya ya Mahakama ya Kadhi itakayokidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye na yatakayosaidia katika kufikiwa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa haki kwa jamii na kuheshimu utawala wa sheria. Aidha, mapendekezo haya yatasaidia sana katika kuzilinda haki za wanawake na watoto ambao ni waathirika wakubwa wa matokeo ya utengano wa familia.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo haya ya sheria mapya, ili kupunguza kasoro za kisheria kwenye mfumo wa Mahakama ya Kadhi sheria mpya inapendekeza mambo yafuatayo:-

Sehemu ya Kwanza, ambayo itahusisha utangulizi. Sehemu hii inajumuisha jina fupi la sheria na kuanza kutumika kwake ufafanuzi wa maneno yaliyotumika na mambo maengine kama hayo.

Sehemu ya pili, inazungumza kuanzishwa kwake Mahakama, Muundo, Mamlaka na Usimamizi wa Mahakama ya Kadhi. Sehemu hii inajumuisha kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi, Muhuri wa Mahakama ya Kadhi, Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi, Matumizi ya Sheria za Ushahidi, Kanuni na utaratibu wa utendaji kazi.

Vile vile, Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Rufaa, Kadhi wa Wilaya, Mrajisi wa Mahakama wa Kadhi, uwezo wa Mahakama ya Kadhi, Mrajisi bajeti na fedha za Mahakama ya Kadhi, Lugha ya Mahakama ya Kadhi, Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, Rufaa kutoka Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, Mahakama ya Kadhi ya Wilaya, Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi ya Wilaya na Rufaa yake.

Aidha Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tatu inazungumzia usuluhishi. Sehemu hii inajumuisha uwezo wa kutoa amri na maelekezo ya kumaliza kesi, uanzishwaji wa kesi kwa usuluhishi na msuluhishi hata utatuzi wa hoja usiri wakati wa vikao vya usuluhishi, muda wa usuluhishi, kuondoa mgororo katika usuluhisi, mwisho wa usuluhishi na hatua za kuchukuwa iwapo usuluhishi umeshindikana.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya nne inaweka masharti ya jumla. Sehemu hii inaweka masharti ya jumla ikiwemo adhabu kwa watakaodharau Mahakama, ushiriki wa wakili na vakili kukubaliwa kwa wakili na vakili, kuingia kwa makadhi na maofisa na kufuta kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Sheria Nam. 3 ya mwaka 1985.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba nichukuwe nafasi hii, kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili rasimu ya sheria hii na hatimaye kupitisha, ili tupate sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi itakayosaidia kupunguza changamoto ziliopo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum karibu.

Mhe. Machano Othman Said: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alikuwa na haraka hakutoa hoja. Sasa sijui naanza na nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Naibu Spika, kama alivyo mwanadamu kupitiwa ni jambo la kawaida. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja ya kile ambacho tunaweza kukiwasilisha.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa kutoa hoja. Tunaendelea.

Mhe. Machano Othman Said: (Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kama kawaida nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ametutujaalia neema ya uhai na uzima mpaka kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kila siku, naomba azidi kutukarimu neema hizo ambazo kwa hakika sote tunazihitaji kwake.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, wakiwemo Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika majukumu yenu ya uongozi, ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hiki.

Aidha, nitumie fursa hii kuishukuru Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa juhudi zao kubwa walizozifanya katika kuufanyia marekebisho mswada huu katika nchi yetu, ambayo asilimia kubwa ya wakaazi wake ni Waislamu.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar pamoja Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria hii, ambayo imekuwa ikileta utata mkubwa katika

utekelezaji wake. Pia, namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuwaongoza vyema watendaji wake kwenye kikao chetu cha kujadili mswada huu, kwa kujibu hoja zote na kujibu hoja zetu vizuri na kuweza kuzitolea ufafanuzi zaidi, na hivyo tukaweza kupata uelewa mkubwa juu ya dhamira ya kuletwa kwa mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kuchangia mswada huu kwa juhudi zao walizoonesha katika kufanikisha Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti mengine yanayohusiana na hayo. Kwani, sote ni wajibu wetu kuweza kuuchangia kwa maslahi ya watu wetu, lakini pia kwa faida ya Waislamu wote wanaoishi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa, kamati inawashukuru wadau hao kwa michango yao mizuri, ambayo naamini itasaidia sana katika kuufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Vile vile, napenda kuwahakikishia kwamba maoni na ushauri wao umezingatiwa na kamati wakati ilipokaa na wizara, ili kupatiwa ufafanuzi kuhusu mswada huu.
Mhe. Naibu Spika, kwa upekee kabisa naomba kutambua mchango wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, ambapo kamati yetu iliwaalika katika kikao kilichojadili mswada huu tulipokuwa na wizara.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inakubaliana moja kwa moja na kufutwa kwa sheria ya zamani na kuanzishwa upya Sheria ya Mahakama ya Kadhi kutokana na changamoto mbali mbali, ambazo zimekuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa sheria hiyo.

Vile vile, sheria hii inaanzisha Fungu la Bajeti na Fedha za Mahakama ya Kadhi, yaani *vote*, jambo ambalo ni muhimu sana katika uendeshaji wa taasisi hii, na pia itaweza kupunguza changamoto nyingi ambazo zimewakabili kutoka na uhaba wa fedha za uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii pamoja na makatibu wangu kwa mashirikiano makubwa ambayo wanatupatia katika kuendesha shughuli zote za kamati yetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba uwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Machano Othman Said Mwenyekiti

2.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul–latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Saada Ramadhan Mwenda	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Nd. Haji Jecha Salum	Katibu

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo kamati yetu imeyafanya. Vile vile naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari wameshapatiwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilikutana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora siku ya Jumatano, tarehe 20 na kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu pamoja na kufanya marekebisho ya kimantiki na kisarufi. Vile vile, wizara iliwasilisha katika kikao hicho mapendekezo ya marekebisho ya mswada huu katika vifungu vifuatavyo: 2, 3, 5, 8, 10, 11, 20, 28 na 33.

Aidha, kamati iliyapokea na kuyajumuisha katika marekebisho ya kamati, ambayo yamewasilishwa ndani ya Baraza baada ya kuvifanyia marekebisho machache pamoja na kufuta marekebisho ya kifungu cha 20.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika baadhi ya vifungu ambavyo kamati imevifanyia marekebisho, kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 2, tafsiri ya neno “Mahakama ya Kadhi” imerekebishwa ili iende sambamba na tafsiri iliyopo katika Mswada wa Kiingereza na baada ya marekebisho hayo sasa itasomeka kama ifuatavyo:

“Mahakama ya Kadhi, inajumuisha Mahakama ya Kadhi wa Rufaa na Mahakama ya Kadhi wa Wilaya, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3 cha sheria hii”.

Mhe. Naibu Spika, aidha, tafsiri ya neno “Mdaawa” imeongezwa kama ifuatavyo: “Mdaawa maana yake ni mdai na mdaiwa katika shauri la Mahakama ya Kadhi”. Kuongezwa kwa tafsiri hii kumetokana na kwamba neno hilo limetumika sana katika mswada huu, hivyo italeta utekelezaji bora kwa watumiaji.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 5(1) aya (a), (b), (c), (d), (e) na (f) zimefutwa na kuandikwa upya kwani maelezo yake yapo tofauti na Mswada wa Kiingereza na uhalisia wake. Baada ya marekebisho hayo sasa aya hizo zitasomeka kama ifuatavyo:-

(a) Ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na hayo;
(b) Nafasi ya wanandoa;
(c) Matunzo na malezi ya watoto;
(d) Wakfu au amana za kidini, hiba na msaada;
(e) Wasia na urithi;
(f) Mgawanyo wa mali ya wanandoa pale ambapo kuna uchangiaji halisi.

Mhe. Naibu Spika, aya (d) imeongezwa katika kifungu cha 8(5), ambacho kinaongeza sifa ya ziada na muhimu katika uteuzi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kitakachosomeka kama ifuatavyo:-

“(d) Mwenye taaluma na uzoefu wa dini ya kiislamu unaolingana na sifa za kuteuliwa kuwa Kadhi”.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na kamati ni kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 9(2), kwa ajili ya kuweka muda wa ukomo wa kuongezwa muda wa utumishi kwa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwekwa kwa muda huo. Mapendekezo ya kamati ni kama ifuatavyo:-

“Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Rais anaweza kuongeza muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kama atakavyoona inafaa, lakini muda huo hautazidi miaka mitano (5)”.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati ilifanya marekebisho katika kifungu cha 13(3) kwa kufuta maneno “*Qur-an* na *Sunnah*” yaliyojitokeza mwishoni mwa kifungu hicho na badala yake kuweka maneno “Sheria ya Kiislam”. Kamati imeona ni vyema kuyafuta maneno hayo kwa sababu tayari yameshajumuishwa katika tafsiri ya Sheria ya Kiislam.

Mhe. Naibu Spika, nina imani kuwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu, wamepata fursa ya kuupitia kwa kina mswada huu, na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri serikali kuhusu utekelezaji bora wa sheria inayotarajiwa kutungwa.

Mhe. Naibu Spika, hivyo ni matumaini ya kamati kwamba, Wajumbe wa Baraza hili Tukufu, watauchangia, wataujadili ipasavyo na hatimaye kuupitisha mswada huu ikiwa ni sehemu ya jukumu la Baraza, na hatimaye kuipa fursa serikali kutekeleza sehemu ya jukumu lake la utekelezaji wa sheria itakayotungwa.

Mhe. Naibu Spika, nachukuwa fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wa uwasilishaji wa hotuba hii.

Kamati inawaomba waujadili kwa kina na hatimaye kuupitisha kwa lengo la kuuboresha, kwa ajili ya kuweka misingi mizuri ya Mahakama ya Kadhi katika kuendesha majukumu yao ya kuwahudumia Waislamu wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri sote tunafahamu umuhimu wa mswada huu. Kwa kuwa mswada huu utasaidia sana katika kuleta haki mbali mbali za wananchi, ningeomba sana tuweze kutoa maoni yetu pamoja na kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, mpaka hivi sasa ninao wachangiaji wawili tu, na mchangiaji mmoja yupo hapa ndani mwengine sijui amekimbilia wapi. Lakini ameleta jina lake na natarajia kwamba nitapata wachangiaji wengine.

Hata hivyo, nina ombi langu na maswala ambayo vile vile yanatugusa sisi akina mama. Kwa hiyo, ningewaomba na akina mama wachangie katika mswada huu, ili tuwatendee haki wanawake wengine ambao wametuleta hapa.

Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe na wengine wote wachangie naanza na Mhe. Rashid Makame Shamsi, baada ya hapo nitamwita Mhe. Mohamed Said Mohmed na atakayekuja baadaye nitamtaja jina lake. Mhe. Rashid Makame Shamsi karibu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya mwanzo katika kuuchangia mswada huu muhimu kama

ulivyotangulia kusema unaohusika na Sheria ya kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3, ya mwaka 1985 na kuanzisha upya Mahakama hii ya Kadhi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi, vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kuuleta mswada huu muhimu kwa taifa letu.

Lakini niipongeze sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum chini ya Mwenyekiti Mhe. Machano Othman Said kwa uchambuzi wao wa kina na kupendekeza marekebisho mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni muhimu sana na mswada huu kabla ya kuletwa hapa maelezo ya nyuma yanaeleza kwamba ulifanyika utafiti wa kina wa kuweza kuitazama Mahakama ya Kadhi, ambayo sheria yake tunaifuta au tutaifuta kupitia mswada huu. Miongoni mwa matokeo ya utafiti ule ilikuwa ni kuondoka au kupungua kwa imani kwa wananchi wengi wa Zanzibar juu ya uendeshahi wa Mahakama ya Kadhi. Hiyo imo katika maelezo.

Sasa kama wananchi wa Zanzibar wameondokwa na imani wengi wao juu ya kuwepo Mahakama hii ya Kadhi, ningependa sana kabla ya kuchangia niwaombe sasa watendaji wetu wa Mahakama hizi za Kadhi kuwa waadilifu, kwa sababu wananchi wanapokosa imani maana yake inawezekana malalamiko zaidi yanakuwa katika uadilifu.

Kwa hiyo, niwaombe sana tukinda sheria hii mpya, basi wale baadhi kwa sababu najua sio wote wale baadhi ya Makadhi ambao wamekosa uadilifu na kuweza kulalamikiwa na wananchi basi wabadilike, ili kuweza kuona kwamba Mahakama hizi zinatenda haki. Mhe. Naibu Spika, inawezekana kwamba kutokana na kutotenda haki, ndio maana wenzetu akinamama na wao wanao utetezi wao juu ya hili kwa sababu wanahisi kwamba haki hazitendeki.

Mhe. Naibu Spika, niombe sana Mahakama hii sasa kwa sababu tunapisha sheria mpya hii basi wabadilike, ili kuweza kuona kwamba mama zetu, dada zetu, watoto wanatendewa haki. Kwa maana hiyo, isije ikawa tena inasikika kwamba kadhi kaachisha ndoa au katengua ndoa halafu mke yule yule kamuoa yeye, hayo ndio malamiko sana yanayotoke, sasa tubadilike. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikienda ndani ya mswada huu pamoja na kwamba kuna jaduweli yangu ambayo nilitanguliza, lakini kuna mambo mengine ambayo nataka niyazungumzie ambayo yanaweza kusaidia katika kuweka sawa mswada huu.

Jambo la kwanza katika sehemu ya kwanza ukurasa wa 126 kifungu namba 2 kuhusu ufafanuzi wa maneno. Hapa ningependa kushauri tu kwamba maneno haya kwanza tukumbuke kuyaweka katika mfumo ule wa kiherufi, ili yake vizuri zaidi.

Lakini la pili katika hapa ni neno ambalo limetafsiriwa "Ulamaa". Mhe. Naibu Spika, tafsiri imetaja sheria ya Ofisi ya Mufti Nam. 9 ya mwaka 2001 juu ya neno hili ambalo linasomeka kama "Ulamaa" ambayo imesema kwamba "Ulamaa" maana yake ingawa wenzetu wamerekebisha lakini inabaki tu kwamba ni mtu mwenye taaluma ya dini wenzetu wamelirekebisha. Lakini aliyeteuliwa kuwa "Ulamaa" chini ya Sheria ya Ofisi ya Mufti ambayo nimeitaja namba 9 ya mwaka 2001, baada ya kuipitia sheria hii ambayo ninayo mezani hapa. Kwa kweli, hakuna kifungu ambacho kimewekwa kwa ufasaha juu ya tafsiri na uteuzi wa Ulamaa. Sasa hili neno wakati lime-*refer* sheria hii sijui tutasemaje.

Kwa hivyo, naomba ufafanuzi juu ya tafsiri hii na sheria iliyotajwa kwamba sheria hiyo hilo neno halikuzungumzwa kwa ufasaha ambayo itakuwa-*refered* katika kuitolea tafasiri. Lakini nishauri tu Mhe. Naibu Spika, katika mlolongo wa maneno haya basi neno Wakfu nalo lingetolewa ufafanuzi.

Nawashukuru sana wenzetu waliliona neno mdaawa ambalo wamelitoa katika mapendekezo yao. Lakini nikija katika sehemu ya pili katika ukurasa wa 127, pendekezo la neno la pembeni, kifungu namba 3(1) na 3(2). Mhe. Naibu Spika, katika vifungu hivi viwili, yaani kifungu kidogo cha (1) na cha (2) katika kifungu cha 3. Kifungu cha mwanzo namba 1 kimezungumzia juu ya uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi. Lakini kifungu cha 2 kimezungumzia muundo.

Kwa hivyo, ninapendekeza kwamba neno la pembeni lingesomeka kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi na muundo wake, kama halitoonekana ni refu basi ninapendekeza liwe hilo, kwa sababu hata tukiangalia ile *heading* ya juu imezungumzia kuanzishwa, muundo pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Mahakama ya Kadhi. Kwa hivyo, vipengele au vifungu hivi viwili neno lake la pembeni ningependa lisomeke kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi na Muundo wake.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha (3), katika kifungu hiki ninapendekeza kifungu hiki kihamishiwe kwenye kifungu namba 19 cha ukurasa wa 132, ambapo neno la pembeni linasomeka Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya. Kwa kweli, nina imani kwamba katika kifungu hicho namba 19 ambacho kiko katika

ukurasa wa 132, kifungu hicho kimezungumzia juu ya Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi.

Sasa kifungu hiki cha (3) ambacho napendekeza kihamishwe, nacho ni kifungu ambacho kinasomeka Mahakama ya Kadhi wa Wilaya itakuwa na Mamlaka ya awali ya kusikiliza Kesi za Madai kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 5 cha sheria hii. Kwa hivyo, kifungu hiki kingehama kikaelekea hasa kule ambapo kuna yale Mamlaka hasa ya Mahakama ya Kadhi ya Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, nije sasa katika kifungu cha 5(2). Mhe. Naibu Spika, nakinukuu kifungu hiki, kinasema "bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki, mtu yeyote ambaye sio Muislamu anaweza kufungua kwa shauri katika Mahakama ya Kadhi dhidi ya Muislamu, kwa masharti ya madai yanayohusu Sheria ya Kiislamu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hiki baada ya kutazama ile *version* ya Kiingereza ambayo imeanza, "*without prejudice the provision of sub section (1) of this section, any person may submit a claim to the Kadhi's Court for any matter that the Kadhi's Court have jurisdiction. "*

Mhe. Naibu Spika, hapa katika kifungu hiki cha Kiingereza hakikusema mtu yeyote ambaye sio Muislamu, kimesema *any person may submit*, yaani mtu yeyote. Sasa unaposema mtu yeyote asiwe Muislamu maana yake umeweza kuipindua hii tafsiri katika *version* ya Kiingereza. Kwa hivyo, ningependa neno hili liondoke na libaki kwamba ni *any person*, kwamba ni mtu yeyote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, *otherwise* kama kuna lolote ambalo linabatilisha hili, basi tubadilishe *version* ya Kiingereza kwanza, halafu tuweze kuweka hii kama kuna mantiki yoyote ambayo inafanya iwe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 8(1) kwenye ukurasa wa 127 ambacho kinasema, "kutakuwa na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa.

Mhe. Naibu Spika, suala la Baraza la Ulamaa mimi sijaliona katika Sheria ya Mufti Nam. 9 ya mwaka 2001. Sasa hoja ambayo naileta hapa ambayo Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kutuwekea sawa ni kwamba Baraza la Ulamaa lipo kisheria na kama lipo kisheria ni sheria namba ngapi, ya mwaka gani na kifungu gani, ambayo inahalalisha sasa hapa uwepo wa Baraza hili la Ulamaa,

kwa sababu kama Baraza la Ulamaa halikutajwa katika sheria yoyote, basi hapa patalazimika kuwepo na mabadiliko.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 17(5) ambacho Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hiki anatakiwa awe Muislamu mwanamme, sasa imekomea hapo awe Muislamu mwanamme. Kwa kweli, Waislamu wanaume tuko wengi sana na inawezekana tuna taaluma hiyo ya Ujaji.

Nashauri kwamba tuongeze maneno, huyo Jaji Muislamu mwanamme lakini awe ni Muislamu mwenye uadilifu, kwa sababu tunaweza tukawa na Majaji Wailsamu, lakini katika masuala haya au mashauri haya anawezekana asije akatenda haki. Kwa hivyo, suala la uadilifu kwa Jaji huyu, napenda liongezwe hapo ili kuwapata Majaji ambao ni Waislamu, lakini watakuwa wana uadilifu katika kuhukumu kesi hizi zinazohusiana na haki za wananchi wetu.

Katika kifungu cha 15 Mhe. Naibu Spika, nashauri kuna neno la kiapo kwa mkalimani. Imetaja tu pale katika kifungu hicho cha 15 kwamba mkalimani ataapa mbele ya Mahakama ya Kadhi au Mrajis wa Mahakama ya Kadhi. Ningependa hili neno la kiapo turekebishe kidogo lisomeke, "Mkalimani atakula kiapo cha utii au cha uadilifu" na hususan katika neno la Kiingereza ambalo limetumika neno *oath* ambalo kwa tafsiri ni *selenium promise*.

Kwa hivyo, hicho kiapo ni lazima kiwe na maneno ya nyongeza, kiwe kiapo cha utii au cha uadilifu, kwa sababu tunaweza tukawa na wakalimani ambao wanaweza kutusaidia, lakini na wasile kile kiapo hasa tunachokitaka. Hivyo, kiapo hiki kiwe ni kiapo cha utii au kiapo cha uadilifu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe wenzetu waweze kuuchangia mswada huu, kama ulivyopendekezwa na hususan wajumbe akinamama, kwa sababu malalamiko mengi yanahusu ndoa katika Mahakama zetu na yanawagusa wanawake na watoto wetu. Kwa hivyo, ni haki yao na nifursa pekee hivi sasa ya wao na wao kuweza kuuchangia mswada huu, ili kuweza kuona kwamba tukianza ukurasa mpya wa Mahakama hii mpya ya Kadhi basi tunaanza vizuri.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na mimi niseme tu naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia mswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, na sasa tunampa fursa Mhe. Omar Seif Abeid na baadaye Mhe. Mohmed Said Mohamed.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu. Lakini sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa *Allah Subhanahu Wataalla* aliyetujaalia tukakutana hapa baada ya muda wa siku kadhaa zilizopita, wengi tulikuwa hatujaonana katika Baraza hili. Lakini kwa uwezo wake yeye Mwenyezi Mungu katujaalia katukutanisha tena.

Kwa hiyo, naendelea kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie atuendelezee kutukutanisha wakati wote mpaka tutakapomaliza muda wetu wa kikao na Mwenyezi Mungu atuzidishie mapenzi miongoni mwetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako leo naweza kusema kwamba mswada ulipo mbele yetu ni mswada muhimu sana. Vile vile, naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuuchangie mswada huu, kwa maana ni mswada ambao unatugusa sisi jamii ya Wazanzibari ambao asilimia 80 ni Waislamu au asilimia 99 ya Wazanzibari ni Waislamu, kuwacha kuuchangia mswada huu tutakuwa hatujatenda haki kwa mujibu wa dini yetu, na kwa mujibu wa Sheria zetu za Kiislamu, ni wakati muafaka ulipokuja mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitakumbukwa kwamba mara nyingi ninaposimama katika mambo haya huwa naiomba sana serikali kuleta miswada ambayo haitakuwa na vipengele vya sheria vinavyokinzana. Sasa mswada huu naupenda, nausifu na ni mzuri, lakini nina wasi wasi mbele tunakokwenda kutakuwa na baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakaja yakaleta mvutano kidogo wa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tukienda katika ukurasa wa 127 kifungu cha 5(1), naomba kukinukuu. Mswada unasema, "Mahakama ya Kadhi itakuwa na Mamlaka ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadawa wake ni Waislamu, kuhusiana na ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa. Kwanza napendekeza hilo neno ndoa liliopo hapo mwisho, kwa sababu huku ndoa imeshatajwa liondoke, ili lisomeke hivi. "Ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na iendelee hapo chini ustawi wa familia, matunzo, malezi na mambo mengine.

Lakini Mhe. Naibu Spika, wasi wasi wangu ambao unanipa juu ya kifungu hiki, kwa sababu ikiwa Mahakama ya Kadhi, ambapo sheria hii tunaipitisha hapa leo, tunasema itakuwa na mamlaka juu ya mambo haya yote ya Kiislamu, kuna baadhi ya mambo Mhe. Naibu Spika, yametokeza na yanatokeza ambayo yanaendelea na yataendelea kuja.

Kwa mfano, inapotokea mtoto wa kike kenda Mahakamani kwa Kadhi kutaka aozeshwe, ikiwa yuko chini ya umri wa miaka 18 tutasimamia sheria gani au tutasimamia kipengele gani. Mhe. Naibu Spika, tukitizama sheria, kanuni zetu tuiangalie ile Sheria ya Elimu kwanza tuiangalie ile Nam. 6 ya mwaka 1982. Sheria juu ya elimu inakataza kwa ujumla katika kifungu cha 20(3), kinasema kwamba "mwanafunzi wa shule ya msingi au na sekondari awali hawezi kuolewa". Tukijitizama kwa wanafunzi wa msingi na sekondari wako chini ya umri wa miaka 18, lakini sheria hii kwa mujibu wa Sheria zetu sisi za Kiislamu, mambo matatu Mtume kayahimiza.

Jambo la kwanza ni kwamba mtoto wa kike anapopata ukubwa aolewe. Jambo la pili wakati wa Sala ukifika pasaliwe. Jambo la tatu, mtu akifa azikwe. Sasa inapotokea mtoto wa kike, kama nitakuwa nimekosea jamani mtanisamehe, kapata ukubwa ndani ya miaka 12, kenda Mahakamani kwa Kadhi kadai aozeshwe, Kadhi akisimamia sheria hii na Sheria hii ya Kumlinda Mwari na Mjane tutasimamia sheria gani.

Mhe. Naibu Spika, naomba hii sheria iwekwe vizuri tuitengenezeni isiwe inakinzana, kwa sababu hapa Kadhi anaweza kusimama kwa sheria na kwa sababu tumempa akawa yuko kwenye *right*, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Sheria ya Kumlinda Mwari na Mjane ipo, Sheria ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kutokumruhusu mtu kuozeshwa ipo haijafutwa, tutasimamia sheria gani. Hilo la kwanza.

Jambo la pili, sisi tunasimamia Mahakama ya Kiislamu, sasa itakapotokea kwenye kifungu cha 7, kinasema Jaji Mkuu atashauriana na Kadhi Mkuu, inapotokea kwamba Jaji Mkuu sio Muislamu, japokuwa kuna lile jopo ya wale watu ambao watamzunguka. Lakini yeye Jaji Mkuu kwa sababu ndiye *head* alitakiwa na yeye awe anazijua Sheria za Kiislamu, kwa nini hapa tunaye Kadhi wa Rufaa au Kadhi Mkuu asisimame kwa niaba ya Jaji Mkuu lazima aingizwe Jaji Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, napendekeza hapa kwamba Kadhi Mkuu ndiye awe Mshauri Mkuu ashauriane na hawa Makadhi wa Rufaa na wengine. Mhe. Naibu Spika, hili litatusaidia sisi kuondosha *conflicts* nyingi ambazo zinaweza kuja kujitokeza kama tulivyokuwa tunasoma sana kule kwenye sheria tumekwenda kule.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana UWAWAZA mumetuelimisha na hili moja tulilizungumza siku ile, kwamba mwisho wa safari, mwisho wa rufaa Mahakama Kuu ndio inaisimamia Mahakama ya Kadhi inapotokea kama tumekwenda kule. Mahakama ya Kadhi imetoa uamuzi wake, lakini mtu hakuridhika na Mahakama

ile anakwenda kukata rufaa kwenye Mahakama Kuu ya Rufaa, bado inakuwa ule msingi mzima wa Kiislamu kwa zile Sheria za Kiislamu utakuwa haupo, itabidi turudi katika mfumo ule ule wa Kimahakama.

Mhe. Naibu Spika, napendekeza pamoja na kuwaomba sana wataalamu wetu wa sheria waitizame na wampe nguvu Kadhi Mkuu, kuanzia Mahakama ya Kadhi ya Wilaya mpaka kama kuna hiyo *supreme level*, yote iwe iko kwenye mtiririko mmoja, isiwe kuna mitiririko miwili kwamba akitoka kwenye Mahakama ya Kadhi mwisho *final* anakua Mahakama Kuu. Jambo hili litatusaidia sana sisi katika kuweka vizuri mambo yetu.

Naizungumza hii kwa tahadhari ambapo itatokea kwamba mtu kakata rufaa. Kwa mfano, leo Mhe. Naibu Spika ninafahamu kwamba kuna kesi kuna watoto wako chini ya umri wa miaka 18 wamekwenda Mahakamani wanaomba waozeshwe waume sheria inakataza, lakini kwa sababu ya Dini ya Kiislam mtoto yule ana haki ya kuozeshwa mume sasa, na sisi tunasema tumlinde mtoto kwa sababu mtoto ni mtoto wetu.

Sasa, mambo haya ni vizuri wakati wa kutengeneza sheria siwatoi makosa, isipokuwa natoa ushauri au ombi kwamba mambo haya yaangaliwe kwa upana zaidi, yaangaliwe kwa kina sana, kwa sababu sisi sote wengi wetu ni Waislam na tunayoizungumza hapa ni Mahakama ya Kiislam. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 130 nimekuta kitu kimoja kwenye 13(7) ukurasa wa 30 kinasema kwamba.

Kifungu 7, ombi lilifanywa chini ya kifungu kidogo cha 6. Mhe. Naibu Spika, napendekeza baada ya kutamkwa ombi lilifanywa itamkwe ombi lililofanywa.

Vile vile, hapa kifungu cha 14 Mahakama ya Kadhi itakuwa na fungu lake la bajeti ambamo. Pia nilikuwa naona tungeandika Mahakama ya Kadhi itakuwa na fungu lake la bajeti ambalo litaingizwa fedha.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la mswada huu ni muhimu nachukua fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kafanya kazi kubwa sana, kwa kweli nimejaribu kusoma mwingi lakini nilipotizama marekebisho kila ninapopita yeye ameshaparekebisha. Kwa hiyo, nampongeza Mwenyekiti pamoja na Kamati wamefanya kazi kubwa ya kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Lakini pia tukirudi tena kwenye ukurasa wa 131 kifungu tunazungumzia tena kuhusu hizo rufaa ambayo hapo mwanzo nimeshaizungumza, nimezungumza kwa kina suala la rufaa, kwa sababu lengo letu la kuanzishwa Mahakama hii ya Kadhi ni kutekeleza yale ambayo yamewekwa katika kifungu cha 5(1), basi narudia tena msisitizo wangu Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu hichi cha kwanza cha 17(1) kifanyiwe marekebisho kuhusu utaratibu wa rufaa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la usuluhishi 133, kwamba msuluhishi pale ambapo huduma ya mtaalam inaweza kupatikana bila ya malipo bila ya gharama au mbo mengine, ninachokusudia kukizungumza ni suala zima la usuluhishi. Kwa maana hiyo, suala la usuluhishi katika Dini yetu sisi ya Kiislam ni kitu muhimu ambacho kimesisitizwa sana ni vyema ikawepo.

Lakini naomba kupendekeza kwamba hawa wasuluhishi waweze kufanywa hata nje ya Mahakama kama ilivyoelezwa, yaani hata nyumbani kwa msuluhishi na ikiwezekana kwenye sheria hii suala la usuluhishi liwemo hasa kisheria kwama moja katika njia ya kumaliza mambo haya ya ndoa na talaka utumike zaidi usuluhishi kulikoni hukumu, kwa sababu tumeona kwamba unapotumia usuluhishi Mwenyezi Mungu anatwambia kwamba itakapotokea mke na mume wamegombana, basi fanyeni usuluhishi Mwenyezi Mungu anasema kwamba suluhu ni bora.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tunapofanya suluhu tunawarejesha watu kwenye umoja wao waliokuwa nao wa asili, tunafanya mapenzi yarudi ambayo hayakuwa na mizozo. Lakini, kama tutaendelea kutumia zaidi Mahakama kwenye masuala ya ndoa bila ya kufanya usuluhishi zaidi, tunajenga au tunachochea sitofahamu kama alivyosema Mhe. Rashid Makame Shamsi, kwamba baadhi ya Makadhi ambao tunawapa sheria wanakuwa hawatumii zaidi uadilifu pamoja na kuwa sheria wanakuwa wanayo.

Mhe. Naibu Spika, napendekeza na naomba sana hili suala la usuluhishi liwekwe moja kwa moja kwenye sheria, kwamba moja katia ya kuamua mizozo ya ndoa ni kufanyika kwa usuluhishi jambo hili litatusaidia na litaondoa chuki kama nilivyosema.

Katika kifungu cha 24, kinasema naomba kunukuu:

> "Mdaawa katika Kikao cha Usuluhishi atakuwa na haki ya kutatua hoja yoyote wakati wa Kikao cha Usuluhishi".

Haki ya utatuzi wa hoja katika Mahakama ya Kadhi ni kitu muhimu sana, hasa kuhusiana na mambo ya ndoa na mirathi. Mhe. Naibu Spika, ni mambo ambayo yanagusa sana familia, na kama tutatishindwa kuyamudu kuyafanyia usuluhishi tunaweka na tunachochea migogoro ya muda mrefu hatimaye kuzifarakanisha familia.

Mhe. Naibu Spika, nawapongeza sana waliozungumza jambo la usuluhishi wamekwenda mbali na wameona jambo zuri, nawapongeza na nawaomba sana Makadhi ambao wanasimamia Mahakama za Kadhi kutumia zaidi usuluhishi kulikoni kufuata sheria, mambo haya Mhe. Naibu Spika ya kusimamia haki hasa kwenye mambo ya talaka ni mambo mazito.

Kwa kweli, tunawapa mizigo mizito Makadhi na Makadhi wafahamu kwamba wana kitanzi katika shingo zao. Kwa hivyo, wakati umefika sheria nzuri imekuja sheria ambayo sisi ni wajibu wetu kama nilivyorejea kuzungumza kwamba tuichangie kwa kina, ili ipate mapana ya kazi tuwape uwezo na uelewa Makadhi ya hii sheria waweze kuitumia, kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu ambao wengi wao ni Waislam.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kwa leo sina mchango mkubwa. Baada ya haya, nasema sina pingamizi yoyote juu ya mswada huu na ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, niendelee kukushukuru sana kwa kuniona. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, vile vile niwapongeze serikali kwa kuja na dhana nzima ya Mswada huu wa Kadhi. Lakini shukurani za pekee kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wake. Mhe. Naibu Spika, bila ya kuwasahau na niendelee kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na ubora wa kuchangia hotuba hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme moja tu la ziada, kubwa tunaipongeza serikali kwa kuja na mswada huu na moja kwa kuwa utakuwa na fungu lake wenyewe, itakuwa inaweza kujiamulia mambo yake wenyewe. Lakini niseme tu sheria hii sitaki kuwa na wasi wasi nayo hata kidogo. Kwanza, kwa sababu wamesema wataalam wamefanyia utafiti wa kutosha, lakini na mimi nikajaribu kuleta *shadow of amendment* ambayo nimeileta kwako Mhe. Naibu Spika, ili basi Waheshimiwa Wajumbe waione na ikiwa ipo hawa watuunge mkono kuweza kuunda Sheria nzuri ya Mahakama ya Kadhi.

Mhe. Naibu Spika, nianze katika kifungu cha 5 cha mswada huu. 1 inasema Mahakama ya Kadhi itakuwa na Mamlaka yake ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadaiwa ni Waislam na kuhusiana na hapa yametajwa orodha moja ya orodha zao zimetajwa, ilikuwa ndoa talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu watu wetu wengi walikosa imani na Mahakama hizi na kukosa imani na Mahakama hizi hasa hasa Makadhi wetu walikuwa wanaendesha sivyo na makarani wao ambao waliwazidi kielimu ya kisheria. Sasa ulikuwa unakwenda pale ndoa zinatenguliwa tu, lakini nataka nitoe ushauri, kubwa langu nataka niseme ukienda kuangalia Mahakamani talaka zimezidi kuliko ndoa.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika tuwaombe serikali, Ofisi ya Kadhi, Mufti pamoja na Mashehe wetu kuanza kuwafundisha vijana wetu wanapotaka kuoana wote wawili dhana ya ndoa ya Kiislam ni nini, ili basi waweze kujua hatimaye zipungue hizi talaka na tuweze kuona hawendi Mahakamani kuomba talaka hizi mara kwa mara au migogoro katika familia kupungua kutokana na sheria hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika kifungu cha 3 kinasema hivi naomba kunukuu.

> "Kila Kadhi atakuwa na Mamlaka ya kusikiliza kosa lolote la kudharau Mahakama inayofanywa kuhusiana na ofisi yake na atakuwa na uwezo wa kuto adhabu kwa mujbu wa sheria hii na kanuni zilizotungwa kwa ajili hiyo".

Mhe. Naibu Spika, sentensi imekaa vizuri sana lakini kitu kimoja ambacho nakiona hakiko sawa, moja tujue dharau hiyo ni dharau gani, kwa sababu anaweza kwenda Mahakamani mtu kusikiliza kesi ya mwengine. Lakini pengine kakaa upande na kanuni inamwambia ukikaa hivi tayari umedharau Mahakama, tutakuwa tunamtia hatiani kwa kosa ambalo hakulitenda. Kwa hivyo, naomba sana tuweze kuiandika vizuri na tujue kanuni hizi zinaelekeza vipi, ili basi tusije tukawatia hatiani watu wasiokuwa na hatia.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu cha 7 naomba kunukuu.

> "Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi Mkuu atatunga kanuni za Mahakama ataandaa Kanuni za Utaratibu na utendaji kazi unaotumika katika Mahakama ya Kadhi".

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuleta *shadow of amendment* na nimesema kiongezwe kipengele cha pili ambacho kitasomeka kama ifutavyo.

> "Kanuni zitakazotungwa chini ya kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki hazitatumika katika kucheleweshe au kumkosesha mdaiwa kupata haki zake kwa msingi wa taratibu tu".

Mhe. Naibu Spika, zipo taratibu nyingi katika sheria mtu anaweza kwenda pale na *affidavit* akaambiwa hii ipo kesi hii haisikilizwi. Sasa kwenye Mahakama hii tungeomba zisiwepo hizi au jina langu naitwa Muhammed nimeandikwa kwa Mo, lakini kwenye *certificate* yangu ina Mu naweza kuambiwa kwa jambo hili hatuwezi kusikiliza kesi yako. Kwa maana hiyo, tuwaombe wenzetu hizi katika Sheria za Kiislam, mambo haya madogo madogo tuweze kuyaepuka tusiweze kuyashughulikia na kumkosesha mdaiwa haki yake.

Mhe. Naibu Spika, niendelee tena katika kifungu cha 8 ambacho kinasema hivi, naomba kunukuu.

> "Kutakuwa na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais na kutokana na mapendekezo ya Maulamaa".

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na hayo lakini nimesema tu, katika kifungu cha 10 huku naomba ninukuu.

> Kifungu cha 10(3)b awe na umri angalau miaka 40.

Mhe. Naibu Spika, naomba na huku tuweze kuweka tu basi hawa watakaoteuliwa na Mhe. Rais Kadhi au Naibu Kadhi Mkuu, basi wawe na miaka 40, kwa sababu gani nikapendekeza hivyo. Kwa kweli, miaka 40 ndio tunaambiwa katika dini yetu tunaanza kupata ushahidi tunaanza kuwa na akili timamu. Kwa hivyo, napendekeza na hapa tuingize basi miaka 40 iwe sambamba au liwe tamko sambamba na kile kifungu cha 10 chenye fasili (b).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu cha 8 ni hicho ambacho nimekisema, lakini sasa naendelea na kifungu cha 9.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 9 kinasema na naomba kunukuu.

"Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu atabaki katika nafasi yake mpaka atakapofikia umri wa miaka 60, ambapo anaweza kustaafu kwa hiyari au miaka 65 ambapo atastaafu kwa lazima".

Mhe. Naibu Spika, sitaki kuwa na tatizo hapo, lakini ninapendekeza tu kisomeke nimebadilisha na kuweka cha pili kisomeke kama hivi ifuatavyo.

Masharti ya kifungu cha kwanza ya kifungu hikiyatatumika kwa Kadhi wa Rufaa na Kadhi wa Wilaya, kwa sababu hii isionekane tu wale Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu lakini kitumike na Kadhi wa Wilaya au Kadhi wa Mahakama Kuu uwe umri ni huu huu kutokana basi umri huu wa kustaafu ndio tayari watu wamechoka, tukiweza kuwazidisha au tukiwa hatukukisema kwenye sheria tutaendelea kusema Naibu Kadhi na Kadhi Mkuu pekee haitokuwa sawa. Hivyo, naiomba sana serikali hichi nacho ikione na kama upo utaratibu basi ituletee kitu kama hichi tuone mwisho utakuwaje.

Mhe. Naibu Spika, nije tena kwenye kifungu hichi cha 10 nimeshakisema pamoja na yale lakini nilisema tuongeze fasili (c) umri wa angalau miaka 40.

Kifungu cha 10 fasili ya 4 naomba iongezwe sasa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hichi kitakuwa na Kadhi Mkaazi wa Rufaa atakayekuwa Pemba ambaye atasikiliza rufaa kutoka Mahakama za Wilaya za Pemba.

Mhe. Naibu Spika, tumeona mengi kuna Hakimu Mkaadhi Pemba na hili linapigiwa kelele siku sote kuwe na Hakimu Mkaazi Pemba, ili basi tuone kesi hizi zinashughulikiwa kwa haraka zaidi. Sasa tukiwa hatuna Kadhi Mkaazi hapa Pemba zote za rufaa itabidi ziletwe Unguja au aone *time* ya kwenda kule, nadhani itakuwa tunachukua muda mkubwa na tunaweza tukaona ile dhana nzima ya mswada huu na sheria tunayotunga haitokuwa na dhana kamili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende tena lakini mwingi nimeshatuma *amendment* yangu, lakini niende tena kwenye hichi kifungu cha 10 nikasema, naomba kunukuu.

"Kadhi au Naibu Kadhi Mkuu anaweza kuondolewa katika madaraka kwa kushindwa kutekeleza haki zake au kwa sababu ya tabia mbaya kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Katiba ya Zanzibar katika kumuondoa Jaji wa Mahakama Kuu".

Hivyo, kule tumeweka jinsi gani Kadhi anaweza kuondolewa lakini humu kwenye sheria hii tulikuwa hatukuweka vipi tunaweza kumuondoa na hapa kama utaona tumeweza kuona akifika miaka 60 au 65 aweze kustaafu. Lakini, kuna mambo haya tunaweza tumeyaleta tuone Kadhi anaweza kufanya mambo mabaya au amekiuka maadili, lazima aweze kuondolewa kazini kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Sheria za Mahakama zinavyokuwa.

Jambo jengine ni kuhusu utaratibu ulioainishwa katika kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hichi utatumia pia kwa Kadhi wa Rufaa, na Kazi wa Rufaa vile vile tunatakiwa atumie tena sheria ile ile ya kuweza kuwaondoa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabla ya yote katika kifungu cha 12, naomba kunukuu.

> "inaanzishwa Afisi ya Mrajis wa Mahakama ya Kadhi ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupendekezwa na Kadhi Mkuu".

Sasa nimesema hii lugha kidogo hapa haijakaa sawa nikajaribu kuirekebishwa inaanzishwa siokutazwa inaanzisha Afisi ya Mrajis wa Mahakama ya Kadhi itakayoongozwa na Mrajis wa Mahakama ya Kadhi na atakaeteuliwa na Kadhi Mkuu baada ya kupendekezwa na Baraza la Maulamaa.

Nilisema hili tuweze kuweka lugha tu iwe sawa na tuendane sana. Mhe. Naibu Spika, nilisema nichangie hayo na nimeleta *shadow of amoment* yangu na ninadhani Waheshimiwa Wajumbe wameipata. Hivyo, naomba waniunge mkono, ili sheria hii iwe nzuri kwa mujibu tunavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, nitaunga mkono hoja hii, nitakapoona majibu ya serikali. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana kwa mchango wako mzuri Mhe. Mohamed Said Mohamed. Mchangiaji anayefuata Mhe. Simai Mohammed Said na baada ya hapo atafuta Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi. Nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia kufika leo sote hapa kuwa wazima na afya.

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi walioteuliwa nafasi mbali mbali katika majimbo yetu wakati chaguzi

zetu zinaendelea za ndani kwa kuweza kuibuka kishindo cha kishindo. Lakini wakati bado mchakato unaendelea basi na sisi pia tutaendelea kushirikiana nao, huku tukiendelea kujibika na kazi zetu hapa za Barazani, kuwatetea na kuwa wasemaji wao.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza marafiki zetu wakubwa Jamhuri ya Watu wa China kwa kutimiza miaka 68 jana juu ya taifa lako. Kwa hiyo, tunawapongeza sana na mimi kama Mwenyekiti wa Tawi la Zanzibar la *Commonwealth Parliamentary Association (CPA)* na Kamati yetu yote basi tunaungana nao pia kwa pamoja. *(Makofi)*

Kwa kweli, leo Mhe. Naibu Spika nimehumiwa, kwa sababu kila ninachoshika katika hichi kifungu huku kunakuta kamati husika imefanya kazi nzuri kabisa ambayo siyo kawaida maana yake unapoangalia lazima utakuta marekebisho.

Lakini cha ziada pia nimepata tabu zaidi niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wawili hasa Mhe. Mohamed Said Mohamed, ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti kwa jinsi ya vifungu alivyovileta tena na maandishi yake pamoja na marekebisho aliyoyaleta. Kila kifungu ukikamata katika hii sheria leo tayari mapendekezo yameshakuja. *(Makofi)*

Vile vile, pongezi ziende kwa Mhe. Rashid Makame Shamsi, huyu ni mtaalamu wa kuangalia haya maandishi ambayo yamo katika hizi sheria, lakini pia na mapendekezo yaliyoyaleta ukiangalia leo hapa Mhe. Naibu Spika, mambo yako mazuri kabisa. *(Makofi)*

Sasa mchango wangu kwa kweli utakuwa ni mdogo sana vitu viwili Mhe. Naibu Spika.

Jambo la kwanza tunaomba sana katika baada hii sheria, kwa sababu hii sheria tutaipitisha naamini tutaipitisha. Hizi Mahakama zetu tunakwenda kuzianzisha huko, basi wafanye kazi kwa bidii haya majina na utani leo yanayozungumzwa nje katika Mahakama zetu hizi, kufika kuitwa mahakama za kimapenzi, basi haya tuyaondoshe wananchi na Waislamu wote waweze kupata huduma ambazo wanazotarajia. Kwa kweli, serikali imekuja na nia njema, na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi naamini na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu hapa pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu tutaunga mkono mia juu ya mia na tuweze kuipitisha sheria hii.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu Makadhi ya Wilaya, ukenda katika kifungu Nam. 11 kinasema, naomba kunukuu.

> "kutakuwa na Kadhi wa Wilaya katika kila wilaya ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama baada ya kupendekezwa na Jaji Mkuu".

Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi una watu karibu 600,000 na kama sio zaidi, yaani Mkoa wa Mjini Magharibi una watu wengi kuliko hata Kisiwa cha Pemba, Mkoa wa Mjini Magharibi una watu wengi inawezekana ukiunganisha Mkoa Kusini na Mkoa wa Kaskazini, basi ukawaleta Mkoa wa Mjini bado kuna watu watabakia.

Lakini Mkoa wa Mjini una wilaya ya mbili. Mhe. Naibu Spika, sasa hapa naomba kushauri katika suala zima la kuchagua hawa Makadhi wa Wilaya, upatikane utaratibu ambao hawa Makadhi wa Wilaya watakuwa na watu wa kuwasaidia, ambapo sheria imruhusu.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu aibebe hii pamoja na waziri mwenye dhamana, ili kuhakikisha pale wananchi watakapokwenda kupata hii huduma na kuomba yale ambayo wanayataka katika Mahakama hizi zetu za Kadhi. Hivyo ni vyema, waweze kusaidiwa pasiwe na ucheleweshaji wa mambo kwa makusudi, ili serikali ikaanza kulaumiwa pamoja na vidole kunyooshewa waziri au makakama ambayo inahusika na masuala haya. Kwa hiyo, naomba sana katika kifungu hichi, basi waziri ajitahidi sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nikuombe wewe leo katika asubuhi hii, kwamba kwa upande upande wangu leo mswada huu tuupitishe asubuhi ya leo tuumalize tuupigie kura, kwa sababu mswada huu wengi kama unavyoona wameunga mkono na marekebisho tayari yameshaletwa, hivyo iliyobakia sasa ni kuupitisha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nikushukuru kwa kunipa nafasi yakuweza kuchangia mswada huu niseme ahsante sana, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said. Mchangiaji anayefata sasa hivi ni Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na baada ya hapo atakuja Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini na ajitayarishe Mhe. Suleiman Sarahani Said.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia japo kidogo. Mhe. Naibu Spika, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwakutujaalia mchana huu tukaweza kuwepo katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kuchukua fursa hii kuona umuhimu wa kuja na Sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi, sheria ambayo itakidhi mapungufu yote yaliyopo katika utekelezaji wa sheria ya mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia katika vifungu viwili kifungu cha 9 na 12. Nitaanza na kifungu cha 9, ambacho kinazungumza muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hichi kimetaja muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu. Hata hivyo, ukiangalia kwa undani wa mswada huu hakuna sehemu yoyote iliyoonesha muda wa utumishi wa Makadhi wengine na utaratibu wa kuondolewa kwao. Kwa mfano, Kadhi Mkuu au Kadhi wa Wilaya na wote Makadhi walotajwa na mswada huu, pale ambapo watakapofanya kosa je, utaratibu upi utatumika kumuondoa katika nafasi yake hiyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuondoka katika kifungu hicho cha 9. Sasa niende kifungu cha 12, ambacho kinazungumza Mrajis, Mahakama na Kadhi. Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi pia kimeeleza uwepo wa Mrajis, Mahakama ya Kadhi, aidha ikitizama kifungu hichi zaidi kimemuangalia Mrajis pamoja na uwazishaji wa ofisi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kifungu hichi naomba nipendekeze kuwepo kwa kifungu chengine kitakachowazungumzia uwepo wa watendaji wasiokuwa Makadhi, kwa mfano, karani, mfagiaji na kadhalika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wakati ukiangalia mswada mzima hakuna kifungu kinachozungumzia suala hilo. hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba atakapokuja Mhe. Waziri kwanza naomba azingatie vifungu hivyo nilivyovichangia, kwa umuhimu zaidi, ili kuweza vizuri mswada wetu.

Lakini mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nilisema nitachangia vifungu viwili. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kujibu hoja zangu azingatie kuboresha mswada huu, na kuleta utekelezaji bora na naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, UWAWAZA oye.

Waheshimiwa Wajumbe: Oye. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Sasa anafuata Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini baadaye atafuata Mhe. Suleiman Sarahani Saidi na ajitayarishe Mhe. Tatu Mohamed Ussi.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia wasaa huu wa kuchangia mswada huu muhimu sana katika nchi yetu ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi na kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi ya kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo. Naomba niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na pia kwa kweli ulokuwa *strait forward* hasa katika masuala muhimu sana katika jamii yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Mhe. Machano Othman Said, kwa kazi nzuri aliofanya yeye pamoja na timu yake na kutualika Wenyeviti wa Kamati kuja na sisi kutoa maoni yetu kusaidia kazi ya pamoja.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli usio fichika kwamba masuala ya Kadhi hapa nchini kwetu yamekuwa makubwa na ukifika ile Ofisi ya Kadhi pale Mwanakwerekwe siku zote pamejaa, na kama walivyosema wenzangu masuala ya ndoa na talaka yamekuwa mengi. Kwa hiyo, hii sheria imekuja kwa wakati muafaka na naamini itasaidia sana.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika naomba sana Mhe. Waziri Mahakama ya Kadhi au Ofisi ya Kadhi kwa ujumla baada ya kupita warka huu, watoe darasa maalum katika vyombo vyetu, kwa sababu hii sheria imeandikika vizuri sana Mhe. Naibu Spika. Hata hivyo, kuna mambo mengine naamini watu hawayajui kama haya kumbe Ofisi hii ya Mahakama ya Kadhi inayafanya, na nitaomba niyakariri kwa mujibu wa sheria yetu Mhe. Naibu Spika, kifungu cha tano.

Kifungu cha tano mtaniwiya radhi kidogo Mhe. Naibu Spika, lakini kwa umuhimu wake, naomba niyasome:

"Mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadaiwa ni Waislamu kuhusiana na mambo yafuatayo:"

(a) Ndoa, Talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa. Hapo mengi yanakwenda hapo, lakini
(b) Ustawi wa familia.

Mhe. Omar Seif Abeid alizungumza vizuri sana. Nafikiri hapa *role* kubwa ya Mahakama ya Kadhi suala la suluhu au upatanishi kama walivyozungumza wenzangu ni suala muhimu sana, mambo mengi sana pengine mambo madogo madogo tu kila mmoja anakamata mpini hasira ndoa inavunjika. Kwa hiyo, mambo madogo yanataka *councelling* tu basi.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri wengi wetu tunafungua televisheni za nje, kwa mfano *CNN* pale au vipindi vyengine, kuna yule mama *Black American*, *Opra* familia zinakwenda pale, wanakwenda na matatizo yao anawazungumza familia muwe hivi na vile, basi kila mmoja anaregeza msimamo mambo yanakwenda vizuri.

Sasa, naomba kutoa ushauri Mhe. Naibu Spika, kifungu cha (b) kimesema ustawi wa familia, hivyo naomba tuongeze neno moja upatanishi au suluhu na ustawi wa familia. Tena hii ninaomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa kweli najua ukizungumza Mahakama watu wanaona ah! Huko bwana kwenda kugombana, vipi basi wengi wanaona, yaani huko mahakamani tugombane, anachukua uamuzi tu, sikutani, talaka kwa heri.
Lakini kama kuna watu au kitengo cha kushughulikia upatanishi, suluhu yote kuweka ule ustawi wa familia nzuri nafikiri hii itakuwa *role* kubwa sana. Kwa maana hiyo, nadhani hii Mhe. Naibu Spika, kwa kweli taaluma itolewe kupitia vipindi vingi sana, hata hizi Mahakama zetu za Wilaya vingewekwa vitengo maalum vya ushauri, na suala hili Mhe. Naibu Spika ni kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha (c) matunzo na malezi ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa, wakati familia iko pamoja *is ok*, lakini wakeshakuachana mizozo inaanza. Sasa yale ninayosema ile *councelling* tunamwachia mama na watoto wadogo wanapata tabu, lakini akifahamishwa baba, bwana *role* yako moja, mbili, tatu, watoto wadogo hawa, ndio yale niliyorudia mambo ya *councelling*.

Vile vile, kifungu cha (d) huduma na misaada, kumbe ofisi hii inatoa huduma na misaada. Halafu *role* nyengine kubwa (e) Wakfu au Amana za Kidini hiba na mirathi, hapa napo pana tatizo Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, kama nilivyosema

haya yote yanatolewa ufafanuzi si watu wote wanayoyajua vizuri (a), (b), (c), (d) zake. Hivyo, naomba kutoa ushauri sana Mhe. Naibu Spika, hili litolewe elimu kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha (f) Wasia, yaani wengi tunangojea familia zetu mpaka mmoja pengine katangulia mbele ya haki tena mizozo inaanza. Lakini wasia utolewe mapema nyote mhai na tutaepuka mambo mengi sana. Mhe. Naibu Spika, nilihisi hili nichukuwe dakika kidogo kuzidi kutilia mkazo umuhimu wa ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba nimejaribu kusoma sijui, lakini nahisi ilivyokuwa tunaipitia tena hii Sheria ya Mahakama ya Kadhi, sikuona stahiki za Kadhi Mkuu wala Naibu Kadhi Mkuu kutajwa nahisi ni vyema kama zipo *somewhere* huko vizuri, lakini katika sheria hii ni vyema.

Kwa kweli, nakumbuka kidogo Mufti alikuwa yeye zake zinafahamika wazi, lakini Kadhi Mkuu na Naibu kulikuwa na *omission* huko nyuma, sasa sijui kama sasa mambo yamekaa sawa *well and good*, lakini kama hayakukaa sawa nahisi nazo zingetiwa wakati wa kazini na baada ya kustaafu yeye stahiki zake zipi ziwe wazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu wetu kiutawala wetu baada ya kutoka juu huko kwenye Mahakama ya Kadhi kuna Wilaya hapa umezungumza Mahakama ya Kadhi ya Wilaya. Naomba kuuliza tu je, Mkoa kwa nini tumeruka Mkoa au ngazi hiyo sio muhimu, lakini nataka kufahamishwa tu sifahamu huu utaratibu ulivyo vizuri. Kwa hivyo, ingekuwa utaratibu wetu Wilaya, Mkoa, Rufaa sasa haimo hii, hivyo nataka kufahamu tu.

Mhe. Naibu Spika, chengine kilichopendeza sana katika sheria hii ni kule kuundwa muundo mpya utakaoongoza katika suala zima la rufaa. Kwa kweli, wengi kama nilivyosema wanaona mambo ya Mahakama kidogo mazito yanachukua muda, na wengine ah! Uchatolewa uamuzi hendi, basi ushatolewa uamuzi hakuridhika anakwambia ah! Namuachia Mwenyezi Mungu kwa kuwa lishatokea namuachia Mwenyezi Mungu.

Lakini sasa kumbe kuna utaratibu wa rufaa, huu utaratibu wa rufaa nao tena unaambiwa utasikilizwa na Jaji wa Mahakama Kuu, ambaye ni lazima awe ni Muislamu, ambalo ni jambo zuri sana. Hii pia ningeshauri sana hii *element* ya kukata rufaa watu wengi waelimishwe. Kwa kweli, watu wengi wanakwambia hivyo ah! Bwana najua wameshamaliza huko namuachia Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kufurahisha nasema kwamba huyo Jaji wa Mahakama Kuu ni lazima awe mwanamme na awe atakayekaa na Maulamaa wanne watakaoteuliwa na Mrajisi kwa mapendekezo kutoka katika Baraza la Ulamaa.

Mimi si *question* hapa kwa sababu mimi ni mwanamme labda mwanamke atajiuliza yeye kwa nini imetajwa *specifically* imetajwa kwamba awe Jaji mwanamme huyo wa Mahakama Kuu. Lakini kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu naomba Mhe. Waziri hili aliweke wazi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi sheria imeandikika vizuri na kwa kweli wote katika sisi hakuna hata mmoja anayepinga isipokuwa tunakazia tu hapa na pale. Lakini nasisitiza sana suala la elimu Mhe. Naibu Spika, kwa kweli litatusaidia sana kupatanisha ndoa zetu.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Mchangiaji wetu anayefuata sasa hivi ni Mhe. Suleiman Sarahan Said, muda ukitosha atachangia Mhe. Tatu Mohammed Ussi na kama ukitosha tena atachangia Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, niwashukuru wananchi wote wanaojishughulisha na kazi hasa kule Pemba kuchuma karafuu katika zao la taifa la uti wa mgongo wa taifa letu. Waendelee kuzichuma karafuu vizuri na kuziuza katika *ZSTC*. Kwa hivyo, nawapongeza sana wachumaji wa karafuu waliokuwepo kule Pemba, wajitahidi wazichume karafuu zote na wasiziuze Kenya au mahali pengine popote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kufanya ziara mbali mbali katika Wilaya zake zote za Unguja na Pemba, na kuweza kutatua kero mbali mbali zinazowakabili wananchi pamoja na kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda nichangie kidogo katika huu mswada wetu, pia nikitilia maanani kwanza kwa walio uratibu huu mswada. Niwapongeze sana kwa hatua ambazo walizozifikia.

Mhe. Naibu Spika, katika baadhi ya maelekezo nitauchangia huu mswada kwa kifungu kidogo baadaye nitauchangia kwa jumla, ili kuboresha matukio halisi yaliyojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, tuna maneno ambayo tunakuwa tunayatumia sana katika mambo mbali mbali, lakini inawezekana katika utaalamu wetu wa kuyafahamu ikawa kidogo kwa wengi hatuyajui. Kwa mfano, tukisema kama neno ulamaa, tunalijua utasikia tunaita ulamaa au maulamaa. Lakini nini kiini, nini sababu na nini ule uhalisia wake wa ulamaa awe amekwenda Makka mara ngapi, au awe amefanya kitu gani mpaka atimie kuwa yeye ni ulamaa awe amefika vipi, maana tusimtaje mtu ulamaa.

Pia, tujue nini maana ya Kadhi, nini Kadhi hasa, awe amefika kiwango gani cha elimu ndiyo awe Kadhi. Tunataja tu Kadhi, Shekhe, imamu, lakini viwango gani ambavyo tunavitumia au maana halisi ya hili neno katika mambo ya ulamaa mambo ya Kadhi ni nini, ili tuweze kujua kwa mswada ambao unatekelezeka na uliokuwa unaletwa tujue kwamba Kadhi anaweza kuwa mwanamke au mwanamme, ulamaa anaweza kuwa mwanamke au mwanamme. Hivyo, sababu zinakuwa zipi za kuwa huyu mtu awe anaweza kuwa na hivi vigezo. Isiwe kwamba tunaweza kumzuia mtu kupata haki yake kutokana na kuelewa nini hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, naomba hawa waliotunga hili jalada maalum waweze kutupa maelekezo zaidi, ili kujua nini maana ya baadhi ya vitu humu walivyovitumia ili tuweze kwenda mbali.

Mhe. Naibu Spika, naona katika jumla ya mambo haya ya Sheria hizi za Mahakama ya Kadhi tutizame kwanza chanzo cha mpaka kufunguliwa kwa Mahakama ya Kadhi nini chanzo cha Mahakama ya Kadhi, mpaka tukafika hapa tulipo na tukaboresha baadhi ya mambo mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia kidogo kuangalia kwa wenzetu inawezekana kama Msumbiji na maeneo mengine ukitaka kufunga ndoa kuna mikataba maalum mnayofunga mpaka ya mali na ikiwa utamuacha inawezekana utamlipa kitu gani. Hali hii kutokana na kupunguza joto la watu wambao wanaweza wakawa hitilafu zao ndogo, lakini kwa sababu kama tulivyozungumza maana ya ujeuri na kitu chengine kikaweza kuchangia mambo yasiyokuwa na maana.

Kwa hivyo, naomba kwamba mikataba yetu ile ya kufunga ndoa, ambayo ni cheti cha ndoa hebu kiboreshwe kidogo, ili kiweze kuwekwa vizuri ili tusiandikie kuowana tu, lakini na kuachana. Sasa unakuta watu wanakusanyana wakati

wakuoana, lakini wakati wa kuachana humpati mtu hata mmoja hata ukimwita haji, kwa sababu hapana mkataba wowote ulioufunga na hapana kinachoendelea. *(Makofi)*

Ninachosema Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa linakuja kama nilivyosoma katika kifungu chetu hapa chengine nafikiri kifungu kinachosema mambo ya ndoa na mambo ya watoto na talaka na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika, tatizo ni haki, mtu akeshakukosa haki yake na niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda Idara maalum au Wizara maalum Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na kwa kuwatafutia haki zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama watu wanavyozungumza ukisema kwamba maji ukiyaziba, basi yatatafuta njia ya kutokea. Kwa hivyo, wanawake wamefika pahala ilikuwa haki zao hawazipati na wakaamua kuingia huko huko kwa wanaume sasa. Kwa kweli, hili ni tatizo kubwa tunawapa kazi mpaka zilizokuwa siyo zao kutokana na matatizo yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tatizo jengine lililojitokeza Mashekhe wetu wakati wa kutuozesha ndoa wanatumia Lugha ya Kiarabu sana. Sasa, yule unayemwambia maneno yale hajui, kwanini ukiozesha humuozeshi kwa Lugha ya Kiswahili anayoifahamu ukamwambia kwamba munaoana kwa wema na ikitokea kuachana basi muachake kwa wema. Lakini Mashekh wanatumia Lugha ya Kiarabu ambacho mume au bwana harusi hakijui akiondoka pale anakunja goti anaondoka. *(Makofi)*

Hivi ni vitu ambavyo vidogo vidogo, lakini vinaleta mantiki kwamba mtu siku ambayo anataka kumuacha mwanamke anakumbuka kwamba niliambiwa neno fulani, nilisema maneno fulani, hayatumiki. Kwa hivyo, kuna mambo ambayo kidogo yanatakiwa yatumike kimpangilio.

Mhe. Naibu Spika, kwa kwenda mbio kidogo nazungumzia suala la *Qur-an*. Mhe. Naibu Spika, *Qur-an* imemaliza kila jambo katika hatua zetu. Kwa kweli, mpaka hizi ndege tunazopanda na kuruka zimo ndani ya *Qur-an* tatizo hatujui tu. Kwa kweli, hatujui kuisoma wala kuitafsiri vizuri *Qur-an*, ndio maana tumefika hapa, haiwi *Qur-an* inaunda ndege na vitu vyengine mbali mbali ishinde kujua haki za ndoa na mambo yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nadhani tatizo na hawa Mashekhe wetu wamepoteza muelekeo, Mashakhe wamejiingiza kwenye siasa, na mambo kama hayo. Kwa kweli, *Qur-an* sasa hivi wanasomewa maiti, hawasomewi tena watu wazima wenye akili zao

wakafahamu, isipokuwa wanasomewa maiti ambao wamekufa zinakwenda kuwafaa nini kule. *Qur-an* imeletwa kwa watu kuja kuamua kesi, na mambo mengine mbali mbali yaliopo hapa, lakini *Qur-an* sasa hivi wanaipeleka kwa maiti kwenye mava unakwenda kuwasomea waliokwisha kufa.

Mhe. Naibu Spika, *Qur-an* itumike hivi sasa kwa sisi tuliomo humu, na ndiyo maana ya kuletewa au kushushwa. Kwa hivyo, ni lazima tuitumie, Mashekhe wetu na wao wasahau wazinduliwe jamani, wale wasomewe, kwa sababu wanakwenda kwa Mwenyezi Mungu wameshafika mbele ya haki.

Lakini na sisi tusomewe tuliyokuwepo huko tusifike huko tukenda kuharibu, sisi ndiyo tunaokaa tumeshaharibu halafu unasomewa huko, ndio maana watu wanasema kwamba unakwenda kufunga banda na farasi keshatoka. Wewe unakwenda kusomewa kule wakati madhambi waliyokwisha kufanya madhamba hapa. Waheshimiwa Wajumbe, wameshafanya madhambi sana halafu kule, sasa ni lazima tusomewe hapa, ili tusifanye madhambi Mhe. Naibu Spika. Siombi radhi, kwani nimemtaja mtu. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumza baadhi ya mambo ni lazima yawe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni tatizo la vyeo. Vyeo ni chakula, cheo ni kila kitu, tunataka vyeo vingi mazogo mengi, lakini maudhui na jambo maalum unalokwenda kulifanya huna utaalamu nalo. Hili ndilo limetufikisha kwenye Mahakama za Kadhi.

Kwa kweli, kule Shekhe utamkuta na koti, lakini hajui chochote pengine na wengine wanajua wanafanya makusudi, kwa sababu alilopelekewa pale hakufahamu nini maana yake. Pengine pale anaamua kesi lakini anamtaka yule mwanamke, mashekhe wengine ndiyo matatizo yao. Sasa inakuwa ile kesi haishi anaona mtu anaonewa mwisho anaacha, anapata matatizo.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza kwamba hata hawa Majiji wa Mahakama sijui kama ndiyo watakuwa maulamaa au Makadhi ama nani. Nafikiri ni vyema kwanza watizamwe na uwadilifu wao, tusimchague mtu kwa elimu tu na uwadilifu anao, hicho ndicho kitu muhimu kuliko hata hiyo elimu, na hayo ndio mambo yanayoweza kuangalia hasa tatizo

Mhe. Naibu Spika, hayo ni hata katika malezi yetu, kwa kweli hivi sasa ndoa haziwezi kuishi, kwa sababu ndoa anayekwenda kuposa mwanamke, mambo ya kwenda kuposa baba hayapo tena anaposa mama au dada. Mambo haya ni mazito, kwa sababu siku zote mwanamke wakati wa kwenda kumposa au dada akiwa

anamtaka yule mwanamke anamtaka. Lakini siku kaka akimkatia kitambaa kizuri na viatu vizuri hakumkatia ndugu yake, basi hampendi tena yule na atatoka ndani ya nyumba kutaka asitake. Mambo yanaanza hapo sasa, na keshapata watoto wawili hajui aelekee wapi na anataka kumposea mwengine sasa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lazima mambo kama haya tuyatizame sana, kwa sababu ya maamuzi ya tatizo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, tulitizame tatizo tuliloundiwa Mahakama ya Kadhi ni ndoa, talaka, haki za mtu, haki za watoto, urithi na baadhi ya mambo mengine. Yapo matatizo makubwa sana yapo na tunayaanzishwa wazee, unafikiri kwamba wale watu *Qur-an* hawaijui wanakwenda na matakwa yao. Sasa wewe mtu wa saba yanakuhusu nini mtu kafa anawatoto wake ana kila kitu, unazuia cha kwake, ya nini lakini pia akenda huko kwenye hiyo haki haipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba hawa waliofanya hiki kitu wamefanya kitu cha kuboresha, lakini kama utekelezaji bado utakuwa ni ule ule, basi sijaona kwamba tatizo linakuwaje. Kutokana na hali hiyo, naomba kama walivyosema wenzangu uwadilifu ni kitu cha maana sana katika mambo yote haya. Lakini pia sheria zitumike na zichukue mkondo wake. Tatizo sheria zipo mbili kuna Sheria ya Kiislamu kuna Sheria ya Kidunia, kila mtu anapita mlango wake. Hapa ni lazima hivi vyombo viwili vikae katika utaratibu mwanamme huku akenda anadai haki, mtoto akija huku anadai haki na huku akija Uislamu unasema hivi, hapa tunakinzana, wameshasema wenzangu mengi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana katika masuala haya kama tumeamua kwenda kidini, basi twende kidini pale kwenye *point*, tuwache mambo ya kidunia, tumpe nguvu mmoja kati ya hawa, tumpe nguvu ili asimame na rungu la kuweza kubagua. Lakini tukiwapa maelezo ya watu wawili akishinda kesi huku anakwenda upande huo. Haya yatakuwa hayeshi na ni tatizo kweli kweli.

Mhe. Naibu Spika, nawaonea huruma sana wanawake wanaoachwa na watoto. Tunao hapa baba anatamba ana mke mwengine na gari mpya ana watoto watano wapo mitaani huko hawaulizi, isipokuwa mama yule anafanya vitu vyake, lakini siku ya kuja kuwa yule mtoto ni Naibu Spika, hee! Anajikaza koti yeye, anakuwa tena mwanangu yule, anakuwa ni kitu gani na siku nyengine kama kuna ndoa anataka kuozesha yeye. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa hebu tumlinde na huyu mama yule baba asiguse hata kama sheria ipo. Sasa hata tuangalie siku atakapokuwa mkubwa tu atakwenda

kusema mwanangu si mwanangu, lakini huku nyuma Mhe. Naibu Spika mlimwandikia angalau ripoti.

Kwa hivyo, kuwe na vitu Mhe. Naibu Spika katika hao wenzetu walioweka hii mikataba ya kumlinda mwanamke. Vile vile, Mhe. Naibu Spika kwa kweli kama mwanamke hatukuweza kumsaidia, basi bado itakuwa kazi ni bure tunayoifanya tutaweka sheria mpaka nyengine itakuwa mabuku hayatoshi, lakini kama bado hakujawekwa sheria maalum ni bure.

Mhe. Naibu Spika, mimi kama mwanamme ninayefahamu nini maana ya kuoa. Mimi nina mke mmoja na watoto na wala sina mke mwengine, lakini na nyinyi Waheshimiwa Wanawake kama mnakubali dini basi mkubali wanawake wengine waolewe, akianza kuoa mke mwengine na nyinyi mnaanza kuona kosa. Hivyo, mukubali kama sheria umeikubali kama wewe ni Muislamu, kama mume bado anao uwezo anataka mke muacheni aoe tena kamchagulie mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi mke wangu nimepa uhuru nimemwambia siku utakayotaka kuja kwamba niongeze mke niambie, yaani namuweka yeye anichagulie mke mzuri anayemtaka yeye. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Suleiman Sarahan Said nakushukuru sana. Naona wanaume wengi wamepiga makofi na wanawake wamenyamaza kimya. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Tatu Mohammed Ussi na baadaye atafuata Mhe. Shehe Hamad Matar.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu anaohusiana na Mahakama ya Kadhi kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu moja kwa moja nitanza na sehemu ya kwanza kwenye utangulizi kwenye sehemu ya ufafanuzi kifungu cha 2. Katika sheria hii imesema "isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo" Kadhi maana yake ni Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Rufaa na Kadhi wa Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza kwanza nitaanza hapa na Kadhi wa Wilaya. Tumeona Mswada huu umelenga kwenye Mahakama ya Kadhi zaidi, kwa sababu Mahakama ya Kadhi ina mambo mengi ambayo inashughulikia hususan mambo ya ndoa na talaka. Tukiangalia Mhe. Naibu Spika, ndoa zinapokwenda pale zinahusu wanawake na wanaume, kwa sababu nyumba ikishakuchafuka tena ndiyo mambo yanakuwa hayo ya kukimbiliwa kwenye Mahakama ya Kadhi.

Mhe. Naibu Spika, hapa kwenye Kadhi wa Wilaya. Tukiangalia Mahakama zetu nyingi za Unguja na Pemba Makadhi takriban wote ni wanaume. Sasa kama Kadhi mwanamme mimi ni mwanamke nimekwenda pale na kesi yangu sifikirii kama mimi nitaweza kuyasema yale yote ninayofanyiwa na mwanamme yule, ili na mimi niweze kupata haki yangu sawa sawa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi kwa muono wangu na mapandekezo yangu naona, pamoja na kuwa Sheria yetu ya Dini ya Kiislamu pengine haituruhusu kuwa kuna Kadhi mwanamke lakini wale wasaidizi wake, wale maulamaa wanne waliotajwa, basi hapa napandekeza Mhe. Naibu Spika miongoni mwa maulamaa hao basi angalau na wanawake wawemo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napendekeza hili kwa sababu, kuna baadhi ya mambo ninapokwenda Mahakamani pale siwezi kukaa wanaume nikawaeleza wote kwa pamoja, isipokuwa hapa napandekeza kama si hivyo baada ya Kadhi pale na Msaidizi wa Kadhi awe mwanamke. Hii itatusaidia wanawake kupata haki zetu vilivyo. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye ukurasa wa 5 wa mswaada ule ambao umefanyiwa marekebisho na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kifungu cha 5 kilichofanyiwa marekebisho ukurusa wa 127. Tumeona pale wenzangu wamelizungumzia sana, tumeona kuna ndoa, talaka na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kila siku mitaani tunaona ndoa zinafungwa kila siku tuna maharusi, lakini na ukipita kwenye Mahakama ya Kadhi kila siku tunakuta kesi za ndoa na talaka watu wanadai talaka.

Mhe. Naibu Spika, hili linakuja na nini linakuja kutokana na ukosefu wa elimu wale wana ndoa kupewa elimu kabla ya kufunga ndoa zao. Mhe. Naibu Spika, naomba wale Makadhi wanaoshughulikia hili, lazima kwanza tuwape wana ndoa elimu kabla ya kufunga ndoa zao. Kwa kweli, tuwape elimu kwa sababu tumekuwa tukishuhudia mtu anaolewa hatimizi miezi miwili wala mitatu anaachwa, na

pengine kama katimiza mwaka au miaka miwili pengine keshapata mtoto anaachwa mtu yule na mtoto anahangaika naye mitaani. *(Makofi)*

Lakini jengine tukija kwenye matunzo na malezi ya watoto. Mhe. Naibu Spika, malezi na matunzo ya watoto hayaji bila ya mama na baba kuwa pamoja, tunashuhudia mitaani watoto wanarandaranda na kuhangaika na pengine wengine wanakosa kusoma kutokana na mama na baba kuwachana. Hivyo ni vyema, ili watoto tuwatunze basi pawekwe sheria maalum itakayofanya mama na baba wakiachana, basi wale watoto wapate matunzo kama ilivyokuwa mama na baba hawajaachana.

Sasa hili linakuja vipi Mhe. Naibu Spika, mutakwenda Mahakamani pengine baba atawekea sheria amsaidie yule mama. Lakini matokeo yake kwa sababu hakuna kifungu kilicho mfanya yule wala hakuna sheria kaambiwa tu pale na Kadhi, basi ataitikia pale Mahakamani kama watoto atawashughulikia, lakini hatimaye anamuacha mama yule anahangaika na watoto peke yake.

Kwa hivyo, hapa naomba tuwekewe sheria ambayo itamfanya baba yule akimuacha yule mama, basi ni vipi mtoto yule atapata matunzo kutoka kwa baba yake.

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye kifungu (f) ule ule ukurusa 126 mgawanyo wa mali ya wanandoa, ambapo kuna uchangiaji halisi.

Mhe. Naibu Spika, mgawanyo wa mali, kwanza niipongeze Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa kuliona hili na kuliweka kwenye sheria hii. Mhe. Naibu Spika, napendekeza na hili liweko kwenye sheria, kwa sababu tumekuwa tunaolewa sisi wanawake na wanaume tunawakuta wenzetu hawana kitu pengine mwanamme hana alichonacho hana nyumba, lakini ukakubali umasikini wenu mkaa pamoja.

Sasa baadaye Mwenyezi Mungu akawajaalia pengine mkajenga nyumba, yeye akitoa saruji wewe unatoa kokoto, yeye akileta mchanga, wewe unapeleka maji ina maana jambo lile ni lenu pamoja. Lakini hatimaye bwana yule akishapata mwengine pengine huko akiona bora zaidi yule, anakuwacha anakwambia nenda zako kwenu na inakuwa wewe huna kitu pale. Mhe. Naibu Spika, inawezekana pengine mumechuma mali nyingi tu, lakini bwana yule anakuwacha wewe unakwenda zako masikini wa Mungu unakwenda kuhangainga tena na maisha mengine.

Vile vile, na hili naomba Mhe. Waziri alione, tuwekewe sheria kile ambacho bwana nimemkuta nacho kile hakihusu, lakini kiangaliwe kile ambacho tumekichuma pamoja, sasa kile tulichokichuma pamoja bwana yule akiniacha tugawane sio achukuwe yeye ale na mwengine mimi niendelee kuteseka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa sababu mengi wenzangu wameshayazungumza niliona niseme na hayo kidogo, ili Mhe. Waziri alione kwa lengo la wanawake na sisi tupate haki zetu, kwa sababu tumekuwa tukihangaika siku nyingi. Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Tatu Mohammed Ussi ahsante sana kwa mchango wako nimekaa hapa nasema tunao wanawake majasiri tunao humu ndani ya Baraza la Wawakilishi wewe ni mmoja wao, kwa sababu kuna maneno mengine wengine wangeogopa kuyazungumza umeyazungumza hongera sana Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Sasa nimpishe nafikiri Mhe. Shehe Hamad Mattar dakika kumi zilizobakia nafikiri utaweza kuzitumia vizuri kumaliza mchango wako ahsante karibu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na nitakwenda moja kwa moja katika mswada kwenye vifungu. Kwanza niwapongeze kwa kuleta mswada huu muhimu katika nchi yetu ambao kuwa utaweze kuweka sawa matatizo mbali mbali yanayojitokeza, hasa mambo ya haki na ndoa na talaka zinatuingia katika familia zetu.

Lakini nitakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 127 katika kifungu Nam. 6 kinasema kwamba kuna Sheria ya Ushahidi. Sheria ya Ushahidi imeelezwa katika Sheria Kanuni ya Ushahidi zitakazotumika katika Mahakama ya Kadhi zitakuwa ni zile zinazotumika katika Sheria za Kiislamu. Swali liko hapa, Makadhi wetu je wanatumia Sheria za Kiislamu ipasavyo, kwa sababu leo zinakwenda kesi Mahakani ya watu kuchukuliana wake leo mtu anakwambia mtu fulani mke wangu anamchukuwa, na huyu anasema anachukuliwa mume wake.

Je, sheria ipi inayochughulisha kwamba kweli kachukuliwa huyu mume wake au mke wake au sheria gani inayoeleza hapo mtu afike kupewa haki mmoja wapo ilo najua niangalie vipi hiyo Sheria ya Kiislamu.

Sheria ya Kiislamu inavyotaka ushahidi mambo mengine mpaka wapatikane watu wanne watimiye, je hapa itawezeka kutumia Sheria za Kiislamu hilo moja. *(Makofi)*

Ukurasa wa 28 kifungu Nam. 9. Mhe. Naibu Spika, naomba kwamba katika hili neno liongezwe katika sentensi ya mwanzo muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuongeza katika sentensi iliyotajwa hapa kwamba inapotajwa muda huu, isitoshe tu kwamba atakapo staafu au kuwacha kazi au kustaafu kwa lazima bali uongezwe kwamba atakapojiuzulu au atakapofariki, pia ni sehemu ya muda wa utumishi akifariki au atakapo jiuzulu.

Vile vile, niende katika ukurasa wa 128 kifungu 10. Mhe. Naibu Spika, nashauri sana kuonesha kwamba zitajwe Kadhi wa Rufaa hapa kifungu cha 10 wametajwa Makadhi wa Rufaa, lakini naomba watajwe kazi zao na muda wa kustaafu pia haukutajwa hapa, hivyo nashauri sana utajwe.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 11 hali kadhalika nao pia vile vile vitajwe kazi zao na muda wa utumishi wao hawa Kadhi wa Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea moja kwa moja hadi ukurusa huo 129 kifungu Nam. 13(1)(a) kuna maneno hapa, kutekeleza baadhi ya uwezo na wajibu wa Kadhi. Kwa hivyo, nashauri hapa utajwe huo uwezo wenyewe upi usitajwe tu, baadhi ya uwezo utajwe kama upi huo uwezo wenyewe katika sheria, hii ni sheria tunaiweka iwe wazi.

Lakini, tuende ukurasa wa 129 mpaka 130 kifungu Nam. 7 inaposema kwamba, naomba kunukuu.

> "ombi litafanyiwa chini kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki itawasilishwa ndani ya siku thelathini"

Mhe. Naibu Spika, naomba iongozwe hapa kwamba iwasilishwe kwa maandishi, isiwasilishwe tu kwa mdomo kwa sababu kiandikwacho hupakia na kisemwacho huruka. Kwa hivyo, naomba liongezwe neno kwa maandishi hapa baina ya neno litawasilishwa ndani kwa hivyo hapa kwa maandishi ushauri wangu nashauri hivyo.

Vile vile, niende katika kifungu cha 26 ukurasa wa 133 kinasema kwamba, naomba kunukuu.

> "muda wa usuluhishi hautozidi siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kikao cha kwanza cha upatanishi na kuhitajika muda wa ziada wa muda huo ni lazima ukubaliwe na pande zinazohusika na usuluhishi".

Mhe. Naibu Spika, naomba liongezwe neno ila asizidi mwezi mmoja yaongezwe maneno hayo napendekeza hivyo ila yasizidi mwezi mmoja katika huo muda anaopewa.

Nikienda moja kwa moja kifungu Nam. 27 kuondoa mgogoro katika usuluhishi kifungu namba 27(2) kinasema upande wowote usioridhika na amri iliyotolewa. Mhe. Naibu Spika, hapa naomba litumike neno badala ya amri litumike neno ushauri au uwamuzi badala ya kutumika neno amri nashauri sana hivyo.

Niende moja kwa moja kifungu 32 katika kukubaliwa tunasema 32(1) kukubaliwa kwa Wakili na Vakili, hapa hazikutajwa wamesema Wakili kifungu Nam. 32(2) Wakili au Vakili atayeruhusiwa kusimamia kesi katika Mahakama ya Kadhi atatakiwa awe na elimu na uzoefu wa Sheria ya Kiislamu.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu hapa naomba kwamba zitajwe zile sifa kama zilivyotajwa Makadhi wa Wilaya na Makadhi Wakuu na hapa zitajwe sifa.

Mwisho, nawashukuru sana kwa uwasilishajai wao na Kamati nao wamechambua vizuri sana niwapongeze sana. Kwa hivyo, naunga mkono hoja mia juu ya mia baada ya marekebisho hayo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wajumbe tumebakisha wachangiaji kama watano ambao wataanza kuchangia jioni tutakaporudi, nao ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Mgeni Hassan Juma. *(Makofi)*

Vile vile tutakuwa na Mawaziri wawili ambao watachangia naye ni Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na vile vile namuona na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kanambia atachangia, kwa sababu haya ambayo yanazungumzwa yanawahusu wananchi, ambao wako chini ya wizara yake, hivyo na yeye ameomba kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kusema hayo naahirisha mpaka jioni saa 11:00.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

(Mhe. Mwenyekiti Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na michangio anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kufika hapa Laasiri hii tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, na pia vile vile shukurani za pekee ziende kwa Mhe. Waziri pamoja na kamati yake waliokaa pamoja na kuujadili mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja nitakwenda katika ukurasa wa 127, sehemu ya 5 (a). Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wengi ambao wamechangia kipengele hiki cha ndoa na talaka, tumeona na sisi pia tuendelee kuichangia ndoa hii na talaka.

Mhe. Mwenyekiti, ndoa na talaka kumekuwa na vijana wetu wa sasa hivi wanaifanya ndoa na talaka ni jambo la mchezo sana, na tukizingatia katika sheria zetu za dini ndoa ni jambo kubwa na talaka ni jambo kubwa sana na si jambo la kuleta mchezo. Lakini tumegundua kwamba kuna vijana wanaoa mke leo na kesho anamuacha tena bila ya tatizo lolote, tatizo dogo kwake yeye linakuwa ni kubwa, tumeona ni kwamba ni kutokuifahamu ile ndoa ni kitu gani. Kwa hivyo, tunaiomba Mahakama ya Kadhi iendelee kutoa taaluma kubwa juu ya vijana wetu wakati wanapotaka kuoa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika kipengele cha (c) matunzo na malezi ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa. Mhe. Mwenyekiti, wanawake tunapata tabu sana na tabu tunayoipata waume zetu wanaoa wake zaidi ya wanne, na wake hawa baadhi yao hawaleti mashirikiano. Anaoa mke leo kesho wewe ukishakubeba ujauzito yeye anakuona si mke tena anakwenda kutafuta mke mwengine, siku ya pili na yule na yeye akishapata ujauzito tayari anaendelea kutafuta mwengine yule siye tena, wakati huku mke wa kwanza ameshamuachia watoto watano, wa pili ameshamuachia watoto watatu yeye anaendela kuoa, na ukija kuiangalia nyumba juu maji yote ikinyesha mvua yamo ndani ya nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba Mahakama ya Kadhi iliangalie suala hili lakini pia na sisi wanawake tunaomba tunapokwenda Mahakamani tuangaliwe jinsi gani ya kusaidiwa kwa yule mwanamme yeyote atakayeoa wake zaidi ya wanne na ikawa hana matunzo ya watoto na mama.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele kidogo katika kipengele cha (e) Wakfu na Mali ya Amana za kidini. Mhe. Mwenyekiti, wazee wetu wa zamani waliposoma na ikawekwa hii Wakfu na

Mali ya Amana waliwekwa kwa maana ambayo inaheshimika kidini. Lakini tumeona kwamba sasa hivi vijana wetu hili neno la wakfu hawaliangalii upana wake. Mzee anakufa pengine anaacha shamba lake akasema hili naliacha wakfu kwa anayetaka yeyote basi ajenge, lakini inafika pahala wale watoto wake baadhi ya wengine wanasema kwamba shamba lile ligaiwe wao hawana habari ya wakfu.
Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba sana itolewe jitihada kubwa ya vijana wetu kupewa taaluma…

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tunaomba utulivu Barazani mazungumzo yanakuwa mengi na ukumbi wetu tunaujua kwamba una *echo,* kwa hivyo tumpe raha Mhe. Bahati ili kutoa maelezo yake yasikikane. Ahsante mheshimiwa endelea.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nitarudia tena kuhusu neno la wakfu naiomba Mahakama ya Kadhi itoe taaluma kwa vijana wetu juu ya neno wakfu. Ili neno hili la wakfu wajue upeo wake ambao uliwekwa na wazee wetu nyuma tulipotoka.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja Nam.6 sheria na kanuni za ushahidi zinazotumika katika Mahakama za Kadhi zitakuwa ni zile tu zinazotumika katika sheria ya Kiislamu. Mhe. Mwenyekiti, hapa na sisi wanawake tunaomba kwamba waekwe wanasheria wawili. Mwanasheria mwanamke na mwanasheria mwanamme ili yule Kadhi aliyepo pale wengine vile vipengele wanavikosea, lakini akiwepo mwanasheria mwanamke na mwanamme basi ataweza kuwasaidia wale wanawake kile kipengele ambacho kuwa kitamgusa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitoendelea sana kwa sababu wenzetu wameshatufilisi sana kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bahati sasa ni zamu ya Mhe. Hamza Hassan Juma lakini simuoni, kwa hivyo namwita Mhe. Salma Mussa Bilal aendelee kutoa mchango wake.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Laasiri hii ya leo kwa kunipa nguvu kuchangia angalau mawili katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, Mhe. Issa Haji Gavu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa niaba ya Mhe. Waziri wa wizara hii kwa kutuwasilishia mswada huu katika Baraza lako hili tukufu na leo tunauchangia.

Mhe. Mwenyekiti, sisemi kwamba umechelewa lakini pia nasema kwamba madhali umeletwa basi umekuja wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze na ukurasa wa 31 kifungu cha 17 ambacho kinasema rufaa katika Mahakama ya Kadhi ya Rufaa. Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi za Mahakama ya Kadhi zinaanzia Mahakama ya Kadhi halafu badala ya hapo zinakwenda katika Mahakama ya Kadhi ya Rufaa. Lakini inaposhindikana mwisho inapelekwa kwa mujibu wa mswada huu kwamba mwisho inakwenda katika Mahakama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi si mtaalamu sana wa sheria lakini nilikuwa naomba kutoa ushauri kidogo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba badala ya kesi kutoka Mahakama ya Rufaa na kutaka kupelekwa Mahakama Kuu ukizingatia kwamba Mahakama ya Kadhi ya Wilaya na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa zina wataalamu zaidi na wazuri wa kidini zaidi. Sisemi hiyo Mahakama Kuu hakuna lakini Mahakama Kuu, Hakimu wa Mahakama Kuu yeye anakuwa ni Hakimu wa kijumla jumla. Lakini hii ya Wilaya ya Kadhi na Rufaa inakuwa hizi ni *special* hasa kwa haya masuala ya Kiislamu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Mahakama ya Rufaa inaposhindikana basi hapo hapo Mahakama ya Rufaa liundwe hilo jopo la Kadhi Mkuu labda akiwemo Naibu Kadhi Mkuu na baadhi ya hao Maulamaa wakae hapo hapo katika Mahakama ya Rufaa. Lakini Katika hiyo *list* ya Maulamaa pia kuwe na uwiano wa wanawake na wanaume ukizingatia kwamba wenzangu walishatangulia kusema kwamba ili kunapotokea masuala ya wanawake ili wanawake tuweze kupata utetezi wa ndani bila ya usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba badala ya kuishia Mahakama Kuu basi iishie hapa katika Mahakama ya Rufaa kwa kuongezea hawa Maulamaa na Kadhi Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jengine nakwenda ukurasa wa 134, kifungu cha 27(3) kifungu ambacho kinachoelezea kwamba ada na gharama za usuluhishi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema baada ya kuridhika kwamba ada na gharama za usuluhishi zimelipwa kikamilifu, usuluhishi unaweza kutengua uamuzi wake wa awali na kuachana na usuluhishi na kwa ridhaa ya wadau wao wote wanaohusika atatoa taarifa ya kuendelea na wana usuluhishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilikuwa na ushauri kidogo, naomba hizi ada na gharama za usuluhishi naomba zisiwe kubwa zianishwe kiasi chake kwa sababu kuna wananchi wetu wengine wanakuwa uwezo wao ni mdogo hawamudu kulipa hizi gharama za ada za usuluhishi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba hizi ada za kipengele hiki ziwekwe ndogo ama ziondoshwe kabisa ili hao wananchi wetu ambao wanakuwa kipato chao ni kidogo na hawana uwezo na wao waweze kupata haki kupitia kipengele hiki cha kuondoa migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani nilikuomba dakika tano tu kwa sababu mengi yameshazungumzwa, lakini na mimi angalau niweze kuchangia kidogo. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono mswada huu nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa naomba nimwite Mhe. Said Soud Said kwa kutoa mchango wake.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nafasi ambayo kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Hii hoja kwa sababu imeandikwa kwa umakini kabisa kilichobakia ni kuwaongezea ili sheria katika nchi hii iweze kuwa na meno katika mazingira mazima ya Mahakama zetu za Kadhi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme endapo itafungika ndoa katika nchi yetu na bila ya kupima UKIMWI basi hilo ni kosa la jinai, lazima tukubali kufunga ndoa bila ya kupima UKIMWI ni kosa la jinai. Kwa hiyo, lazima watu kwanza wapime UKIMWI halafu baadae wafunge ndoa katika nchi yetu. Pia ni vyema tukaweka sheria madhubuti katika hii kuongeza vitu ambavyo vitasaidia ndoa ambazo ni za mkeka katika nchi yetu mara nyingi sana kuna ndoa za mkeka watu hukamatiana huko ukasikia muowe, muowe basi akaolewa mtoto siku 20 ameshatia gharama ukoo mzima umeingia gharama watu wamepika mapilau na mabiriani wamechinja mang'ombe lakini baada ya siku 20 ndoa hiyo imekatika.

Sasa lazima hapa paongezwe vifungu vya sheria kwa waume wa aina hiyo, kwamba endapo mtu atakuwa amefunga ndoa ya lazima ambayo si ile ya kisheria, yaani nakusudia amebaka au amechukua mtoto wa watu basi ni vizuri tukaongeza sheria kwamba ndoa hiyo haitovunjika baada ya miaka 7, ama aivunje Mwenyezi Mungu kwa kufa bibi au kufa bwana. Lakini ikiwa wako wawili pamoja kuwe na sheria ambayo itaongeza nguvu ili kuwasaidia Makadhi na migogoro inayopelekwa ambayo haina kichwa wala haina miguu. Kwa misingi hiyo ni kwamba ikiwa tutakuwa tumefanya hivyo basi hizi ndoa zitaweza kudumu, kwa sababu katika nchi yetu sasa hivi imekuwa talaka na ndoa kila siku zipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi tokea nimekuja hapa Unguja kukaa kila siku ya Ijumaa kuna harusi, yaani nataka niseme kwa uhakika hakuna Ijumaa ya Mfunguo sita wala ya mfunguo nane Ijumaa yoyote kuna harusi Unguja. Hii ni dalili ya kusema kwamba *Alhamdulillah* watu wanatekeleza wajibu wao wa kufunga ndoa, lakini ndoa lazima ziwe na mikakati ya kudumu sio za kwenda pale watu wakababaisha siku 20 au 30 watu wakaachana kwa nia tu ya kwamba hawawezi kuvumiliana. Uvumilivu lazima ujengwe katika misingi ya *traditional* zetu ambazo kama Wazanzibari tumekuwa na utamaduni wa miaka mingi, na haimaanishi kwamba sheria hizi za Kadhi ni sheria zitakazovunja misimamo ya Dini ya Kiislamu, hamna. Sisi kama Wazanzibari, sisi kama Waislamu tuna haki ya kutetea Mahakama za Kadhi ziheshimiwe na ziwepo katika utaratibu wa kusimamia Dini ya Kiislamu kama vile ilivyoagiza Kur-ani.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa na utaratibu wa ndoa zile ambazo zinazisimamiwa na wazazi wawili na hizo ndio ndoa ambazo upande wa kiukeni na upande wa kiumeni wanasimama katika mazingira ya kusimamia ndoa hiyo mpaka inafungika. Lakini pia kumekuwa na utaratibu ambao Mhe. Mwenyekiti, ndoa hizo huvurugika baada ya wazazi wenyewe kutokujielewa. Mtoto mwanamke anaondoka katika nyumba ya mume anakwenda kwa baba mzazi wake yeye au mama mzazi matokeo yake hapo sasa anakuwa amezuiwa na mazingira hayo ni mazingira ya kutokuwa na imani na Dini ya Kiislamu. Baba hana mamlaka ya kuzuia mke wa watu, wala mama hana mamlaka ya kuzuia mke wa watu, sheria haisemi hivyo.

Sasa basi kama kutakuwa kuna mivutano kati ya mke na mume ni vyema tukaongeza sheria kwamba mke huyo ataruhusiwa kwa kukaa siku tano kwao ili suluhisho lipatikane kwa misingi ya kuwarudisha pamoja mke na mume waweze kukaa pamoja na kulea familia yao. Na ni vyema pia tukatambua kwamba wale watu ambao wanafanya kazi za serikali halafu wakachukua nafasi ya kuwatekeleza wake zao kwa mazingira ya kwamba keshamuacha lakini amemtupia na watoto. Tutengeneze sheria au tuongeze sheria ya nusu mshahara kwenda kwa mama ya watoto, ili mama yule apate nguvu za kukimu wale watoto wake na watoto wale wapate kujijua kwa sababu

sisi sote akina baba tuna mazingira magumu ukishakumuowa mwanamke ukishamzalisha watoto watatu au wanne basi wewe unatafuta mwengine yule ndio hana maana tena. Hiyo haiwezekani, nchi kama hii ambayo ina utamaduni wake haiwezekani lazima watu walee ndoa na ndoa zisimamiwe. Makadhi wetu wanajitahidi sana katika mazingira ya kuzisimamia ndoa, lakini tunachotaka kusema ni kwamba sisi kama wazazi tuna wajibu mkubwa wa kusimamia ndoa za watoto wetu ili ndoa hizo zisivurugike na ni jambo la busara kabisa kusema kwamba baadhi ya vifungu vya sheria viongezwe ili kuzilea ndoa hizo zisivurugike. Utaratibu ule ambao tumejizowesha wa kuowa na kuacha "*Yuzawwiju, Yutwaliku hatta Yuwafiku*", hiyo sio mikakati ya ndoa, hakuna sababu ya kwamba wewe mwanamke umempenda mwenyewe, umemtaka mwenyewe, halafu unamuowa siku tatu unamuacha kwa sababu kuna maneno watu wanasema; *Yuzawwiju, Yutwaliku, hatta Yuwafiku* hamna hiyo. Hayo ni maneno ya kutunga si maneno ya kitabu wala si maneno ya swahaba yeyote.

Katika jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelichukia ni talaka, Mwenyezi Mungu amelichukia sana neno hili na ndio maana akaweka mpaka mikakati ya yule mwanamke kukaa miezi minne ili wewe umhudumie na ili roho yako irudi muweze kuishi na kulea familia yenu. Yote ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu hayo katika ndoa, leo inafikia hatua kwamba Zanzibar tunacheza na maelekezo ya Mwenyezi Mungu halafu tunawatia dhiki Makadhi, tunawatia dhiki Mashekhe tunafikia pahala tunakuwa sisi ni watu tu tusiokuwa na maamuzi sahihi haiwezekani, lazima ndoa zilindwe na sisi kama serikali tunasema kwamba sasa umefika wakati muwafaka wa kulinda ndoa za Wazanzibari ili zisivunjike ovyo. Tutafikia pahala sisi kama serikali kuhakikisha kwamba wale wote wanaofunga ndoa wanadumu na ndoa zao katika mazingira yale yaliyoelekezwa na kitabu kitukufu cha *Kur-ani*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia ningetaka niseme tu kwamba, sio jambo la busara kwa wanaume watu wazima wenye akili timamu kuwavunjia masomo watoto wa kike eti kwa sababu wanataka kuwaowa, sio jambo la busara. Kwa hiyo, ni vyema tukakubali kwamba wanawake wanahitaji kupata elimu ili kulisogeza taifa hili la Wazanzibari na taifa la Watanzania pale linapotakiwa. Kwa vile ile mipangilio ya kuchukua akili ya mtoto wa kike ukaivuruga na hatimaye ukaweza kumuharibia maisha mimi nashauri kipengele cha kumfunga huyo bwana miaka mitano kirudishwe kama alivyofanya Hayati Mzee Abeid Amani Karume; aliyasimamia hayo basi hakuna ya kuwa yasitokee. Ninaamini chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi anavyotetea haki za wanawake na jinsi anavyozisimamia haki hizo, basi naamini kwamba serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanalindwa katika mazingira ya kutokuharibiwa maisha yao ili waweze kupata elimu hadi kufikia vyuo vikuu.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa niwaombe radhi kidogo, Mhe. Said Soud Said alikuwa katikati katika orodha yangu hapa nikamwita kwa bahati mbaya, lakini kwa vile wachangiaji wapo nisiwakoseshe nafasi naona tutaendelea na kuwaita walioko *back bencher* waendelee kuchangia michango yao na baadae watafuatia mawaziri. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya Mwaka 1985 na kuanzisha upya Mahakama ya Kadhi na kuweka masharti mengine kama yalivyo katika huu mswada.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana serikali kwa kuona kwamba kuna mapungufu katika utekelezaji wetu hasa katika usimamizi wa hii Mahakama ya Kadhi, lakini vile vile na mambo mbali mbali ambayo yanayotekelezwa. Lakini pia kuna mengine hayakuainishwa moja kwa moja kwenye sheria. Kwa hiyo, kutokana na matatizo mbali mbali yanayojitokeza na kuna baadhi yao Waheshimiwa wameyazungumza hapa basi imeonekana wazi kwamba kuna sehemu inapunjwa katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu tuuchangie ukishamalizika basi naamini yale matatizo mengi yaliyokuwa yanajitokeza pengine ilikuwa hakuna muongozo wa kisheria basi yanaweza yakapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nije moja kwa moja katika mswada huu naanza na kifungu cha 3 cha mswada kinachosema, kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi ambapo kifungu kidogo cha (2) kinaelezea kwamba Mahakama ya Kadhi itaundwa na Mahakama ya Kadhi ya Wilaya na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa. Sasa labda nimuulize Mhe. Waziri tunajua utaratibu wa Mahakama zetu hizi kuna ngazi ya Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mkoa na Mahakama Kuu, lakini hii Mahakama ya Kadhi tumeruka moja kwa moja kutoka ngazi ya Wilaya mpaka tunakwenda kwenye rufaa. Sasa sijui kuna sababu gani iliyoonekana hapa ikawa hakuna ngazi ya Mahakama ya Mkoa, hapa kidogo nitahitaji nije nipate ufafanuzi ili tujue nini hasa kilichokusudiwa.

Chengine Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kifungu cha 5(1) kinachosema 'Mahakama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadaawa ni Waisilamu kuhusiana na...' haya mambo nitakayoyataja.

(a) Ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa na ustawi wa familia. Naomba niende moja moja.

Mhe. Mwenyekiti, kuna michango mingi ya wadau hasa wanaotetea masuala ya kijinsia, hapa nazungumzia zaidi akinamama. Katika hii Mahakama ya Kadhi mara nyingi mahakama zetu majaji wanaoteuliwa wanakuwa ni wanaume na akinamama hawa wanapokwenda na kesi zao kuna baadhi ya mambo mengine kiutamaduni na mila zetu wanashindwa kuyaelezea moja kwa moja kwenye jopo la wanaume watupu. Kwa sababu kesi za ndoa na talaka kuna mambo mengine ni nyeti ambayo yanasababisha watu wadaiane hizo talaka au mtu adai talaka kwa nguvu. Sasa nataka niulize katika Mahakama ya Kadhi kwa bahati mbaya mimi sijawaji kuacha wala sijawahi kushtakiwa na mke wangu kwamba namsumbua akanipeleka kwa Kadhi na ninaomba waendelee hivyo hivyo wasije wakaniburuza kwa Kadhi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka niulize katika hii Mahakama ya Kadhi katika uendeshaji wake Kadhi anakuwa mmoja anaamua peke yake au kuna jopo la wasaidizi ambao wanamsaidia katika kuamua hizi kesi? Hili naliuliza kwa sababu moja, kuna mifano ambayo imetokezea ya

kuhadithiwa ni kwamba kama hapa inapofika pahala unaeleza zile kesi lakini kuna mambo nyeti ambayo mtu hawezi kuelezea mbele ya mwanamme moja kwa moja na zaidi mambo ambayo yanagusa masuala ya udhalilishaji wa wanawake. Sasa kama kunakuwa hakuna jopo yaani mfano kama zilivyo Mahakama nyengine kama Mahakama ya Ardhi, kuna Hakimu pale wa Mahakama ya Ardhi halafu kuna wale ma-*assessor* ambao wanamsaidia katika kutoa yale maamuzi. Sasa nilikuwa nauliza je, huyu Kadhi anakuwa na jopo linalomsaidia? Kama anakuwa analo jopo yumo mwanamke japo mmoja ambaye yeye wanashauriana na Kadhi katika kutoa yale maamuzi?

Sasa hapa natoa ushauri, natoa ushauri kwa sababu kwenye vifungu sikusudii kuja kuzuwia kifungu kwa ajili ya kupata ufafanuzi, kwa hiyo hoja yangu naijenga kabisa. Kama Kadhi anakuwa peke yake ambaye anatoa maamuzi hana jopo basi nadhani katika sheria hii tuongeze kifungu kitakachoeleza kwamba Kadhi atakuwa na jopo la kumsaidia katika kutoa yale maamuzi. Katika jopo hilo basi lazima uwepo ushiriki wa kijinsia, yaani wawepo na Maulamaa wanawake ambao watamsaidia katika kutoa hayo maamuzi. Hii ni kwa sababu gani, kwa sababu kama yatajitokeza yale mambo ya mwanamke alikuwa anataka kudhalilishwa na mumewe kama anakuwa anaona haya au anaona aibu kuyaelezea mbele ya Kadhi mwanamme basi ataweza kukaa na wale wasaidizi wa Kadhi wanawake aeleze yale mambo halafu baadae aweze kupatiwa ufumbuzi. Nafikiri hapa tunaweza tukawa tumetengeneza kitu ambacho kitawasaidia akinamama hawa wanapokwenda katika Mahakama hizi za Kadhi na wao kuweza kusikilizwa na hoja zao zote ziweze kujengwa. Vyenginevyo itakuwa kesi inakwenda kuhukumiwa lakini kuna ushahidi mwengine haukuweza kutolewa kutokana na mtu kuona aibu kwa yale ambayo yamemtokezea.

La pili, haya majukumu au mamlaka ya Mahakama ya Kadhi ni kuzungumzia kuhusu suala la ustawi wa familia na hili nataka kidogo nalo nilizungumzie. Kimsingi sijui hili kadhi atalisimamia vipi, kwa sababu kuna baadhi ya Waheshimiwa waliwahi kuzungumza hapa mfano hata Mhe. Bahati Khamis Kombo nilimsikia anazungumza kwamba, kuna sisi akinababa wengine mtu anaowa akishamuona mtu keshamzalia watoto watano anakwenda kuongeza mke mwengine anapiga kule watano, anakwenda kuongeza mke mwengine, lakini watoto wanabakia wanakuwa ni mzigo wa mwanamke. Sasa baba yeye huko anajua wakati shughuli zinakwenda huku nyuma anakuwa anaacha. Sasa hapa sijui udhibiti utakuwa vipi, kwa sababu na hali zetu tunazijua pengine baba kima chake cha mshahara ni cha chini lakini ana watoto 20 au 15, sasa hapa sijui atatakiwa awahudumie vipi ukiacha katika lile suala zima la kuwalisha na kuwaweka katika makaazi yaliyo salama.

Vile vile kuna suala la matunzo na malezi ya watoto waliozaliwa ndani ya ndoa. Hili nafikiri linafanana na hili la ustawi wa familia. Lakini vile vile kuna suala zima la huduma za misaada. Sasa hii huduma za misaada tulikuwa tunataka tupate ufafanuzi hii misaada iliyokusudiwa hapa ni misaada ya aina gani. Kwa sababu katika masuala mazima ya huduma za misaada kwa sababu kama mtu yumo katika ndoa chochote atakachokifanya pale hakuna suala la msaada pale anakuwa anatimiza wajibu wake. Sasa hii huduma za misaada labda hapa pia tuje tupate ufafanuzi ili ijulikane misaada ya aina gani maana siku hizi kuna misaada mingi, kuna wafadhili wanaosaidia mayatima lakini hapa unapozungumzia suala la ndoa ina maana uyatima unakuwa bado haujakuwepo.

Pia kuna suala la wakfu au mali za amana za kidini na hiba na mirathi. Hilo sina tatizo nalo lakini nakuja katika suala zima la wasia. Mhe. Mwenyekiti, sisi Wazanzibari sijui kama tunafika angalau asilimia 20 ambao tunaandika wasia, hii tunajua katika Dini yetu tumehimizwa kwamba tuandike wasia wakati tunapokuwa hai, lakini Waswahili unahisi mtu kwamba ukiandika wasia labda ndio unajichongea kifo. Kwa hiyo, kila mtu anakuwa anasita sita kuandika ule wasia. Sasa iwapo mtu amefariki hakuandika wasia sasa wao hapa hii Mahakama ya Kadhi watachukulia wasia gani ambao ulioachwa na marehemu au labda baada ya kupitisha sheria hii tutatakiwa sote ambao tuna familia lazima tuandike wasia au vipi na uhakiki wake utakuwa ukoje.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kifungu (g) hiki kinasema kwamba "na jambo jengine lolote ambalo Mahakama ya Kadhi imepewa na mamlaka ya sheria nyengine yoyote kulishughulikia". Sasa hapa sisi tunaitunga sheria ya Mahakama ya Kadhi na mimi sijawahi kuona sheria nyengine yoyote ambayo tumeipitisha hapa Barazani iliyoipa mamlaka moja kwa moja Mahakama ya Kadhi kuweza kushughulikia jambo jengine lolote. Kama tulivyoelezwa kwamba hapa Mahakama hii inazungumzia zaidi masuala ya maslahi ya Waislamu lakini vile vile kulinda na mali za Waisilamu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 5(2) naomba nikinukuu kinasema kwamba: "Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki mtu yeyote ambaye si Muisilamu anaweza kufungua shauri katika Mahakama ya Kadhi dhidi ya Muisilamu kwa mashauri ya madai yanayohusu sheria za Kiisilamu".

Mhe. Mwenyekiti, sasa Kadhi anahukumu zaidi katika sheria ambazo zina miongozo ya Kiisilamu na sheria hizi vile vile zinafuata misingi ya sheria za Kiisilamu, sasa huyu mtu ambaye yeye sio Muisilamu na yule Kadhi pale atakwenda kuhukumu kwa sheria za Kiisilamu hii itakuwa ina mantiki gani. Nadhani hii Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu cha 5(2) kingeliondoka. Kwa sababu katika suala la ndoa na mirathi mtu akiwa si Muisilamu ina maana masuala hayo yatakuwa moja kwa moja hayawezi kumuhusu. Kwa hiyo, kifungu hiki cha 5(2) nilikuwa nahisi kiondoke kwa sababu hii sheria inawagusa zaidi wale ambao wanakwenda kushtaki kwenye Mahakama ya Kadhi ambao wote wanakuwa ni Waisilamu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6 kinasema sheria na kanuni za ushahidi zitakazotumika katika Mahakama za Kadhi zitakuwa ni zile tu zinazotumika katika sheria ya Kiisilamu. Sasa kifungu hiki ndio kinachokifuta hiki kifungu cha 5(2) kwa sababu kinatumia hukumu zote zitahukumiwa kwa sheria za Kiisilamu. Kwa hiyo, nadhani hiki kilikuwa kinakazia ile hoja yangu ya juu kwamba kifungu cha 5(2) kiweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nakuja katika kifungu cha 8 kinachosema kutakuwa na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa. Sasa hapa Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwahi kuziona sifa za Kadhi Mkuu, lakini Naibu Kadhi Mkuu sifa zake zimetajwa. Sasa huyu Kadhi Mkuu kwa nini sifa zake hazikutajwa kwenye sheria hii na vile vile inasema kwamba watateuliwa kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa.

Sasa Baraza la Ulamaa nilikuwa naomba nijue au nije nijuulishwe muundo wake unakuwa vipi na katika huu muundo wa Baraza la Ulamaa sijui kama utakuwa umo katika sheria hii au uko

katika sheria nyengine. Lakini hapa ndipo mapendekezo yangu yanapokuja kwa kuwa Baraza la Maulamaa ni chombo ambacho kinachohusisha zaidi ya mtu mmoja ndio hapa napendekeza uwiano wa kijinsia uweze kuzingatiwa.

Kwa hiyo, katika Baraza la Maulamaa napendekeza na kina mama lazima wawemo na kwa sababu kwa bahati nzuri na sisi wenyewe tuliwahi kushiriki wakati wadau walipokuja kutoa ushauri wao tumegundua Zanzibari kuna akina mama wamesoma sana elimu wa Dini tena wanadigirii na wengine wana *masters* za Sheria za Kiislamu tena wamesoma katika vyuo ambavyo vinavyotambulika duniani na tunahisi wana mawazo mazuri sana ya kuweza kumsaidia katika haya masuala ya haki za Waisilamu katika masuala ya ndoa, mirathi na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti.....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda.

Mhe. Hamza Hasssan Juma: Mheshimiwa haya naomba nimalizie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia.

Mhe. Hamza Hasssan Juma: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 9 naomba kifungu cha 9 (2) kinasema:

"Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha kwanza Rais anaweza kuongeza muda wa Utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kama atakavyoona inafaa". Sasa Mheshimiwa kama ukisema kama atakavyoona inafaa mtu anaweza akaja, sitaki kusema akaja kufia kwenye kiti lakini ule umri unaweza ukawa pengine mpaka akawa na miaka 90, kwa sababu hakuna sheria iliyo m-*control* Mhe. Rais kuhusu kumuongezea muda.

Sasa mimi nadhani kwa kuwa sheria inasema kwamba atastaafu itakapofika miaka 60 au miaka 65 sasa hapa lazima kuwe na kipindi kile cha kuongeza mikataba si zaidi ya mara mbili. Sasa kifungu hichi kimekuwa *infinity*, hakina *control* ya aina yoyote. Kwa hiyo, napendekeza kifungu hichi iwe kwamba iwe baada ya ule umri wa kustaafu basi anaweza akaongezwa mkataba wa vipindi wa miaka miwili miwili mara mbili ili baadae aweze kupisha wenzake.

Lakini vile vile kifungu cha 10 (2) kinasema Kadhi wa Rufaa hatoanza kazi ya afisi yake mpaka pale ale kiapo cha utii na kiapo kingine cha utekelezaji wa kazi zake kama inavyoelezwa na sheria sasa hapa sheria ipi. Sasa mimi hapa nilikuwa napendekeza liongezwe neno kama itakavyoelezwa na sheria hii.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ili nimalizie kifungu cha 17(5) kinazungumzia rufaa kutoka Mahakama Kuu na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa. Kifungu cha 5 kidogo kinasema Jaji anaekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hichi atakuwa anatakiwa awe Muisilamu mwanamme. Mheshimiwa hapa tutakuwa tunatunga sheria ya kibaguzi. Kwa hiyo, Katiba yetu ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha 4 hichi cha 17 kinasema:

"Kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 maamuzi ya Mahakama Kuu yatakuwa ni ya mwisho kwa mujibu wa katiba. Sasa katiba hiyo hiyo ya Zanzibar haikubagua hakuna hata sehemu moja kwenye Katiba ya Zanzibar inayotaja mwanamke au mwanamme. Kwa hiyo, hapa nilikuwa naomba kwamba hili neno au awe Muisilamu mwanamme liondoke na ibakie maneno Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hichi anatakiwa awe Muisilamu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, lakini vifungu vyote vinavyoelezea ubaguzi wa kijinsia naomba tuviondoe kama nilivyopendekeza ili hii sheria iwe sheria ambayo ya Kiislamu inayotekelezeka. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ashante Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Sasa namwita Mhe. Said Omar Said nae kuweza kutoa mchango wake.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia japo maneno mawili matatu.

Lakini pia niendelee kuupongeza mswada huu kuletwa muda huu hapa Barazani mswada ambao utairejesha Zanzibar katika hadhi yake ya mwendo uliozoeleka katika Zanzibar ya zamani.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imekuwa maarufu sana duniani kutokana na sekta ya elimu na hususan elimu ya Dini. Zanzibar inaeleweka nchi za Kiarabu, nchi za Ulaya kutokana na fani yake ya Dini ya Kiislamu. Kiasi ambacho kama utamchukua Ulamaa aliyesoma hapa Zanzibar ukampeleka akapambana na Ulamaa aliye na *master* basi ima watakuwa sambamba au mwenye *master* ata-*surrender*. Kwa sababu mwenye *master* amesoma sana lakini miaka 7 kule, lakini aliyesoma Zanzibar barazani amesoma miaka 25 katika kikao kimoja kurasa baada ya kurasa yeye hakusoma kwa kufuata mitaala anasoma ukurasa kwa ukurasa miaka 25. Kwa hivyo, huko Ng'ambo huko yanaithamini ya wanaiamini Zanzibar kutokana na elimu na wataalamu wa Dini.

Kwa maana hiyo, na sisi hapa leo tupo katika kujadili sheria ya Mahakama ya Kadhi au Mahakama ya Kiisilamu. Kwa hvyo, lazima tuende sambamba na Mahakama ya Kiislamu. Kuna mambo kidogo yaliyogongana gongana ambayo hata mwenzangu mchangiaji wa mwanzo au sijui mchangiaji mmoja aliyenitangulia aliliona hilo kuna mambo kidogo yamegongana gongana. Sasa haya tuyafanyie ufumbuzi yaani katika Sera ya Wizara ya Elimu na Sheria yetu ya Kiislamu mambo yamegongana pale. Sheria na Sera ya Wizara ya Elimu ni kwamba msichana haruhusiwi kuolewa mpaka amalize kusoma, sasa mtu kusoma hamalizi eti! Mimi siku moja nilitaka kuoa nikamuuliza vipi akanambia mimi nakutaka lakini mpaka nimalize kusoma nikamwambia aah hukuoleka wewe. Kwa sababu kusoma hakuna mwisho atamaliza lini kusoma.

Sasa kama tutaweka hivyo hawataolewa hawa mvulana ambaye keshaposa anhesabu miaka anahesabu miezi ya harusi. Sasa akiambiwa kuwa mpaka amalize kusoma hamalizi kusoma kwa sababu elimu ni sawa na chombo katika bahari wewe unajiona kama una MV. Mapinduzi kubwa hapa lakini ukiingia kwenye mkondo kila ukienda kwenye mkondo ukifika ule mkondo hasa ndio unapojiona kuwa kumbe huna chombo unahitaji zaidi chombo. Kwa hivyo, sasa na elimu ni hivyo hivyo.

Sasa kwa maana hiyo tuipe nasafi sheria yetu ya Kiislamu kwamba mtoto akifika baleghe aolewe ndio tupo kwa ajili hiyo sasa hivi, tupo kwa ajili hiyo mtoto akifika muda wa kuolewa baleghe aolewe *finish*.

Sera ifanye utaratibu wa kuwasiliana na wazazi wa mtoto na mume na kuweka masharti kwamba wewe unamuoa huyu lakini uhakikishe huyu atafanikiwa katika masomo yake mpaka afikie lakini wakati huo huo ameshaolewa tayari. Hatukukuika sheria yetu hili la kwanza.

La pili katika talaka, wenzangu wametangulia juzi nilikuwa sehemu Michenzani pale kuna jamaa mmoja akanambia unamuona yule hebu muangalie, nikamtizama mwanamme yule ana miaka 37 lakini ameshaoa wake 25 daaa! 25 enhee!. Sasa kwa nini iwe hivyo ni kwamba leo anakwenda kumchukuwa mwari wa mtu anakamatwa anaozeshwa anakaa nae miezi minne anamuacha keshokutwa anakamatwa na mwengine anaozeshwa anakaa miezi sita anamuacha. Sasa Mahakama ifanye kazi hapa iweke taratibu maalum yoyote yule atakaekamatwa na kigori wa watu baada ya kuozeshwa awekewe miaka maalum ya kudumu nae kama miaka 20 au 25 lakini paanzwe hapo. Kwa sababu akifikia miaka 20 wameshazoeana, kwa hivyo hawaachani tena.

Halafu hapo hapo katika kuacha kuna wanaume wanawaacha wanawake baadae wanawadai kitu mahari, ni kweli kwamba wanamke anayedai kuachwa akidai kuachwa....

Mhe. Mwenyekiti: Meshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Said Omar Said: Heee Mtume! anapodai kuachwa mwanamke akadai ana wajibu wa kutoa mahari ampe yule mume nae akatafute mke mwengine anaempenda, lakini sasa mambo lazima yaangaliwe vizuri kwa sababu hakuna mtu anaetaka aachwe kwa nini yule akasema aachwe ina maana keshapambana na mazito pale. Kwa hivyo, Mahakama iangalie vizuri sana.

Mwisho kabisa kwa kuwa muda haupo kifungu cha 6 sheria na kanuni za ushahidi imeambiwa ifuatwe Sheria za Kiisilamu.

Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanakwepa ushahidi, linaweza likatokea tukio pahala yupo akatakiwa ushihidi akakimbia. Sasa ndani ya Uisilamu kwanza neno "shahid" maana yake ni kuona, hii maana ya shahid ni kuona. Kwa hivyo, yule alieona ndio shahidi akata asitake lazima twende hivyo, hakuna shahidi kwamba Mheshimiwa kuna kosa ukanikalie ushahidi alaa! shahidi ni alieona. Kwa hivyo, aliona hakiuki sheria. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said sasa ninamwita Mhe. Mgeni Hassan Juma na yeye kutoa mchango wake.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi ya kutoa mchango wangu mdogo sana katika Sheria hii ya Mahakama ya Kadhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye ametupa uhai na uzima kuja kufanya shughuli zetu za leo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza moja kwa moja na nitaanza kidogo kwenye suala zima la usawa wa kijinsia. Mhe. Mwenyekiti, wengi hapa wamezungumzia suala la kuwa na wasi wasi kwamba sheria hii ina muelekeo wa kumkandamiza mwanamke kwa njia moja au nyengine. Lakini wengi wameonesha kwamba wengi wanataka mwanamke nae ahusishwe katika Sheria hii ya Kadhi moja kwa moja. Mimi niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia kwa upande huo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi la kwangu ni suala zima la ulamaa. Mhe. Mwenyekiti, Sheria inayozungumzia masuala ya Ulamaa iko chini ya Sheria ya Afisi ya Mufti namba 9 ya mwaka 2011. Sheria hii imewataja Maulamaa kwamba ni mtu yoyote mwenye taaluma ya masuala ya Dini ya Kiislamu kwa sababu imetaja hivyo na sheria hii imempa nafasi maana yake mtu yoyote inawezekana sana kuwa ni mwanamke au mwanamme.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mpaka hii leo tunavyozungumza hajawahi kutokea Ulamaa mwamamke. Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu hiyo katika suala zima la kutoa ufafanuzi wa Ulamaa ningependekeza kwamba maana ya Ulamaa awe ni mtu mwenye taaluma ya maslahi ya Dini ya Kiislamu awe mwanamme au mwanamke alieteuliwa kuwa Ulamaa chini ya Sheria ya Afisi ya Mufti namba 9 ya mwaka 2011.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la msuluhishi mwenzangu aliyetangulia Mhe. Tatu Mohamed Ussi alizungumzia kwamba mara nyingi sana wanawake wanakuwa hawapati hali zao hasa wanapokwenda kupeleka matatizo yao ya ndoa na talaka na mara nyingi sana wasuluhishi ambao kama hawa wasuluhishi wapo lakini mara nyingi sana wale ambao wanasikiliza kesi wanakuwa ni wanaume. Sasa watu wanasema kesi ya Nyani wanaipeleka kwa Tumbili, wanawake wanakuwa hawapati haki zao, ni muhimu sana ili kuhakikisha kwamba wanawake na watoto wanapata haki zao katika suala zima la Baraza la Suluhishi wanawake na wao wahusishwe kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kwenye ibara ya 5 kifungu namba 1. Hapa kuna tafauti katika *version* ya Kiswahili na *version* ya Kiengereza. Kwenye *version* ya Kiswahili inazungumzia 5 (1) inazungumzia ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na ndoa, lakini kwenye Kiengereza wanasema *marriage divorce custody of children and other related issue*. Sasa hii *custody of children* imepelekwa wapi kuna tofauti baina ya mambo yote yanayohusiana na ndoa na *custody* ya watoto.

Kwa hiyo, hapa nilikuwa naomba sana pawe na marekebisho ambayo yatasaidia kuweka sawa hii *version* ya Kiswahili na *version* ya Kiengereza. Lakini jengine kuna vipengele ambavyo mimi nimehisi kwamba hivi vipengele ni muhimu sana kuwepo katika kifungu hichi namba 5 ikiwemo kusimamia madai ya mahari, mgawanyo wa mali zilizochumwa kwa pamoja, pamoja na mwanamke kujivua katika ndoa wanaita "ghului".

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana talaka zinatolewa ovyo ovyo hata mwanamke akisema tu anadai talaka apewa talaka bila ya kuchunguza matokeo yake yanaleta migogoro mikubwa sana ndani ya familia. Kwa hivyo, ningeomba vifungu hivi vitatu ambavyo nimevitaja kusimamia madai ya mahari, kwa sababu wengi sana ambao mara nyingi wanaolewa wanatolewa mahari

nusu, halafu anaachwa yale mahari hayajamalizwa anaachwa bila ya kupewa mahari yake ambayo yalitajwa kwamba yatakuwa ni mahari yake siku ya ndoa yake.

Lakini jengine ni mgawanyo wa mali, suala hili ambalo amelizungumza mheshimiwa kwamba mara nyingi sana. Mimi hapa sizungumzii tu kwa sababu mwanamke ndio anayeonewa peke yake, lakini tunaona hata wanaume saa nyengine wanapata matatizo haya. Kwa hivyo, ili mheshimiwa kuliweka tatizo hili bayana tungeweka kifungu cha (i) ambacho kitasema mgawanyo wa mali zilizochumwa kwa pamoja ndani ya ndoa.

La mwisho kabisa ni lile ambalo tumelizungumzia ambalo nimeshalitaja Mhe. Mwenyekiti, linazungumzia kujivua kwa ndoa mwanamke ambalo ni muhimu sana kulifanyia kazi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile mwenzangu ameshalizungumza vizuri sana Mhe. Hamza Hassan, lakini pia Mhe. Rashid Makame Shamsi kifungu 17(5) kidogo kimenitia wasi wasi, hii sheria jamani mnataka kuifanya ni ya kibaguzi. Huyu mwanamme kwa nini tunapozungumzia sheria nyengine tunakataa kusema mwanamke au mwanamme, lakini hapa imeelezwa *clearly* kwamba Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hiki anatakiwa awe Muislamu mwanamme. Sasa kwa bahati nzuri sasa hivi tuna Majaji wanawake ina maana hawa tunawanyima haki ya kuwa Majaji katika Mahakama hizi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala ambalo tunaomba sana liwekwe sawa ili ionekane kwamba ni Muislamu yeyote anaweza kuwa Jaji katika Mahakama hii.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nina mapendekezo ambayo nahisi kwamba katika kifungu cha 21(3) ambacho kinazungumzia uwezo wa kutoa amri na maelekezo ya kumaliza kesi. Napendekeza kiongezwe kifungu kinachosema "mtu hatofaa kushikilia nafasi ya usuluhishi mpaka awe mfuasi na Muumini wa Dini ya Kiislamu, awe Mwislamu mwanamke au mwanamme, awe muadilifu na anayeheshimika asitoke miongoni mwa Makadhi, awe muelewa wa masuala ya Dini ya Kiislamu na awe muelewa katika masuala ya utatuzi wa migogoro"

Mhe. Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu suala zima la ndoa linakwenda sambamba na migogoro sote tunafahamu. Lakini mara nyingi sana wale ambao wanahusika katika kutatua migogoro ya ndoa wanakuwa hawana uwezo au hawana uwelewa mzuri wa kutatua migogoro, hata kama watu wale wana elimu ya Dini ya Kiislamu, lakini bado wanakuwa hawana uwezo wa kutatua migogoro. Kwa hivyo, ningeomba sana suala hili tulitilie maanani na liwemo katika kifungu hiki.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza lile ambalo wenzangu wengi wamelizungumza. Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana serikali kwa kutuletea sheria hii, kwa sababu sheria hii tulikuwa tunaihitaji kwa muda mrefu, kumekuwa kuna matatizo mbali mbali na wanawake wengi wamekosa haki zao kwa sababu sheria ile iliyopita ilikuwa haikidhi mahitaji yaliyokuwepo sasa hivi. Lakini vile vile watoto wengi wamekosa haki zao kwa sababu pia sheria hii ilikuwa imeshapitwa na wakati.

Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, pia ningeomba sana Ofisi ya Kadhi sheria hii pale tu ambapo Mhe. Rais ataisaini, basi sheria hii itungiwe kanuni zake mara moja ili iweze kutekelezeka. Tatizo kubwa ni kwamba mara nyingi kunakuwepo sheria lakini kanuni

zinachelewa na ucheleweshaji wa haki unakuwepo mkubwa sana. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba baada tu ya sheria hii na tunatarajia kwamba leo tutaipitisha sheria hii, lakini vile vile iwe kwamba kuna kanuni ambazo zitakuwa zinaongoza masuala mbali mbali yanayozungumzwa katika Sheria ya Kadhi.

La mwisho kabisa ningeomba vile vile kuna umuhimu mkubwa wa kutolewa elimu suala la ndoa. Tunaona kwamba sasa hivi familia nyingi zinasambaratika kwa sababu wengi wanaingia ndani ya ndoa, lakini hawafahamu nini maana ya ndoa. Kwa hivyo, tungeomba sana Ofisi ya Kadhi suala hili la elimu katika ndoa lipewa umuhimu wake mkubwa, kama hatutolipa umuhimu tutaona sasa namna maadili ya jamii yetu yanavyovurugika.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba vile vile wenzetu Tanzania Bara wana Sheria ya Ndoa, sheria hii ya ndoa inasaidia sana katika kuangalia ustawi wa familia, lakini kwa bahati mbaya sisi hatuna. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali ilete sheria ya ndoa tuipitishe hapa ndani ya Baraza ili nayo isaidie katika kuzifanya familia zetu na ndoa zetu ziwe familia ambazo ndoa zao ziwe ni za kudumu, lakini vile vile kuendelea kuweka ustawi mzuri wa watoto wetu.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nitazungumza kidogo. Nashukuru sana kwa kunipa fursa hii, nawapongeza wengi ambao wamechangia na mimi naamini leo sheria hii tutaipitisha ili iweze kuanza kutumika baada tu ya kutiwa saini na Mhe. Rais. Ahsante nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa nimwita Mhe. Naibu Waziri Khamis Juma Mwalimu naye kutoa mchango wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa fursa hii leo hii ya kupata nafasi hii ya kutoa michango katika mswada wetu huu wa Sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi.

Mhe. Mwenyekiti, katika michango yangu nitakwenda moja kwa moja katika kugusia baadhi ya hoja za wajumbe na kuzitolea ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kwanza kabisa inayohusiana na kuwekwa kwa maneno yaliyotafsiriwa katika utaratibu wa *Alphabetical Order*. Hoja hii Mhe. Mwenyekiti, au ushauri huu tumeuchukua na tutaufanyia kazi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja nyengine ya tafsiri ya neno "Ulamaa" wapi ambapo limetokea. Mhe. Mwenyekiti, neno "Ulamaa" limetafsiriwa katika Sheria ya Mufti nambari 9 ya mwaka 2001 na Kanuni ya Baraza la Ulamaa ya mwezi Machi mwaka 2012.

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja kuhusu kasoro za kimaandishi *typing error* zilizojitokeza katika mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huo umepokelewa na tunaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja iliyoibuliwa na mjumbe kuhusiana na mgongano wa kisheria kati ya Sheria ya Elimu namba 6 ya mwaka 1982, Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 na Mswada wa Sheria hii ya Mahakama ya Kadhi. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba Uislamu unaruhusu mtu kuolewa baada ya kubaleghe, lakini Makadhi wanazingatia pia ustawi

na maslahi bora ya mtoto kabla ya kuwaozesha, kama ilivyoainisha katika Sheria ya Mtoto na Sheria ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine iliyoibuka kuhusiana na Jaji Mkuu kushauriana na Kadhi Mkuu katika baadhi ya mambo ya Mahakama ya Kadhi, ikiwemo kutunga kanuni na rufaa ya Mahakama ya Kadhi kwenda Mahakaka Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa mfumo wetu wa Kimahakama, Mahakama ya Kadhi ni sehemu ya Mahakama Kuu. Kwa hivyo, Jaji Mkuu ndiye kiongozi wa Mahakama na rufaa za Mahakama ya Kadhi zinamalizia Mahakama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine iliibuka kuhusu umuhimu wa kutolewa elimu inayohusiana na ndoa. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu umechukuliwa kwa sababu ni vyema kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata elimu hii ya ndoa kabla ya kuingia katika ndoa. Tunaamini kwamba unapotoa elimu hii ya ndoa kuna baadhi ya migogoro mingine katika ndoa inaweza isitokee.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo kulikuwa kuna suala jengine kuhusiana na aina ya dharau ambazo Kadhi anaweza kumchukulia mtu hatua. Mhe. Mwenyekiti, neno "dharau" mjumbe alikuwa anatoka kulijua, dharau gani hizo au hatua gani ambazo Mhe. Kadhi anaweza akazichukua, na kwenye mswada huu haikuelezwa hatua gani ambazo anaweza kuzichukua.

Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tu mjumbe kwamba baadhi ya mambo ambayo yanakosekana katika sheria, lakini kanuni zinakuwa zinayaingiza. Sasa niseme kwamba zitaelezwa katika kanuni zitakazotungwa kwa kupitia kifungu cha 7 cha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na umri wa kustaafu Makadhi wa Wilaya, hoja hii pia iliibuliwa. Lakini ni vyema tukatambua kwamba muda wa kustaafu kwa Makadhi wa Wilaya ni miaka 55 ya hiyari kama vile watumishi wengine na miaka 60 ya lazima.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na utaratibu wa kuwaondoa Makadhi, sheria hii haikuweka kinga ya kuwaondoa Makadhi kazini, hivyo utaratibu wa kuwaondoa utatumika kama vile inavyotumika kwa wafanyakazi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo iliibuliwa na wajumbe kuhusiana na pendekezo la kuwepo kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mrajis. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu tumeuchukua na Mahakama watatumia utaratibu wake wa ndani kupata wafanyakazi wa Ofisi ya Mrajis.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Kadhi wa Rufaa Pemba, nayo hoja hii pia ilipata nafasi ya kuelezwa na mjumbe. Utaratibu ni kwamba utaratibu huo wa kuwa na Kadhi wa Rufaa Pemba upo, kwa hivyo Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi kwa hilo.

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, hoja iliibuka kuhusu kuongeza idadi ya Makadhi katika maeneo yanayoonekana katika Wilaya zinazoonekana zina watu wengi. Mjumbe alitoa hoja hiyo kwa maana kwamba aliona ni vyema ikaongezwa idadi katika zile sehemu ambazo zinakuwa na watu wengi. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huo umepokelewa na tunaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo ilitolewa ni kuhusu stahiki za Kadhi Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, stahiki anazostahiki kupata Jaji wa Mahakama Kuu ndizo anazostahiki kupata Kadhi Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ilikuwa kuhusu haja ya kuwa na Mahakama ya Kadhi katika ngazi ya Mkoa. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa mashauri ya Kiislamu kesi zote zina uzito unaolingana. Kwa hivyo, kwa sasa hakuna Mahakama za Mkoa katika Mahakama ya Kadhi. Kuhusiana na kuwepo kwa msaidizi Kadhi mwanamke. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nayo pia ilipata kuibuliwa na baadhi ya wajumbe. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii ina tofauti ya kimtizamo kwa mujibu wa madhehebu, mila na silka za jamii husika. Kwa hivyo, kwa mujibu wa taratibu zetu na madhehebu ya waumini walio wengi, bado haikubaliki kuwa na Kadhi mwanamke.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine iliyotolewa na wajumbe kuhusu mgawanyo wa mali. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ya Mahakama hii iliyopewa kushughulikia ni pamoja na mgawanyo huo wa mali.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ilikuwa inahusiana na kuhusu muda wa usuluhishi. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 26 cha mswada huu imeruhusu usuluhishi kufanyika ndani ya wiki mbili, aidha wahusika wanaweza kuomba kuongeza muda.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine iliyotolewa na wajumbe ni kuhusu sifa za Wakili na Wakili kutajwa. Mhe. Mwenyekiti, ushauri huo tumeupokea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kusema kwamba na mimi kwa upande wangu naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia juu ya mia. Lakini pale ambapo tutakapopitisha vifungu niwaombe Waheshimiwa Wajumbe basi tuvipitishe vifungu vyote bila ya wasi wasi wowote, na tunaamini kwamba mara tu sheria hii itakapotiwa saini In Shaa Allah tutakuwa pamoja. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa namwita Mhe. Waziri ili kuja kutoa majumuisho.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Kny. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia salama. Pili ni imani yangu kwamba tutakamilisha zoezi hili kwa busara, hekma na utulivu. Lakini pia tutarudi katika miongozi ya jambo hili ambalo tunakusudia kulikamilisha hapa, ni jambo ambalo linatugusa kwenye nafsi zetu katika msingi wa kiimani, na kama linatugusa katika msingi wa kiimani basi kuna mambo yatatulazimu kurudi katika muongozo wa imani zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukuomba kwanza kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wajumbe wote wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi, kwa michango yao ambayo ililenga kutoa ushauri na maelekezo kwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kufanya mswada wa sheria ya Mahakama ya Kadhi kuwa bora zaidi. Michango yao tumeipokea na tumeichukua na nina hakika

wakati tutakapopitisha vifungu hivi mtaona namna ambavyo kamati hii imeweza kuuboresha mswada huu na kuleta tija na maslahi ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, kipekee naomba nichukuwe nafasi ya kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Machano Othman Said na wajumbe wote waliosaidia katika kutoa ushauri na maelekezo kuhusiana na mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu, hususan kwa wale waliopata fursa ya kuchangia mswada huu kwa maelezo na michango waliyotoa yote inaonyesha dhamira ya kutaka kujenga na kuimarisha uimara wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umepata bahati ya kuchangiwa na jumla ya wajumbe 16 kwa mmoja mmoja kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambuwe waliochangia kwa kusema na wapo wajumbe watatu waliochangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, waliopata bahati ya kuchangia kwa kusema wa kwanza ni:

1. Mhe. Rashid Makame Shamsi
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said
3. Mhe. Omar Seif Abeid
4. Mhe. Mohammed Said Mohammed
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini
8. Mhe. Tatu Makame Ussi
9. Mhe. Shehe Hamad Mattar
10. Mhe. Bahati Khamis Kombo
11. Mhe. Salama Mussa Bilal
12. Mhe. Said Soud Said Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
13. Mhe. Hamza Hassan Juma
14. Mhe. Said Omar Said
15. Mhe. Mgeni Hassan Juma
16. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Aidha waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2. Mhe. Zainab Abdalla Salum na
3. Mohammed Mgaza Jecha.

Mhe. Mwenyekiti kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kuzitolea ufafanuzi ama kuongezea yale maeneo kiujumla baada ya Mhe. Naibu Waziri kutoa maelezo ya ufanisi katika ufafanuzi alioutoa. Maeno makubwa yaliyozungumziwa ni maeneo matatu kwanza ni suala la muundo wa Mahakama kutoka chini mpaka kufika Mahakama ya Rufaa, mpaka kupata Baraza la Maulamaa na kuweza kupata ile *section* ya *High Court* yake.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi kwamba Mahakama ya Kadhi inaanza katika ngazi ya Wilaya inakwenda katika ngazi ya rufaa, na inakwenda katika ngazi ambayo kwa rufaa yake ya kuweza kukaa majaji wanne kwa ajili ya kutoa uamuzi, maelezo ni kwamba katika Uislam makosa yote yana usawa katika kuhukumiwa kwake na kama mtu hakuridhika na ngazi ya kwanza maana yake anapata nafasi ya kulalamika katika ngazi inayofuata. Lakini pia kwa nini kwamba hakuna Mahakama ya Mwanzo hakuna Mahakama ya Mkoa matarajio yetu kwamba si malengo ya kuongeza kesi matarajio yetu kwamba kuona Mahakama hii baada ya kuiboresha kuipa nguvu namna ambavyo Kadhi tumempa nguvu, namna ambavyo tumeongeza kupanua wigo kwa kuona kwamba tumepungua eneo la kuwa suluhishi ni matarajio yetu kwamba kesi kule Mahakamani zitapungua kurundikana, lakini pia wenzetu wa suluhishi watachukua dhima na jukumu kubwa la kuweza kupunguza matatizo ambayo yangeweza kujitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la pili limeonekana ni eneo ambalo limegusa maeneo kwa maana ya kwamba labda mapendekezo ya sheria hii yana sababu au yana muonekano kama wa kubagua baina ya mwanamke na mwanaume hasa katika nafasi za uongozi katika Mahakama hii, kwa maana kwamba katika nafasi za kutoa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema mwanzo kwamba suala hili linatugusa wengi katika nyoyo zetu kwa sababu linatokana na msingi wa kiimani na kama linatokana na msingi wa kiimani maana yake kuna jambo ambalo linatuongoza katika imani yetu, na katika Uislam sheria zimegawika maeneo mawili. Kuna sheria ambazo zinatokana na Qur-ani kuna maeneo ambayo yanatokana na sunna, hadithi, Ijmaa Istihsan na uono wa wana zuoni. Matarajio yangu kwamba tunapozungumza kumpata Kadhi maana yake lazima tujue kwamba tunazungumza kumpata Walii kwa mujibu wa Uislam na miongozo yake, na tutakapomtafuta Walii maana yake tunamtafuta Walii kwa sifa zake zote kwa mujibu wa muongozo wa Qur-ani ama khadithi, ama sunaa, istihsan au hijma.

Sasa haitokuwa busara kama tunazungumzia suala la kiimani tukakubaliana kwamba katika eneo moja tuondoe utaratibu wa kiimani halafu tuongeze katika upande wa pili turudi katika utaratibu wa kiimani Walii maana yake ni kiongozi, hatuna sababu ya kwamba tumkubalie tuwe na Walii katika eneo moja la Mahakama ya Kadhi lakini Walii huyo huyo tumkatae kwenda kutuongoza katika sala katika ibara zetu. Mwanamke ni yule yule tunapompigania haki hapa tujue tunampigania haki katika msingi wa kiimani na miongozo ya kiimani inaelekeza mwanamke yupi atakuwa kiongozi, maeneo yepi hatokuwa kiongozi.

Kwa hivyo niombe tu kwamba jambo hili linahitaji tafakari pana tusiende katika tafakari ya kutizama usawa tu wa kijinsia hapana, turudi katika imani ya Dini yetu nafasi tuliyopewa na maamuzi na haki ambayo tunaweza tukaitumia lazima tufikirie na tuone kwa nini mwanamke akaruhusiwa hili afanye kwa nini hili hakuruhusiwa kufanya kwa msingi wa kiimani, sio msingi wa kinadharia sio msingi wa kimagharibi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba tu kwamba tunapotafakari kwa nini tusiwe na Kadhi Mwanamke tuone tu kwamba tunapomruhusu Kadhi maana yake tunamruhusi kwa maeneo yote, yeye anakwenda kuwa Walii na anatakiwa kutenda haki kwa wakati wote na anatakiwa kusimamia hayo kwa nyadhifa na vitabu vyote na kila wakati anapaswa kusimamia hilo katika msingi na muongozo wa Dini yetu ya Kiislamu.

Lakini la pili limezungumziwa masuala yanayohusu utaratibu huu wa Makadhi kwa nini tumemtaja Kadhi, kwa nini tumetaja mtu mmoja msingi ambao tunakusudia hapa kwamba sheria hii iweze kuwaongoza watu kwa madhehebu yao wote. Dini ya Kiislamu ina madhehebu wapo watu ambao ni Shia, wapo watu wa Sunni, wapo watu wa Ibadhi na katika hao Sunni wengi wetu ndio sisi tunayo makundi hapa wapo wanamfuata Imam Malik, wapo wanaomfuata Shafii, wapo wanamfuata Hambar, wapo wanaomfuata Hanas. Madhehebu yote haya yanahitaji kulindwa yanahitaji kuongozwa ili na wao haki yao iweze kutendeka.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo limezungumziwa ni kwa namna gani Mahakama hii itaweza kupata nguvu katika usimamizi mzima wa suluhishi, madhumuni ya kuwa na wasuluhishi ni kutafuta namna ya kuweza kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu. Ni matarajio yetu kwamba baada ya kuwa na wasuluhishi hawa idadi ya kesi katika Mahakama zetu itapungua tutapata fursa na wigo mpana sasa wa kuona sasa wasuluhishi hawa wanatusaidia katika kufikia malengo na madhumuni yaliyokusudiwa kwamba tunapunguza changamoto ziliopo hivi sasa.

Lakini kubwa zaidi naomba nirudi Mhe. Mwenyekiti, nilikumbushe Baraza lako tukufu kwamba sisi kama viongozi tuna jukumu la ujumla la kuona kwamba tunaendelea kuiyasa kuiongoza na kuielimisha jamii yetu, wengi wa wajumbe waliozungumza wamezungumza suala zima la umuhimu wa elimu ya ndoa na sisi kama Serikali tunakubaliana umuhimu huo tuuchukue sote kwa ujumla wake kwamba tunapaswa kufikisha elimu ya ndoa na madhumuni ya ndoa, madhumuni ya ndoa sote tunayajua kwa maana ya kwamba kila mmoja wetu amshawishi aliye karibu yake kuona kwamba anarudi katika malengo ya muda mrefu ya kuweza kuishi kama wenza.

Lakini suala jengine Mhe. Mwenyekiti, limezungumzia suala la wasia namna ya kuweza kuandika wasia kwa nini watu hawaandiki wasia, tufanyeje ili kulinda wasia nadhani Mhe. Mwenyekiti kama yalivyo mengine masuala ambayo yanahitaji muongozo na maelekezo ya Dini yetu wasia nao pia una miongozo yake, namna ya kuandika, wakati wa kuandika, namna ya utekelezaji wake na vipi utekelezwe. Unatekeleza wasia baada ya kukamilisha yale majukumu ya msingi ikiwemo pamoja na kulipa madeni kama marehemu ameacha, mtatekeleza wasia wake akiwa mtu huyo ameacha mali au hakuacha mali lakini pia kima cha kuweza kusimamia katika ugawaji wa wasia nacho pia kimeelezwa katika misingi ya Dini yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante hoja imetolewa wale ambao wanakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mkono, wasiokubaliana waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 3 YA 1985 NA KUANZISHA UPYA MAHAKAMA KADHI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

SEHEMU YA KWANZA:

UTANGULIZI

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA PILI:

KUANZISHWA MUUNDO MAMLAKA NA USIMAMIZI WA MAHAKAMA YA KADHI

Kifungu cha 3 Pamoja na Marekebisho yake

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ustadhi Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maelezo yake mazuri alivyokuwa akitoa ufafanuzi pamoja na zile fatwa alizozitaja, lakini katika kifungu cha 3(2) niliuliza suala nafikiri hakuwahi kulijibu, nilikuwa naomba tu kidogo nipate ufafanuzi kwamba niliulizia kwamba katika sheria hii tuna ngazi mbili tu za Mahakama. Kuna Mahakama ya Kadhi ya Wilaya na Mahakama ya Kadhi ya Rufaa haikutajwa Mahakama ya Kadhi ya Mkoa, sasa hapa tulikuwa tunataka ufafanuzi kidogo wa kisheria ili tuendelee ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna Mahakama ya Kadhi ya Wilaya na tuna Mahakama ya Kadhi ya Rufaa, lakini kama Mheshimiwa Mjumbe alikuwa ananisikiliza vizuri nimesema kwamba katika kuliona hilo Serikali imekuja na mapendekezo kwamba katika hii Mahakama ya Kadhi ukitizama ile wingi ambao tumeufungua wa usuluhishi maana yake itachukua jukumu au dhima ya kupunguza kesi nyingi sana.

Lakini la pili kwamba hatuna Mahakama ya Mkoa ya Kadhi kwa kutambua kwamba hii Mahakama ya Kadhi ni *Division* katika Mahakama Kuu na hapa Mahakama ya Kadhi ina mambo maalum ambayo inakwenda kushughulikia.

Lakini la tatu kwamba Mahakama hii ya Wilaya inazungumzia katika masuala ya Wilaya na yanapokwenda kwenye rufaa haimaanishi kwamba kuna nafasi imekiukwa ya Mkoa, ukitizama katika Mahakama ya Kawaida kuna ngazi zile kutoka ya kwanza Wilaya, Mkoa, Taifa zinatokana na wingi wa kesi na mifumo yao maana kwamba Mahakama zile zinazungumzia *civil*, zinazungumzia *criminal* pamoja na mengine. Sasa Mahakama hii ya Kadhi inazungumzia vitu maalum kwa watu maalum wenye imani maalum, kwa hivyo tuna imani kwamba kuanza na ngazi ya wilaya kuja zako Taifa kwa kutambua kwamba tumetengeneza *corridor* ya kuwa na usuluhishi imani yetu ni kwamba Mahakama itakuwa imejitosheleza na mrundikano wa kesi ulipo sasa utakuwa umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nimeridhika na hoja za Mhe. Waziri kwa kuwa ameeleza kutakuwa hakuna mrundiko mwingi wa kesi katika Mahakama ya rufaa basi naomba tuendelee.

Kifungu cha 5 Mahakama ya Kadhi, Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, pia tu nilikuwa nahitaji ufafanuzi katika hili katika kifungu cha 5(2) kinachosema bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki mtu yoyote ambaye si Muislam anaweza kufungua shauri katika Mahakama ya Kadhi dhidi ya Muislam kwa mashauri ya Madai yanayohusiana na Sheria ya Kiislamu.

Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti ilikuwa inasema kwamba hii Mahakama ya Kadhi inahukumu kwa mujibu wa Sheria za Kiislamu sasa unapotoa nafasi mtu ambae si Muislamu kwenda kushitaki kwenye Mahakama ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi inahukumu kwa kufuata misingi ya Sheria za Kiislamu pamoja na kitabu chetu, sasa huyu si Muislamu hicho kitabu chenyewe hakitambui wala Sheria za Kiislamu hazitambui ataweza vipi kukubaliana na hukumu itakayotoka katika Sheria za Kiislamu ambazo yeye hazitambui.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa suala la Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini mimi naomba labda niseme kidogo tu ili labda anifahamu vizuri Mhe. Hamza Hassan Juma, elimu ya ujumla katika suala la Uislamu ukisoma tafsiri ya Uislamu hukumu taratibu na sheria inaelezea maana Uislamu ni kitu kisafi, kwa mtu ambae si Muislamu unapomwambia jambo la Uislamu maana yake unamjenga imani kwamba Uislamu ni kitu kizuri kinacho muongozo sahihi na

tunayo mifano. Tunaishi na watu ambao sio Waislamu unapofika wakati wa kuchinja haridhiki nafsi yake kama hajenda kuchinjiwa na Muislamu ili kile anachokila ahakikishe kwamba kiko halali.

Lakini inatokezea wakati kuna mtu ambaye sio Muislamu anahitaji kununua au kuuza nafsi yake yeye inamuongoza kwamba mimi nikifanya jambo hili katika misingi ya Kiislamu nafsi yangu itakuwa imeridhika zaidi, ndio Mahakama hii inatoa nafasi kama wewe una jambo lako si Muislamu unataka litendwe kwa Uislamu wewe mwenyewe ukiwa umeridhia maana yake Mahakama imepewa nafasi ya kuweza kusimamia jambo hili.

Hayo sio mageni wakati wa uongozi wa Sayyidina Umar ibin Khatab Alayhi Wasalam alikuweko Kureshi ambae hakuwa Muislam alikuwa ameokota ngao ambayo ilikuwa ngao ya Muislamu, walipokwenda kudai yule mwenye ngao alikuwa ni Muislamu lakini alishindwa kutoa uthibitisho wa kuainisha kwamba ngao hii yangu ni ya kwangu, Umar akamtunuku yule ambae alikuwa ameokota ambae hakuwa Muislamu na yeye ikawa ni kivutio cha kumuingiza katika Uislamu kwamba kweli hii ni Dini ya haki na hii ni Dini ambayo inasimamia bila ya dhulma. Huyu kwa kushindwa kwake kutoa uthibitisho kumenipelekea mimi kupata haki lakini kwa sababu mimi ninajua nimeiokota akamrejeshea na yeye akaingia katika Uislamu, kwa hivyo hapa ni sehemu ya kuwavutia wasio Waislamu kuja katika Dini ya uongofu. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua leo kitabu changu nimekisahau ningeliweza kumjengea hoja lakini mimi hofu yangu inakuja hapa ukiangalia msingi wa kifungu cha tano kinasema Mahakama ya Kadhi itakuwa na Mamlaka ya kipekee katika masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadaawa ni Waislamu, yaani wadaawa hapa kwa mujibu tulivyotolewa ufafanuzi ni mlalamikaji na mlalamikiwa. Hapa kifungu hichi kidogo cha pili kinapingana na hichi kipengele cha 5(1) kwa Sababu huku kimesema kesi zote ambazo wadaawa ni Waislamu kuhusiana na haya mambo mpaka (j) sasa lakini hichi kifungu kidogo cha pili naona kinapingana na kifungu hichi, hapa kaingizwa mtu ambaye siye muislamu, maana mfano tuje kama kesi ya ndoa. Ndoa ina maana hapa kwa sheria zetu za kiislamu mwanamke na mwanamume wa kiislamu sijui labda mufti utaniambia kwamba hii itakuwa inasihi hapa au vipi.

Kwa sababu hapa kama ikija katika masuala ya kesi kwa Kadhi inamaana watakwenda kushtakiana sasa hapa ndo kidogo nnapata tabu kwa sababu ningepata maelezo ya ziada ili nikaweza kuridhika na ndio maana nikapendekeza hichi kifungu kidogo cha pili kifutwe ili kisije kikagongana na hichi kifungu cha kwanza cha tano ahsante naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti labda nimrejeshe Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba nimuombe asome vizuri haya maelezo ya kifungu cha pili, kwa maana ya kwamba ukianza kusoma Mhe. Mwenyekiti kinaeleza wazi kabisa.

> *"Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hichi kwa maana kwamba kile cha kwanza, mtu yoyote ambaye si muislamu anaweza maana yake tafsiri yake kwamba yeye mwenyewe akiwa amevutiwa atapata hiyo fursa ya kwenda katika Mahakama ya Kadhi kwa lile ambalo analiomba".*

Lakini yeye kwa sababu si muislamu kama hakuvutiwa atafata utaratibu mwengine kilichoelezwa hapa kwamba ikitokea mtu ambaye si Muislamu, yeye mwenyewe amevutiwa na kutaka kufata utaratibu wa kiislamu katika madai yake anayoyadai maana yake mwenyewe atakuwa ameridhia sheria ya kiislamu imuongoe, haimanishi kwamba wewe muislamu una mgogoro na mtu ambaye si muislamu ukamshtaki katika Mahakama Kadhi hapana. Yule ambaye si muislamu akiwa amevutiwa na sheria za kiislamu katika Mahakama ya Kadhi yeye amepewa nafasi ya kuweza kwenda kufikisha shauri lake katika Mahakama ndivyo kifungu kinavyoelekeza, na mimi kwa upeo wangu naamini kifungu hichi kimesaidia na kuongoza vizuri zaidi.

Na hakuna sababu ya kukifuta kwa sababu tukikifuta hiki, maana yake akitokezea mtu ambaye si muislamu akiwa amevutiwa na sheria za kiislamu hawezi tena kuja kutafuta muongozo katika sheria zetu za kiislamu katika Mahakama ya Kadhi, kuendelea kubai kifungu hiki maana yake tunampa nafasi yeye kumpa nafasi pana ya kuweza kujipima na kutafakari kama amevutiwa na sheria za kiislamu ili aweze kutendewa haki kwa lile ambalo ameweza kuwa na changamoto nalo, Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti labda basi nisaidie ufafanuzi wa kisheria kwenye maandishi unaposema bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki, kifungu chenyewe ndo hicho kinacholingana na hicho kifungu kidogo cha kwanza. Sasa hapa hatuoni basi labda ingelikuwa bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu cha

5(1), kwa sababu ukisema bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, sasa kifungu hiki ndo maana tayari kinajieleza lakini hapa kifungu hichi athari yake nnavyohisi mimi kitakuwa bila ya kuathiri kifungu hichi kilichotanguliya cha 5(1), kwa sababu ukieleza bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki inamaana kifungu hichi ndo kinajiombea mwenyewe ikiwemo kwenye sheria. Sasa hebu mngelitusaidia unajua hii mambo ya uandishi wa kisheria hii kidogo una namna yake ungelitusaidia hii tafsiri bila ya kuathiri yaliyoelezwa katika kifungu hiki je inaingia hapa hapa au tufanye marekebisho bila ya kuathiri kifungu cha 5(1) labda mtusaidie wanasheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mjumbe na inawezekana ikawa kuna kosa la *typing,* lakini ukirufaa na kile kifungu cha kiingereza kiko vizuri kabisa.

> *"Without prejudice the provision of sub section (1) of this section, any persom may submit a claim to the Kadhi's Court for any matter that the Kadhi's Court have jurisdiction".*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nadhani *concern* inafaa ya kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma umesharidhika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nashukuru, nakushukuru sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo nihoji kifungu kimekubaliwa pamoja na marekebisho yake.

Wajumbe: Ndio.

Kifungu 6. Sheria ya Ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kimekubaliwa.

Wajumbe: Ndio.

Kifungu 7. Kanuni za Taratibu na Utendaji kazi na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nimejaribu kuleta *schedule of amendment* lakini wakati Mhe. Waziri anazungumza hakuweza kuweka wazi kama kakubaliana na mimi au la juu ya kifungu hichi na wakati nimeongeza kifungu cha pili katika nambari 7. Naomba maelezo tu kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti maelezo ya Mheshimiwa Mjumbe anataka tuongeze tuwe na kifungu 7 cha (2), maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti nadhani yatakuwa yanakinzana na utaratibu wa kiuandishi wa Sheria, na nnasema hilo kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kifungu kinavyosomeka naomba nikinukuu.

> *"*Kwamba Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi Mkuu atataunga Kanuni za Mahakama ataandaa Kanuni za utaratibu na utendaji kazi utakaotumika katika Mahakama ya Kadhi".

Sasa anachokiomba Mhe. Mjumbe naomba ninukuu katika pendekezo lake kwamba kifungu cha 7 kirekebishwe kuongeza kifungu kidogo kipya cha 2 na kisomeke kama ifuatavyo:-

> *"*Kanuni zitakazotungwa chini ya kifungu hicho cha kwanza cha kifungu hichi hakitatumika katika kucheleweshа au mkosesha mdaawa kupata haki zake kwa misingi ya taratibu tu".

Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunachokizungumza hapa ni kwamba tunatengeneza Sheria kwa ujumla wake, jukumu la kutunga Kanuni tunalibakiza kwa Jaji Mkuu. Kama vile sheria nyengine tunatunga sheria kwa ujumla, jukumu la kutunga Kanuni tunalibakiza kwa Waziri. Sasa ukiongeza haya maneno anayosema Mhe. Mjumbe, maana yake ile *format* na ile *standard* ya waandishi wa sheria itakuwa tunaikiuka.

Maana yake itatulazimu sasa hivi kila sheria inayokuja haya maneno yawe yana *refer* kwa maana kwamba tumetunga sheria ni jukumu sasa la Jaji Mkuu, ambaye ili sheria hii itekelezeke vizuri ni lazima yeye kuchukua muda mfupi katika uandalizi na kuweza kuona kwamba Kanuni zinatumika ili sheria na malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa. Kwa hivyo sikubaliani na Mjumbe kuongeza kifungu kipya isipokuwa ningeomba tu kiendelee kusomeka hivi hivi kilivyo na jukumu tuendelee kumsihi na kumtaka Jaji Mkuu atunge Kanuni ili sheria hiyo iweze kutumika vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na hapa tunatunga imani, tunasema tunakwenda kwenye imani na imeonekana sana kuna vipengele vingi ambavyo vinamkosesha yule mdaiwa kushelewesha kesi, tusema mathalan *affidavit* au nimezungumza jina limekosekana "o" na hii tunakwenda kwenye imani hatuendi kwenye kutunga zile sheria ambazo tunasema sio za Kiislamu, hapa tunakwenda kwenda kwenye Sheria za Kiislamu. Kwa hivyo mimi bado nataka kukinzana naye sana na alisema lazima

tunakwenda kwenye imani, kwa hivyo nahisi kipengele hichi bado kina umuhimu mkubwa wa kuweza kukiendeleza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti atupe *concern* yake kitu gani, maana yake hatuwezi kubadilisha utaratibu wa uwandishi wa vifungu vya sheria kwa kusema kwamba kanuni hizi zisimuadhibu mtu, hatuwezi kuandika hivyo sheria sasa atupe *concern specific* atuambie tuweze kujua lakini hapa tulichokisema kwamba tunamaliza kupitisha sheria jukumu la kutunga Kanuni liltakuwa la Jaji Mkuu, sasa yeye kama hakubaliani na hicho, atamwimbie hicho ambacho yeye anakipendekeza. Sisi pendekezo letu ni kuona hilo kwamba tumalize kupitisha sheria, jukumu la kutunga Kanuni libaki kwa Jaji Mkuu.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti hapa tunatunga sheria tukisema sasa tunampa jukumu Jaji Mkuu ya kutunga Kanuni mimi nipo kwenye sheria ndogo ndogo za Kanuni vile vile, lakini tuna uzowefu mkubwa sana kwa hizo Kanuni, hatuzioni wala hazipiti kabisa hapa sisi tutakuwa na jambo gani na hapa tunatunga Sheria, mimi ningeona kifungu hichi bado ipo haja ya kuweza kukiangalia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu, hebu tupe ufafanuzi kama una maeliza ziada, tupe maelezo ya ufafanuzi zaidi kuhusu Kanuni hii.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo amesema.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Mahakama ya Kadhi inapotekeleza kazi zake, inafanya kazi hizi kwa kutumia sheria ya ushahidi, *no* Sheria ya *Civil Procedure Act* (sura ya 8), Sheria kwa Kiswahili inaitwa Sheria ya Mwenendo wa Madai sura ya 8 ndio inayotumika sasa hivi, ukitizama na ile sheria kubwa kidogo na imeandikwa kwa Kiingereza. Kinachoandikwa hapa nadhani Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) anachotaka ku-*emphasize* anatochaka kutuelekeza ni kwamba tunapotunga zile Kanuni tuondoe kwa Kiingereza wanazoita *technicality*, kwa sababu kwenye sheria hii ya ya *Civil Procedure Act* tuna hizi *technicality* nyingi unaweza kuandika madai yako ukaipeleka ukaambiwa hujaitia saini kwa hiyo yale madai yanakataliwa, unaweza ukapeleka yakawa hujatiwa tarehe yale kwa hiyo madai yanakataliwa anachotuomba Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kama tunapotunga hizi Kanuni basi tuwe makini ili *technicality* ndogo ndogo tuziondoe.

Sasa hoja yake mimi ninadhani kama alivyosema Mhe. Waziri ni sawa, lakini haina haja kuwekewa kifungu ni kama ushauri ambao ameutoa nadhani Mhe. Waziri amekubaliana na ushauri huo basi tutakapotengeneza hizi Kanuni tutajaribu kwa namna pana sana kupunguza hizi *technicality* ambazo zipo sasa hivi. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nimemfahamu sana *Attorney General* tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa kifungu kimekubaliwa.

Wajumbe: Ndio.

Kifungu 8 Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi na Marekebisho yake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naendelea tena kukushukuru kwa kunipa nafasi nikapata ufafanuzi nilipokuwa nikichangia katika kifungu hichi kinachosema kutakuwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa.

Sasa humu katika tafsiri kulikuwa hakuna neno Baraza la Ulamaa, isipokuwa kuna neno Ulamaa, sasa tukajaribu kuangalia katika ile Sheria ya Kadhi hili Baraza la Ulamaa halijatajwa moja kwa moja sasa tulikuwa tunataka nijue upatikanaji wa hili Baraza la Ulamaa liko katika Sheria ipi. Ili tujuwe hili Baraza la Ulamaa ambalo linamshauri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi linapatika katika eneo gani, kwa sababu hapa kwenye tafsiri imeelezwa tu tafsiri nani Ulamaa sasa hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti *concern* aliyoonyesha Mhe. Mjumbe katika maeneo ambayo yametafsiriwa ni jumla eneo hilo halikuwahi kutafsiriwa lakini yeye anataka kujua kwamba Baraza la Ulamaa linapatikana wapi kwenye sheria, nadhani tumerejea ukisoma ile Sheria ya Mufti, Sheria Nam. 9 2001 nadhani kifungu 17 au 15 kimempa nguvu Mhe. Waziri anayesimamia Ofisi ya Mufti kwa kuweza kutunga Kanuni. Ni imani yetu kwamba katika Kanuni zile zimetungwa na Mhe. Waziri ukenda ukasoma utalikuta Baraza la Ulamaa, ambapo kwa sheria hii ina-*refer* ya Sheria ya Mufti katika uanzishaji wa Baraza hilo la Ulamaa, kwa hivyo Sheria ya Mufti inaongoza huo mtiririko, sifa na nini maana halisi ya Baraza la Ulamaa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa nitakwenda kuangalia Kanuni, tuendelee.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kushukuru wakati nikichangia nilileta kwa muendelezo *schedule of amendment* ambayo li-*press* kwake Mhe. Waziri lakini bado sikupaka jibu, naomba jibu litoke.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 8 ambacho Mhe. Mjumbe amependekeza kufanya marekebisho anapendekeza kama katika katika kifungu cha 8 (5) tuengeze kifungu cha (d) ambacho katika kifungu cha (d) anataka tuengeze kwamba " miongoni mwa sifa za mtu kuweza kushika nafasi za Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu awe na umri usiopungua miaka 40.

Sasa kuweka umri sio tatizo lakini nadhani tutakuwa na *binding* sasa kwa maana kwamba utumishi wa Serikali unatengeneza utaratibu kwamba nafasi ya Serikali inawekwa kuipata kwa sababu wa ukomo wa umri wa mtu mwenye sifa, ukisoma sheria zetu za utumishi, Katiba iko *very clear* kwamba waliowekewa ukomo wa umri ni viongozi, hasa viongozi wa kisiasa. Mwakilishi tumewekewa miaka 21, Rais amewekewa miaka 40, hawa waliobakia ni watumishi wa Serikali sidhani kama itakuwa busara tuchukuwe kikomo cha umri kama kiwe kilingo cha kumtafuta mtumishi mtu ambaye ana sifa kwa sababu tu hajafikisha umri huo, iwe sisi tunamtoa kwa sababu hajakamilisha umri.

Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, sifa zilizoelezwa zinamuwezesha mtu kuwa na busara, hekma na uwezo wa kuweza kuongoza, tukianza kuweka umri ili mtu apate nafasi awe na umri kadhaa manaake tutafika mahali katika nyengine za utumishi wa umma tutalazimisha watu waliopewa nafasi wawe na umri huo. Lakini ukitazama nadharia Mhe. Mwenyekiti ukitizama sifa na uzowefu uliotajwa *obvious* mtu atakayeshika nafasi hiyo atakuwa mtu ambaye ame-*mature* ana upewe na busara kubwa.

Lakini mimi sioni mantiki ya ulazima wa kuweka umri maana yake ukitokezea yule ambaye hajatimiza umri anaweza akawa na sifa zote hizo, tukawa tumemnyima na tukawa tunatengeneza *precedent* mbaya kwa kuona kwamba nafasi za utendaji katika Serikali tunazipeleka kwa mtindo umri na kuwanyima watumishi ambao wana haki na fursa na sifa zinazostahiki. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nimeelewa maelezo marefu sana ya Mhe. Waziri wakati akizungumza, nimesema hapa tunatunga Sheria lakini sheria tunayoitunga hapa tunaongeza Dini na imani. Lakini niki-*refer* kuwa miaka 40 ndio mtu ameanza kuwa "shaib", ameanza kutekeleza yale maagizo muhimu sana kama Mtume wetu S.A.W alipopewa Utume alikiwa na miaka 40, lakini nina *refer* kifungu Nam. 10 anasema mtu hatofaa kuteuliwa kuwa Kadhi wa Rufaa awe Muumini, lakini 1 (b) awe na umri angalau miaka 40 sasa huku tunamteua Kadhi na Naibu Kadhi hatujaweka *limit*, lakini huku Kadhi wa Rufaa tunasema awe na miaka 40 hainiingii akilini kwa hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) imwingie akilini, imwiingie akilini kwa kuona kwamba malengo na madhumuni ni kutaka kujenga wala si kwa lengo la kutaka kushindana au kufanya tambo au kubishana aah! mimi sidhani kama tuna lengo hilo. Mimi nime-*raise concern* zangu kwamba huyu ni mtumishi wa umma tukifika pahali tukitengeneza umri iwe ndio kigezo cha mtu kumpa nafasi manaake na huko kwengine itatubidi tukaweke kigezo hicho hicho.

Kwa hiyo kama yeye ameona kuna pahali pamewekwa umri anayo nafasi ya kuhoji na tutatoa maelezo na kama kuondoa tutaondoa sisi tunachoamini kwamba mtumishi wa umma hakuna sababu ya kumuekea kigezo cha umri, hakuna sababu ya kumuekea kigezo cha umri kwa sababu utumishi huo wa umma haulazimishi kwamba mtu mwenye umri maalum ndio apewe nafasi, isipokuwa Serikali inatengeneza utaratibu na sifa ambae atakuwa amekidhi zile sifa ana haki ya kupewa hiyo nafasi kwa hivyo nimuombe Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) imwingie akilini wala asiwe na jazba wana asiwe na pupa tupo kwa ajili ya kutaka kujenga kuwa na sheria nzuri itakayowaongoza Waislam katika mambo yao ya *Matrimonial* na mambo mengineyo kama hayo ili kuweza kuona haki inatendeka vizuri kama yale malengo ya kuanzishwa kwa sheria hii.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, hapa hatujibiani mipasho tunajibiana kile kitu ambacho kipo. Mimi sikuwa na jazba na tunatunga sheria na kila mtu anatunga kwa upeo anaouwona na anawakilisha jimbo lake kadri anavyoona inafaa. Sasa mimi nimesema kumchagua Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu haielekei kwamba tusiweke umri wale watu ni wakubwa sana na hawa ni lazima tuweke miaka 40 nimenukuu Mtume wetu Muhammad (SAW) alipewa Utume akiwa na miaka 40 kwa sababu tayari alikuwa ameshakuwa "shaib" na hapa tunakwenda kwenye Dini na imani, sasa ni lazima miaka hii 40 hapa iwepo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tuongozwe vizuri na kiti chako ndiyo kituongoze vizuri. Mimi naamini kwamba kwa vigezo hivyo hivyo vya Mitume ipo Mitume ambayo imepewa Mitume chini ya miaka 40 akiwepo Nabii Issa bin Maryam (AW) amepewa Utume chini ya miaka 40 alikuwa ana miaka 33 ameiongoza dunia kwa wakati wake alipoondoka amekuja Mtume Muhammad (SAW) na yeye ameongoza dunia kwa wakati wake.

Mhe. Mwenyekiti, niombe tu *concern* yetu ipo *very clear* kwamba tunachoona kwamba tunaondoa umri kwa sababu tu kwamba huyu ni mtumishi wa umma kama tunaweka kigezo cha umri na kwengine tutakuja kupata matatizo hayo hayo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nadhani mara tatu imeshafika basi tuamue tu Baraza likiamua sisi hatuna pingamizi na hilo kwa sababu wale wengi watakuwa wameamua na huo ndiyo msingi wa demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumezisikia pande zote mbili sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri kwamba iendelee kama ilivyo, wanaoungana na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa). Waliokubali ya Mhe. Waziri wameshinda.

Kifungu cha 9	Muda wa Utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 10	Kadhi wa Rufaa Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 11	Kadhi wa Wilaya Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 12	Mrajisi wa Mahakama wa Kadhi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 13	Uwezo na Kazi za Mrajisi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 14	Bajeti na Fedha za Mahakama ya Kadhi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 15	Lugha ya Mahakama ya Kadhi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 16	Mahakama ya Kadhi ya Rufaa Pamoja na Marekebisho Yake

Kifungu cha 17 Rufaa Kutoka Mahakama ya Kadhi ya Rufaa

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kifungu cha 17 nilifanya *reference* kifungu cha 17(4) kinachosema kwa kuzingatia masharti ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Maamuzi ya Mahakama Kuu yatakuwa ndiyo ya mwisho.

Lakini vile vile hoja yangu ilikuwa kwenye kifungu cha 17(5) kinachosema Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hichi anatakiwa awe Muislamu mwanamme. Kwenye Katiba ya Zanzibar sijaona hata eneo moja linalozungumzia aidha mwanamke au mwanamme kwa maana hiyo nilipendekeza kwamba kifungu hichi tuondoe neno Muislamu mwanamme na ibakie kama hivi ifuatavyo.

Jaji anayekaa Mahakama Kuu chini ya kifungu hichi anatakiwa awe Muislamu hili neno "mwanamme" litaonyesha ubaguzi wa kijinsia na ubaguzi katika sheria, lakini vile vile Katiba tutakuwa tunaikiuka. Sasa naomba sana Mhe. Waziri anikubalie kwa sababu hili neno mwanamme kidogo halituletei afya, libakie tu Muisilamu kwa sababu mteuzi yeye mwenyewe ndiyo anayejua. Lakini ukisema mwanamme hapa ina maana tayari Katiba hapa inabagua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikiliza kwa umakini sana maelezo ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambapo amenukuu Katiba katika kifungu cha 4 na kukiainisha na kifungu cha 5 na kusema kwamba labda tunahisi jina Katiba kwa kuona kwamba tumekuja na jambo kwamba linabagua.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimtoe hofu Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba katika kifungu cha (5) hatujabagua isipokuwa tumeongeza sifa kati ya hao Majaji tumeongeza mwenye sifa ya uwanaumme, hatujambagua mtu. Jaji maana yake aidha awe mwanamme au mwanamke, tulichokiongeza hapa ni sifa ya ziada kwamba katika hao Majaji awe mwanamme. Awe mwanamme kwa sababu tunakwenda hapa kutafuta mtu wa kutoa fatwaa kwa maana ya kwamba ikifika pahali ya kwamba kura au kuna mgongano katika suala la kiimani yeye kama mwanamme Muislamu anapata nafasi ya kutoa fatwaa.

Nasema hivyo kwa sababu tu Mahakama yetu ni *secular* ambayo haina msingi wa Dini, tunao Majaji ambao siyo Waislamu ambao wana sifa zote za kuhukumu. Lakini kwa sababu jambo hili linagusa imani ndiyo tukaanza na huyo Muislamu kwa sababu hili jambo linagusa imani, ndiyo maana katika hao Majaji tukachagua awe Muislamu, la kwanza.

La pili katika hao Waislamu mwanamme atakuwa na sifa ya ziada na kwa sababu sote tunajua kwenye msingi wa Uislamu nafasi ya mwanamke na mwanamme ziko sawa lakini ikifika wakati wa uongozi mwanamme amepewa shufaa ya kusogea mbele katika uongozi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ndio pale niliposema haya yanawezekana yakaonekana machungu, yakakera, yakabughudhi, lakini tunarudi katika msingi wa imani yetu ndiyo unaotuongoza. Kwa bahati mbaya katika Uislamu hatukupewa nafasi ya kufanya *amendment* aidha ukitaka kufanya *amendment* utoke, ukibaki katika Uislamu maana yake uufate wote kwa ujumla wake na katika hili ndiyo maana hatukumbagua kwa kusema labda mwanamke aah! hapana. Mwanamme hapa maana yake ni sifa ya ziada kwamba huyo ni kiongozi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Hamza Hassan Juma hatuna dhamira kumbagua mwanamke na mwanamme hapa, hatuna dhamira ya kuiharibu jina la Katiba ya Zanzibar, hapana tumesema sifa ya kwanza ni Muislamu, sifa ya ziada awe mwanaume. Sasa mimi nikuombe tu Mhe. Hamza Hassan Juma tukubaliane, tupitishe vizuri tuendelee mbele ili haki ikasimamiwe vizuri kama utaratibu wa Dini yetu, miongozo ya Sunna, Ijma, Istighfani zinavyotutaka tufanye. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Hamza tupitisha kifungu hichi.(*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kweli tunapitisha sheria ambayo inatugusa moja kwa moja katika misingi ya imani lakini huyu Jaji ambaye atakaekuwepo katika Mahakama Kuu ya Rufaa. Huyu Jaji hakuna *Interview* kwamba zitatangazwa watu wanakwenda kwenye *Interview* atakayeshinda, huyu anateuliwa na kwa kuwa anateuliwa kwa kushauriana na Baraza la Ulamaa. Hilo Baraza la Ulamaa wataangalia fatwaa, wataangalia na mambo mengine yote, wao wakishakufika pahala wakaona sisi Baraza la Maulamaa kwa elimu zetu tunahisi Bi. Khadija anaweza kuwa Jaji ina maana hili litakuwa halikotoka hivi limeotoka kwe wenye taaluma ya Kiisilamu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukiweka lazima iwe sifa ya ziada ni mwanamme, sasa wewe utegemee hilo Baraza la Ulamaa kama Dini ya Kiislamu halikubali huyu Jaji wa Mahakama Kuu ya Rufaa watamteuwa mwanamke. Mimi nafikiri Mheshimiwa hapa tutapiga kura kwa sababu moja tu kwamba huyu mtu ni tofauti na ajira nyengine zinatangaziwa mwenye sifa lakini huyu Jaji anateuliwa baada ya kuchujwa na sifa zote, sasa hata ukaona kapenya kwa Maulamaa basi ina maana ndiyo tayari vitabu na sheria na kanuni zisharuhusu.

Sasa mimi bado nataka niseme tukitia hili neno tunatunga sheria ya kibaguzi na Uislamu haumbagui mtu na kwa kuwa kuna uteuzi bado naendelea kusema hizi ingelikuwa watu wanashindana, hizi Mheshimiwa huyu mtu Jaji anateuliwa tena na Jopo na Baraza la Maulamaa, hata ukaona wao wamekaa wakaamua kwamba Jaji huyu awe mwanamke sasa hilo litakuwa siyo kosa, lakini tukiliingiza katika sheria itakuwa tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, unajua zamani nimeacha kusoma sheria lakini hapa kidogo tutakuwa hatuwendi vizuri. Sheria zetu hapa tutaanza kuzipinda pinda, ahsante Mwenyekiti, naomba neno mwanamme liondoke libakie anatakiwa awe Muislamu kwa kuzingatia msingi wangu mwanzo kwamba huyu haombi kazi isipokuwa huyu anateuliwa na Jopo la Maulamaa Waislamu waliobobea. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri sana maelezo ya Mhe. Hamza Hassan Juma zamani akiitwa George Saitoti kuhusiana na kifungu cha 17 (5). Sisi tumekuja na mapendekezo haya lakini kwa kuwa Mhe. Hamza ametoa maelezo mazuri na marefu basi mimi nimuombe jambo dogo tu kama yeye atabeba hii dhima ya kumuondoa mwanamme hapa yeye akikubali kuibeba hiyo dhima na sisi tutakiondoa kifungu hichi. Dhima ije kwako sisi tutakubaliana tukiondoshe hichi kifungu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa dhima wataanza Baraza la Ulamaa kumshauri Mhe. Rais amteuwe Jaji, amteuwe huyu Kadhi wa Mahakama Kuu, basi itakuwa hiyo dhima nabeba mimi na Baraza la Ulamaa niko tayari.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa kwa hivyo tunawahoji hivi hivi kifungu kimekubaliwa pamoja na marekebisho yake. Subirini Waheshimiwa subirini kwanza. Naomba sasa niwaulize maana kuna mambo kupingana hapa Waziri na Mhe. Hamza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, labda kidogo naomba ufafanuzi, Mhe. Waziri alivyotoa ufafanuzi anasema kama nakubali kubeba dhima yeye hana tatizo. Mimi nimekubali kwa sababu nitakuwa siyo peke yangu nitakuwa pamoja na Baraza la Ulamaa waliopendekeza kwamba huyu ateuliwe kuwa Kadhi wa Mahakama Kuu, sina tatizo. Kwa hivyo kama hivyo ina maana Waziri keshakubali na kwamba neno mwanamme liondoke.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningetegemea kwamba kusengekuwa na ujanja ujanja wa kupenya penya. Mimi nimesema *very clear* kama Mhe. Hamza Hassan Juma unabeba wewe dhima sema tu kwamba mimi nabeba dhima tukiondoshe, sasa usiwachanganye wengine, wengine hawamo, hapa tunakuuliza wewe. Wewe unabeba hii dhima tukiondowe, tujibu tu nabeba mimi dhima tukiondoe hichi kifungu. Hilo ndilo swali langu ni dogo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hasan Juma kaa kitako wewe umeshajibu umeshamaliza majibu yako, umeshasema acha tumsikilize Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Machano Othman hakujenga hoja, hakuzuia kifungu.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kujenga hoja wala sitaki kuzuia kifungu nataka kufanya utaratibu wa Baraza. Kwa hatua tuliofikia utaratibu hauwendi hivyo, kwamba huku aseme ajenge dhima au kule Waziri akubali. Tumefikia pahala kwamba hii hoja Serikali bado inashikilia kwamba lazima awe Jaji mwanamme na sisi wengine tunaunga mkono kwamba Jaji awe mwanamme. *(Makofi)*

Sasa twende katika utaratibu wa Kibaraza wanaojenga hoja ya Serikali wanyooshe mikono na wanaomuunga mkono Mhe. Hamza Hassan Juma wanyooshe mikono ili tuangalie nini kinachofanyika.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ibaki kama ilivyo, wanaokubali hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, waliokubali wameshinda.

Kifungu cha 18	Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 19	Mamlaka ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 20	Rufaa

SEHEMU YA TATU
Usuluhishi

Kifungu cha 21	Uwezo wa Kutoa Amri na Maelekezo ya Kumaliza Kesi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 22	Uwasilishaji wa Kesi kwa Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 23	Kazi ya Msuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 24	Haki ya Utatuzi wa Hoja Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tufuate utaratibu, hamuwezi kujibu kabla sijawauliza.

Kifungu che 25	Usiri
Kifungu cha 26	Muda wa Usuluhishi
Kifungu cha 27	Kuondoa Mgogoro Katika Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 28	Mwisho wa Usuluhishi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 29	Usuluhishi Ukishindikana

SEHEMU YA NNE
Masharti ya Jumla

Kifungu cha 30	Kudharau Mahakama ya Kadhi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 31	Ushiriki wa Wakili na Vakili Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 32	Kukubaliwa kwa Wakili na Vakili Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 33	Kinga kwa Makadhi na Maofisa Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 34	Kufutwa kwa Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya mwaka 1985 na Kubakiza Pamoja na Marekebisho Yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wanyanyue mikono, wale wanaopingana na hoja ya Mhe. Waziri. Waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na Kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya 2017

(Kusomwa Kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na kuweka masharti mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa niwahoji Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wanyanyue mikono, wale wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na Kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria wa Serikali uliosomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa hapo ndiyo mwisho wa Mswada wetu wa leo na ndio mwisho wa shughuli zetu za leo. Sasa naomba nichukue fursa hii kuwashukuru pamoja na utulivu wenu lakini mwisho wa siku tumekubaliana. Sasa niliakhirishe Baraza hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:24 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 28/9/2017 saa 3:00 asubuhi)